# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## VERBATIM REPORT OF

# CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, BAHARI CONSTITUENCY, HELD AT ST. TERESA SECONDARY SCHOOL

# ON

# 03RD JUNE 2002

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, BAHARI CONSTITUENCY, HELD AT ST. TERESA SECONDARY SCHOOL ON 3RD JUNE, 2002**

**Present:**

1. Com. Isaac Lenaola
2. Com. Ibrahim Lethome
3. Com. Hon. Phoebe Asiyo

**Secretariat in attendance:**

1. Joash Aminga - Programme Officer
2. Rachel Kitonyi - Assistant Programme Officer
3. Patricia Mwangi - Verbatim Recorder
4. Eunice Kasisi - Sign Language

The meeting started at 10.00 a.m, with Commissioner Lenaola as the Chair.

**Com. Lenaola** - Utuombee, kisha tuwajulishe ni akina nani wako hapa kuwasikiza. Mzee moja atutolee maombi?

**Maombi**- (Name unannounced). Baba mwenyezi Mungu tunakushukuru. Tunakushukuru kwa nafasi ulio patia leo ambayo ni siku muhimu. Siku yakuwa tuna zungumuza juu ya katiba ambayo itakuwa ina tu tawala, ina tuongoza, ina ongoza taifa letu. Kabla hatuja anza mazungumuzo yetu, Baba Mwenyezi, tuna kukaribisha ili mazungumzo haya ikawe Ukiongoze na tuweze kutoa maoni yetu kwa faida ya wa Kenya wote. Baba tunaomba wale ambao hawaja fika hapa lakini wana kuja uwe Una walinda, na Uwaongoze vizuri, mpaka wafika hapa. Tuna omba hayo kwa jina la Kristo, Mkombozi wetu – amen.

**Com. Lenaola** - Asante Sana. Ninge penda ku wajulisha Makomisha ambao wako hapa leo kwa sikiza, na pia wafanya kazi wa tume. Mkono wangu wa kulia niko na mwezangu Ibrahim Lethome, ambaye ni Kamishona, hapa niko na Mrs. Patricia Mwangi, ambaye atakua akiangalia chombo cha kunasa sauti, tuko na Joash Amiga ambaye ni Programme Officer kwa Secretariat, hapa tuko na Rachel Kitonyi ambaye pia atachukua notes na kuandika maandishi. Tuna muongoja mama Kamishona, mama Phoebe Asiyo, atachelewa lakini atafika badaye mchana, na pia Eunce Kasisi ambaye atatusaidia kwa mambo ya viziwi, wale hawajui kuongea, kama kutakuepo, tutakuwa na mtu wa ku interpret kazi yao.

Mimi naitwa Isaac Lenaola, mimi pia ni Kamishona. Kwa hivyo, karibuni katika huu kikao, na kabla sija muita mtu wa kwanza, ninge penda kuwajulisha vile tuta panga kazi ya leo. Jambo lakuanza, ikiwa hauna memorandum yakusoma, uta zungumza tu mambo yako kwa dakika kumi. Baada hizo, kama kuna swali kutoka kwa Makomishona, tukuuliza tu maswali ya ku fafanua mambo yale unayasema. Kama ukona na memorandum, uta angazia yale mambo ambao ni muhimu kwa hio kibarua, na utachukua dakika tano, halafu badaye, tuta kuuluza maswali kama kuna mambo ambayo hatujaelewa vizuri. Halafu, unahaki ya kuongea kwa lugha yoyote, ya kuongea ki Chwonyi, ama Kiswahili, Kiingereza, lugha yoyote. Tuko na watu kutafsiri kama sisi hatuelewi lugha hio. Kwa hivyo, uko na uhuru kuongea kwa lugha ambao unasikia ni sawa.

Jambo la mwisho, tunge penda heshima kwa kutowa maoni. Mtu akitowa maoni, kama huyapendi, mpe nafasi amalize, yako nafasi utapata useme yako, na pia wewe utakubaliwa kusema bila mtu wa kusumbua. Kwa hivio, tungependa kwamba tuheshimiane. Kama hupendi yale anasema, nyamaza tu, mpe mtu nafasi aseme yake, uta sema yako baadaye. Tume agana? Sawa sawa? Haya Asanteni. Sasa tungependa kumuita mtu wa kwanza, naye ni Thomas Nyale. Tuta kuwa wengi na ni vigumu ku.. kwa vile tukona list tiyari, tuna waita tu kwa jina, ukija kuitwa, tuta kujua wewe ni nani. Kwa hivyo Thomas Nyale, jitambilishe, useme wewe ni nani halafu uanze kutoa maoni yako.

**Mr. Thomas Nyale** - Jina langu mimi naitwa Thomas Kiti Nyale. (interjection – many voices at the same time – inaudible) Niko na memorandum hapa ambayo sikuitengeneza kufuata kile ki booklet, maana nilikuwa sija kipata kile kibooklet.

**Com. Lenaola** - Endelea tu na kufuata hio.

**Mr. Nyale**: Okay. Kwa hivyo nina memorandum yangu na introduction inasema. We understand that the Constitution is a statement, outlining the agreed basic principles of formal organizations, ranging from national government to private class.

Here, we are concerned about the constitution of national government named Kenya. We also understand that in general, constitutions establish the structure and purposes of the government. The powers of the officers are too defined. Equally defined is the method to be used in selecting the officers and duration they will stay in the office. The constitution… the Kenya Constitution Review Commission was appointed and given the task of reviewing the present constitution of Kenya because the objectives of the whole exercise of reviewing the Constitution is to come up with the document that all Kenyans will feel as their own and ultimately accept it and value it. The Commission has to seek for the views of wananchi. We believe it is in that context that you are here, you Commissioners. We thank the Commission for providing us this forum.

The following now are our views, opinions and suggestions on the kind of the constitution we would like the Commission to produce at the end of the exercise.

Constitution and wananchi; we want a constitution that will guard and protect wananchi by guaranteeing basic rights to the citizens. Some of these are, recognition of the equality and dignity of all persons, regardless of race, tribe, religion, sect, or social standing. It should, that is the constitution, hold that everyone is equal in the court trials and other legal matters; no one should be above the law, including the head of state. The constitution should provide for freedom of speech, freedom of press, freedom of religion, freedom of association and freedom of movement among others. The new constitution should give powers to the people, unlike the present constitution in which virtually all powers were taken from the people into the hands of the executive. It is our view that wananchi should lave powers over the parliament, and executive, regarding some sensitive issues such as changing the constitution, extending the life of parliament, including salaries and allowances of ministers and members of parliament, granting exemptions to people, exemption to people of certain categories to import vehicles and other items tax free. The constitution should forbid parliament and executive from making decisions on such matters. Instead, such issues should be subject to a public referendum. It is through this public referendum that wananchi can participate and feel, not only recognized, but important as well.

Members of the Commission, whom I believe are Kenyans and were there in 1963, when Kenya became independent, are aware there had been no public referendum. That is not because there was no need for public referendum, there were, and I have given an example here of an issue which should have been subject for public referendum.. referendum, that is mlolongo voting. Wananchi should have been given the opportunity to decide how they will elect leaders. Instead they were forced to elect their leaders by queuing behind and some beat their wives because they voted for people who is their enemies.

Now I come to another one, constitution democracy. We want a constitution, which will promote the good democracy. We know that the constitution should guard against dictatorship and totalitarian government where only a few people enjoy the national cake. Mr. Chairman, we realize that it is not possible practice through democracy such as the one practiced in United

Greece, where citizens of a state gathered at one place and formulated laws. Instead we have settled on a representative democracy. That being the case, we shall therefore be called upon from time to time to elect representatives who will form parliament. We want a constitution that will provide for free and fair elections from level grounds, grounds. Facilities like radio state radio and television should not be a monopoly of certain people or one political party. The constitution should provide a formula, which will curb those with much money to have no advantage over poor people on matters of election. The constitution should fill all loop holes that may allow corruption including rigging so that wananchi are given the chance to elect people of their choice without inducement,. It is only that way, those elected to serve in the National assembly and Local Authorities shall be true representatives from the people.

Nominated MPs. These are not representatives of the people and therefore, according to us, have no rights to speak in the house of the representatives. The loyalty of these people, they are to the people who appointed them. Our views is that the provisions for the nominated MPs and Councilors should be abolished. In need be, we increase six parliamentary seats but there should no nominated MP, nominated Councilor. If that provision is scrapped off, the party that wins with a small number of majorities will be forced to seek the for support of another party so as to increase its strength in parliament, thereby involving more elected persons in the management and running of the affairs of the wananchi.

Gender issues - There has been much talk about women representation in parliament, and other senior positions in the government. Since we are for a constitution that recognizes equality irrespective of sex, among other rights, we do not think there should be a provision which qualification is gender sex. Women should be bold enough to take courage and face the electorate such that fights with their men counterpart.

Independence of parliament - One of the most important measures of the extent to which any parliamentary correct the practice in democratic or dictatorial is the freedom with which the National Assembly operate independence of the executive. The central questions are, who summons parliament? That is who decides, when and where parliament meets, who has the powers to terminate any section of parliament, and who has the powers to dissolve parliament, then who decides what is to be discussed or debated by the National Assembly? The more powers the executive has over such matters, the more dictatorial the parliamentary practice. That is the more operation parliament dependent in the person of the executive, since the executive is bound to call parliament when their interest is not in place. We think parliament should be independent, it should decide before, in calendar, it should draw its own programmes, people should be allowed to submit motions.

**Interjection Com. lenaola -** (inaudible)

**Mr. Nyale –** Okay. Parliamentary and executive, decisions and appointments. The appointments should be subject to parliamentary vetting; should not be left to the executive, because that is …if the appointment is done by the executive, those appointed to positions like the managers to the Parastatals, Ambassadors, Judges, Attorney Generals and so on, their loyalty

would be to the person who has appointed them instead of eh wananchi.

Now, Parliamentary vetting – we feel the president should propose those to be appointed and then send names to parliament, then parliament approves. If there is somebody who is corrupt, has a bad record, parliament will object and parliament represents us. It should not be the case for the executive to decide. We also feel the ministries should be decided by parliament, not the president to decide how the number of the ministries.

Controlling the executive – we feel parliament should control the executive, not the executive to be above the parliament so that whatever parliament does should be ….and that entails accountability.

**Interjection Com. Lenaola –** What is the last item?

**Mr. Nyale** - The last item is Local Government, and I suggested that the powers of the minister of local be trimmed so that Local Authority can have confidence and can work without fear, councilors can work without fear.

**Com. Lenaola** – Hand in your memorandum now, and sign the book, thank you very much.
**Mr. Nyali** – Where do I sign?
**Com. Lenaola -** Right there – thank you very much. Peter Safari.

**Speaker – Peter Safari**

Maoni yangu, Jina langu ni Peter Safari. Maoni yangu ya kwanza kuhusu hii katiba, tuende Kwa wazee, village elders. Village elders, ni watu ambao wana tusaidia, sio hapa peke yake, section nzima. Ni watu ambao wame tegemewa, ndio grass root, ndio wako kwa committees kuanzia sub chiefs, machiefs na kuendelea. Maoni yangu ni kuwa tunataka constitution ambayo ita allow hawa village elders pia kuwekwa kwa payroll ya serikali. Walipwe mshahara wa encourage. Tuna pata ni watu mahali popote pale wako, ndio wanafuluhisha mambo ya watu wa ule mtaa, ama pale mahali kila siku. Kwa hivyo waki wekwa kwa payroll, bila shaka mambo hayata enda kombo, ita kuwa sawa sawa.

Oni la pili – uhuru wa masda wetu ya shambani, mazda mnazi. Mnazi ni mti ambao ume tusaidia sana. Tuna pata baadhi yetu sisi, hasa watoto hapa tumesoma na huo mti. Kwa hivyo, ninge onelea, pia mnazi upewe ule umuhimu, ufunguliwe vilabu, na utafiti ufanywe ile tuweze, hasa sisi wakaaji wa hapa pwani, tufaidike nao, angalao tujaribu ku toa huu umaskini ama ukoso wa elimu tuko nao.

Oni la tatu, ninge onelea tuwe na serikali ya mchanganyiko, **Coalition Government.** Kwenye hii serikali, wanchi wapewe pia nafasi ya kuchagua makamu wao. Wakienda wakichagua kama ni mbunge, diwani, president, pia kuwa na ile nafasi yakuwa naweza kupigia kura pia makamu wa rais. Asanteni.

**Com. Lethome:** Umesema kuwa mimea ya huku pwani iweze kukamilika. Umetaja tu mnazi peke yake. Hakuna mimea mengine ambao unge penda kuyatambuliwe huku pwani?

Peter; Kuna mikonge hapa pia. Ikiwezekana kuletwe kiwanda. Ule mikonge tukiona tumeletewa kiwanda ita tu encourage, kuzidi kupanda kwa wingi na tufaidike.

**Com. Lethome.** Na korosho na pamba

**Peter**: Pia uwe moja wao. Pamba na mengineo.

**Com:** Mathias Dena

**Mathias Dena:** Jina langu ni Mathias Dena. Asante sana ya kupata hii fursa ya kutoa maoni. Lakini it is unfortunate kwamba whatever I had intended to speak already imekuwa covered na ile memorandum ambao imeshaelezwa maoni. Kama kwamba nikiongea, itakuwa ni repetition of whatever I had said. Thank you.

**Com. Lenaola:** - Alex Munga

**Alex Munga:** - Kwa majina naitwa Alex Munga. Na ninge penda kuchangia hasa katika katiba yetu hii, ambapo kutoka zamani kime kuwa ikiendelea ilikuwa ni ya chama kimoja, na wakati tulikuwa wadogo, tume kuwa katika hali hio ambapo serikali ilikuwa ni chama chake kimoja. Kwa hivyo ilikuwa inaendesha mambo yake ambayo wengi walikuwa hawapendelewi lakini walikuwa hawawezi kujitetea. Manake walitumia kila njia kuhakikisha kuwa lolote lili linaongewa, liliwe naenda sawa na vile wanvyo taka wao.

**Com Lenaola:** - …unapendekeza.

**Mr. Munga:** - Sasa ninavyotaka mimi, ni kwamba tunataka na ule uhuru wa kuzungumza. Kila pahala utakapo ingia katika ofisi ya serikali uwe uta ruhusiwa na usikizwe maoni yako yale ambayo yame kupleka pale.

Na jambo lingine ambalo nina taka ku sizitiza ni kwamba kuna hii hali ya kumiliki mashamba. Hii ni hali ambao kwa muda mrefu sana hasa hapa pwani tumekuwa na matatizo sana. Na matatizo yenyewe ni kwamba sisi wenyeji tumekaa, tuko mahali ambao tune jua tumezaliwa hapo hapo. Lakini kuna semekana kuwa hapo mahali sisi hatuna uhaki nako mahali. Kwa sababu, bado hatujapata ma title deeds na hatuja horodheshwa katika afisi za lands ijulikana kuwa sisi hapo mahali tuko haki tunapoishi.

**Interjection**: **Com: Lenaola** - (inaudible)

**Mr. Munga:** Sasa tunavyo taka ni kwamba serikali ifikirie sana, kuhakikisha inarekebisha zile sehemu ambazo zili kuwa zina vunja watu wengine kwa upande wa mashamba. Ili hata sisi pia tujue tume kaa, tuko Kenya, na tuko na uhuru wa kuishi mahali ambao tunajua tuko kwetu, tunafanya kazi zetu, na hakuna mtu mwingine yule anaweza kutia tisho hapa mahali wewe unastahili kukaa. Kwa hivyo sehemu kama zile ambazo zilikuwa zumechukuliwa na wazungu tuseme kama shamba hili kubwa hapa ya makonge ni sehemu ambayo ilikuwa pamoja na zile shamba kule kwetu wenzetu bara, zilikuwa zime kombolewa zikagawisa wananchi. Lakini tuli, tuna shangaa kuona kwamba hili shamba bado imechukuliwa, na hakuna mtu ambaye ana, ana jiufisha. Na, wale ambae wanajiufisha hawapewi hizo nafasi ya kuwa wanaweza ku shugulishia hizo shamba. Kwa hivyo tuna taka kama ilivyo fanya kule kwa wenzetu kule bara, kuchukua pasa ambazo zinachukuliwa kwa fadhili, na kuwalipa wale wenyeji wazungu, kwa hivyo wafanye huvyo hivyo pia ili hii shamba iwe ita chukuliwa na ku gawiwa wananchi ndio itaondoa hili jambao la maskota. Kwa hivyo, kwa hayo machache, nasema asante.

**Com: Lenaola**: Asante sana. Michael Karisa Kahende

**Michael Karisa Kahende**: Asante sana. Mimi kwa jina naitwa Michael Karisa Kahindi. Ninayo matatu hapa ya kuzumuza. Mwanzo nataka pendeleo ya kwangu ni serikali ya Majimbo kwa sababu kusema hivi, tangu tuweke hu ufumo ya serikali ya chama kimoja,sasa tumeteseka sana wafanyi kazi wa huku pwani. Mara tuna mambo ya makazi hatupati. Hata uki angalia mambo ya mimea, tuna jilimia huko kwingine ambazo sasa kama mnazi. Kuenda hupo vipingo au wapi, serikali ina tu nyanyasa. Tuna shikwa na tuna fungwa. Kwa hivyo pendekezo langu sana tuwekwe katika Majimbo na tuweke sisi wenyewe wajumbe, sisi wenyewe, ambao hata baada huo Majimbo, tuna weka wajumbe baadaye tuna weka governor, halafu sisi tutakuwa hapo tuwe sisi wenyewe huku pwani.

Na kuongelea upande wa kazi pia sisi kazi tuna nyanyasa sana. Wengi sana hatuna makazi huku kwetu. Wote wamechukua watu wa, wa juu. Sasa upendekezo wangu kwamba, sisi wenyeji huku kwetu tuwachiwe huo nafasi za kazi. Kwa hayo machache nasema asanteni.

**Com: Lenaola:** Umesema kazi zote katika jimbo liwe kwa pwani ama sili mia fulani ya makazi ya wachiwa watu wa humu?

**Mr. Karisa:** Asili mia fulani.

**Com: Lenaola:** Kama gani?

**Mr. Karisa:** Kama tuseme mahotelini.

**Com. Lenaola:** Asili mia?

**Mr. Karisa:** Asili mia kubwa iwe ni ya hapa, wengine ndio wametoka nje.

**Com. Lenaola**: Taja tu, sabini, sitini….

**Mr. Karisa**: Sabini na tano.

**Com: Lethome –** Umesema kuwa kwa muda mrefu mume kuwa china ya chama kimoja, na sasa wataka Majimbo. Ninge penda ufafanue hapo, siku fahamu vizuri. Mume kuwa chini ya serikali ya umoja, ama tume kuwa chini ya chama kimoja?

**Mr. Karisa**: Tume kuwa chini ya uongozo moja hapo zamani. Sasa ule ufumo wangu nina taka tuwe na Majimbo, tuwe tuna jitawala sisi wenyewe.

**Com: Lenaola:** Francis Mbwana

**Francis Mbwana –** Nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kutoa maoni…

**Interjection Com: Lenaola –** Sema jina lako

**Mr. Mbwana –** Mimi naitwa Francis Mbwana. Kulikuwa kuna mwenzangu tume panga aje atoe maoni lakini bado haja aja. Mimi ndio nita toa kidogo. Kwa kusema kweli nita angalia wakati wa nyuma tulikuwa na chama kimoja na ilikuwa kina tugandamiza sasa. sana. Lakini sasa vilipo kuja vyama vingi, tume ona sasa tuna nafuu kidogo. Kwa hivyo, ninavyo penda mimi ni kwamba tuna taka tuwe na vyama vimbi ili wale wanyonge wasi gandamizwe. Pia nina unga mkono upande wa mnazi. Tuna pata shida hatujui tupeleke wapi mali yetu. Tuwekewe mahali pa kuuza mnazi hapa, hapa Chwonyi, kwa jumla pwani. Tuna omba serikali ituangalie na sisi hatuna kazi. Watu wengi wako nyumbani, mashamba pia yana shida, ukikaa hapo unaambia si kwako. Pia tunaomba serikali ichunguze sana kwa sababu wale ambao ni wanyonge hawana kitu ndio wana gandamizwa. Mara undondolea utakwenda wapi, unawacha mali yako pale. Kwa hivyo ninaomba serikali ituangalie sana shida zetu hapa pwani, upande we kazi, na nazi sijui tuta peleka wapi. Pia kuna michunguwa, mananasi. Tunaomba serikali utusaidie sisi wanyonge ambao hatuna kazi. Sina zaidi.

**Com: Lenaola -** Asante sana, jiandikishe pale. Donald Ngala

**Mr. Donald Ngala Mwananje**: Asanteni kwa kupewa ananfasi. Kwa jina naitwa Donald Ngala Mwananje. Kwanza nina furahi kupewa hi nafasi kutowa machache ambao labda yale ambao labda mengi wezangu wame zungumza, nataka kuweka

mkazo. Hasa jambo hili la mnazi na mamiti hapa pwani. Mnazo na mkorosho ndiyo vitu ambao ni cash nut crop yetu hapa. Hii inaonekana ime sahauliwa sana. Ime sahauliwa hivi kwamba hata factory ziko nao za mkorosho zime kufa, hazifanyi kazi, (inaudible). Sasa imekufua kabisa. Mtu inaitwa mnazi ambao hata mnaona hapo nje mti una faida nyingi sana. Kunayo makuti, kuna fagio, kuna tembo ambao unatoka kwa huu mnazi, ni tembo safi sana, ina leta ulinzi, ambao hata labda inashinda zile tembo za bia ambao tuna pisha mbele zaidi. Nchi zingine huko mna zunguko huo utafiti mpaka unapelekwa sehemu zingine ambapo watu wana pata pesa. Lakini hapa kwetu una kuta tuna finywa sana, hasa hapa kwa ma administration. Sababu nina jua kwamba ile Act,

**Interjection – Com: Lenaola-** Upendekeze mnazi ..

**Mr. Mwananje:** Nina pendekeza kwamba mnazi huu ukiitwa manazi ufanyiwe utafiti kama nchi zingine, na huo utakuwa manufaa kwetu, isiadie wale wanao ishi hapa.

Jambo langu zingine ni administration, hawa watu waitwa ma DO, ma Chiefs, Assistant Chiefs, ni watu ambao wana dhulumu watu sana. Na ninge pendekeza, kama hawawezi kuondolewa kabisa basi wafanyiwe uchaguzi kama madiwani, na wambunge. Ni kwa kufanya hivio ndio tutakuwa na fasa zao vizuri. Sababu nina kumbuka, kuna wakati Assistant Chief, kuna wakati amechukua kazi, kazi, hana pesa, ata ngonjea mnazi huko awapokonye pesa the next day ana enda kulima na tinga tinga. Watu kama hao hawatufai kabisa. Kama haiwezikani, kwamba wasiondolewe kabisa, mara machief sasa wafanyiwe uchaguzi kama wana siasa.

Uhuru wa vyama. Tuna jua hapa tuna vyama vingi sana. Lakini utapata chama kimoja pekeyake ndio kinapewa uhuru zaidi hata kufanya mkutano. Utapata vyama vingine wakitaka kufanya tena wana angaishwa sana. Na kwenye katiba kila chama tuupe uweza ku kutana wakati wowote vinapo taka. Sio lazima wachukue permit kwa mtu yeyote.

Jambo langu la mwisho ni ku teuliwa kwa mabunge na madiwani. Hawo watu wanao teuliwa hua hawanan kazi yoyote, hawa wakilishi mtu yeyote, isipokuwa labda kwa wale ambao wame chagua. Kwa mfano, ukipata diwani ambae ni wa kuchaguliwa, nominated, akua kule kwa custody. Basi hata kama ni, kupatwa kura kura, afika tu pengine ataambiwa na DC wewe piga pande hii. Kwa hivyo hata kuwahafanyi hio kwa maoni yake, isipokuwa ni kama ambaye ana lazimishwa. Kwa hivyo wata hawa hawana umuhimu kabisa, ndivyo nataka hawa waondolewe kabisa. (inaudible) Kwa hivyo kwa hayo machache, nasema nashukuru tena kwa kunipa nafais hii, asanteni sana.

**Com: Lethome –** Bwana Mwananje, umesema vyama vingi vidumishwe. Viki ongezeka vibaki hivyo hivyo viko vingi?

**Mr. Ngala –** No, kama vinne vitano hivi nafikiri five.

**Com: Lethome –** Uta tumia style na njia gani kujua hizo tano?

**Ngala –** Sasa, kusema kweli, huko nchi zingine, nafikiri kuna vyama vinne ama vitatu. Na kama wale wanatumia njia hio, kwa nini hapa Kenya haiwezekane, ile njia wanao tumiwa na wenzetu kule nje, kuweka vyama vitatu, hata sisi pia tufanye hivyo. Tu copy kutoka kwa watu wengine huko.

**Com. Lenaola**: Bwana Ngala (inaudible) Unge penda serikali aina gani?

**Mr. Ngala**: Serikali ya mseto

**Com. Lenaola**: Stanley Mwagambo

**Stanley Mwagambo**: Kwa jina ni Stanley Mwagambo. Kwanza ninge anza kugusia kuhusu mimea. Mimea yetu ukosefu wa kuweka Board au kuchunguza zaidi juu ya hizi mimea na mpangilio maalum ndio imetuletea umasikini mwingi sana. Kwa mfano tuna mnazi, mikorosho, tunayo mziksa, tunayo miwa pia tunayo mingi hapa pwani. Lakini hii yote zime puzwa mapka viwanda vingi vime fungwa. Na hii imaleta umasikini mwingi. Unajua sisi tuki zungumuza habari ya mnazi, tuna sema mnazi ni ule wa kunywa. Lakini mnazi sio kunywa. Watu wengi, hawaanywi mnazi. Sio wote wana kunywa mnazi. Lakini mnazi, au faida ilio na mnazi ni kubwa sana hata kama vile kule bara wana ita mkahawa. Hii kama inge patwa vizuri unge leta utajiri mkubwa sana hapa. Lakini unaona kwa ukosefu wa upangilio mzuri kwa huu mnazi au miti yetu mimea yetu, mpaka sasa watoto wengi hawasomi, umasikikini ume jaa. Hata hivi sasa, watu hawaoni faida ya kusoma ni nini. Mara mtu ata some afike mpaka form four hata zaidi, kisha aje tu ku randa, randa bara barani. Hakuna kazai. Lakini kama ni nazi inge wekewa, au mimea inge wekewa viwanda, watu wange pata kazi na wange ona faida ya kusoma. Sasahivi unaweza somesha mtoto wako wewe mpaka form four. Tazama huko nyuma una kama watatu wawili wanao mfuata. Huyu ata kwenda hana kazi, na wale wengine wana kuja ni wewe uwasomeshe, huna kazi ya kufanya. Kwa hivyo, kama inge kuwa yule mkubwa ange pata kazi, ange rudi kusomesha hawa wenzake kuwasomesha. Lakini wewe peke yako, unasomesha, kufika standard, form four, ule mtoto ana lala chini. Ni wewe tu una vuruta, na akifika pale form four una shindwa mpaka una warundika nyumbani kama tano hivi hawana kazi wote. Kwa hivyo hii umeleta umasikini kubwa sana. Mimi ninge pendekeza viwanda vijengwe na kuwe na kuwe na Board ya kudumisha hii matunda yetu, au mapato yetu ya nchi.

Kitu kingine ni mashamba. Mashamba, tuna ambiwa tuna himizwa sana. Nende mjiandikishe mpate title deeds, mjiandikishe mpate title deeds, hivi sasa niki kwambia karibu sote tuna kila mtu ana title deed yake. Na ukienda benki kuomba mkopo, hupewi kabisa. Hupewi, ukipewa labda shillingi elufu arubaini, mwisho. Shilling elufu arubaini utafanya kitu gani shillingi elufu arubaini? Tuna taka tukienda benki una toa title deed yako, unapewa million na kitu, ndio unweza kufanya kazi, sio shilling mia nne eluf. Hii unaweza kufanya kitu gani. Kwa hivyo uta ona kuwa title deed tunazo nyingi lakini hazi tufai kitu. Mimi mwenyewe nina mbili tatu, na sasa sina chochote. Hata nikienda benki nilipo enda mara ya mwisho, nilipewa shillingi elufu

ishirini. Shillingi eluf ishirini, hata sasa nikienda ita nisaidia kitu gani? Niki enda tena nina ambiwa ngoja, ngoja, ngoja, na ukisikia pahali imetoka pesa, hizo hakuna. Kwa hivyo, hizi title deeds, tuna zichukua kweli lakini hazi tu fai hapa.

**Interjection Com: Lenaola –** Munge taka nini?

**Mr. Mwagambo** - Tunge taka, ikiwa wange abiriwa hawa mamanagers, maana ukienda uta sungumuza na managers. Managers, huku kwetu hatuna managers wa bank. Na ukifika kule uta ambiwa mambo mingi ambayo haya wezi kufaa. Kwa hivyo wale mamanagers, kama wange ambiwa kwa waweze kuwa wata saidia kila mtu, wange fanya hivyo. Lakini sasa inaonekana kuna upungufu, yani kuna mambo mengine ambayo yana fanywa sio halali. Ndio, tuna enda sisi, hasa hapa pwani; Mimi naona ni hapa hatupati mikopo. Mikopo tukipata tuna pata pesa chache sana, shillingi elufu ishirini, ikizidi sana, pengine mia moja elfu, hii huwizi kufanya kitu. Utaona hapa sasa, watu wanaleta matractor kutoka bara wakilima hapa, maana wale wakienda banki wana pewa pesa nyingi; pesa ambao unaweza kuenda kuchukua tractor, moja akalete. Lakini wewe unapewa pesa hizi ndio utakuwa wakukodesha tractor kila wakati tu, kila wakati kodesha tractor. Na huwezi kodesha. Acre moja, shillingi elufu moja na mia tano, kila mwaka utafanya hivyo, uta fanya hivyo, unamtajirisha yule mwenye tractor. Kwa hivyo, hatuoni maana ya kuwa na hizi title deeds, kama wange kuwa tuna, zina fanya kazi, basi zifanye kazi kila mahali.

Na kitu kingine ninge ona, kwa vile nimeona mambo haya yote yanatokea ni kwamba ni kwa ile serikali ya kuwa pengine nchi yetu ni kubwa, na ile serikali ikiwa kule Nairobi, inaonekana inasahau sehemu nyingine, nyingine. Sisi tume sahauliwa. Kama inge kuwa tuna regional serikali hapa, jimbo la serikali, serikali moja iweko, lile kubwa, lakini, kama tunge kuwa na serikali mengine sehemu, sehemu, nafikiri tunge kumbukua zaidi. Lakini inaonekana tume sahauliwa zaidi kwa kuwa nchi inatawaliwa kutoka mbali uko halafu sisi tuna fananywa ku agizwa, fanyeni hii, fanyeni hii, fanyeni hii, kuingine tuna sahauliwa.

Ikija employment, si kuwa Kenya haina kazi, au pwani hakuna kazi, kazi zime jaa nyingi. Tunao mahoteli, tunayo bandari, tuna vitambuliza, lakini inaonekana sehemu nyingi hata ukifika pale, kazi zime chukuliwa na watu wa pale. Sisi hatuna kazi. Na sikuwa hakuna kazi. Uki enda hapo port…..

**Interjection -Com: Lenaola**- Unataka namnagani?

**Mr. Mwagambo**. - Nina taka, hata kama watu wata andikwa kusaidika, tupate majority kutoka hapa. 80 percent. Asili mia thamanini itoke kwa region, wengine watoke nje, ndio tunaona tumaliza hii mashaka ya watoto kuzunguka. Ukifika barabarani ime jaa, ma fees hakuna. Hii umasikini ume zidi zaidi, hata tuki sungumza umasikini, hapa pwani ndio kwao, masikini.

Administration – Administration kama vile unavyo ona kuna machifu, kuna ma sub chifu, ni siku hizi wame punguza, punguza kidogo, lakin nikuambia kwamba administration ya hapa, huwezi kwenda kulalamika kwa chifu, au kwa DO bila kulambwa, kulambisha kwa kitu, huwezi. Wewe ndio umeingiliwa kwako nyumbani upigwe usiku, ukienda kule kwa DO anakwambia towa shillingi mia tano tuka chukue mafuta, tutie gari. Hatukuona hivyo, wakati waukolonia. Wewe ume umizwa mpaka ume

katwa katwa, mtu anataka kupelekwa polisi, polisi ukifika unaambiwa toa elufu mbili tukatie mafuta. Hii itatokea lini, na mimi nime pigwa kwa sina hata nduru nyumbani, nita peleka wapi malalamiko. Ukienda, toa pesa, kila pahali toa pesa, toa pesa. Na watu hawana pesa.

**Interjection - Com. Lenaola** - Mapendekezo …

**Mr. Mwagambo –** Ndio naona kama hatuta weza kuweka watu hawa basi tuwapungue, ili badala ya kuwa na chifu, sub chifu hata DO, tunge kuwa tu na hawa wazee ambao wata lipwa, wazee wa mitaa ambao wata lipwa, lipwa hivi, hivi; kama jambo likishindwa kwa wazee tunaenda polisi maramoja. Tuna fanya wazee wa mitaa. Kila kitu ikifanywa na wazee wa mitaa ambao wana lipwa, liki washinda wao wazee, hakuna haja ya kuenda kwa chief, hakuna haja ya kuenda kwa DO, hakuna hata kwa sub chief, ata kufanyia nini? Tuendeni kwa polisi mara moja. Kwa hivyo hawa wengine, nafikiri maneno haya yaondolewe. Asanteni.

**Com Lenaola –** Japheth Mwango

**Mr. Japheth Mwango –** Kwa jina naitwa Japheth Mwango. Nashukuru kwa kupata fursa hii. Ninge penda katiba, maoni yangu ya kwanza, ninge pendekeza Katiba ile ita pendekeza serikali ya Majimbo. Oni langu la pili, ninge pendekeza katiba iwe itapendekeza mti huu wetu wa mnazi iwekewe Board kama kule kwa wenzetu bara, kama ule mimea wa majani chai, mkahawa. Na oni langu la tatu, hasa kwa upande wa administration. Ninge omba kama katiba ita pendekeza hasa kwa upande wa wafanyaji kazi, ikiangalia population ya Kenya ni kwa juu na serikali mpaka sasa bado ina pendepeza mtu anafanya kazi kwa serikali muda kama miaka arubaini ama hamsini. Kwa hivyo ninge pendekeza, ninge penda katiba kama iki wezekana, mtu akiandikwa kwa administration, ama kwa serikali iwe ita pendekeza andikishe miaka kwa wale walio nyuma nao pia wawe ata pata muda wa kuajiriwa na kutengeneza kile mtu ana taka. Sina zaidi.

**Com: Lenaola** - Ume sema kwamba miaka ya chini ni miaka ngapi?

**Mr. Mwango -** Ni kama miaka ishiri na mitano mpaka thalathini.

**Com: Lenaola –** Kwa kazi …

**Mr. Mwango –** Yani upande yote yani kazi yeyote.

**Com. Lethome –** Una maanisha mtu akifika miaka thalathini ana staabu?

**Mr. Mwango** - Eh, a staabu kwa vile sasa (laughter) kwa vile una ona uchumi wa Kenya ime kuwa na inflation ya juu,

wengine ni sisi hatuna kazi na tuna tarajia kufika miaka thalathini, hata arubaini unatarajia.

**Com. Lethome** - Uko na miaka mingapi?

**Mr. Mwango** – Mimi sasa hii nikona thirty two.

**Com: Lethome** - Kwa hivyo, hufai hata kuajiriwa kazi?
(Laughter)

**Com: Lenaola** – Haya asante. Winston Ngala. Useme jina ndio…

**Winston Ngala** - Jina langu ninaitwa Winston Ngala, natoka ziani location. Na niko na maoni haya kuhusu mabaliko ya katiba. Kwanza kabisa, mimi hufurahia serikali ambayo ina chaguliwa na rahia wenyewe. Na uchaguzi usi simamiwe na serikali ambayo ina maliza mamlaka wakati wauchaguzi. Ninge penda ikeiwezekana, hatuna haja ya kwamba tuleke wajuzi kutoka nje wasimamie kura, hapana. Tunao wenye ujuzi wengi wa kutosha, bora tu kila mukowa, uwe katika ile Commission ya uchaguzi wakati wa uchaguzi.

Jambo la pili ni kuhusu rasilimali za nchi hii. Kwanza ninge penda kuongea kuhusu mambo rasilimali za pwani kwa sababu mimi mwenyewe ni mkaaji wa hapa pwani. Tunajua ya kwamba sisi tumebarikiwa tuna port hapa. Katika nchi nzima ya Kenya, kuna kakiport nusu tu Kisumu lakini port yote iko hapa Mombasa. Na ni jambo la kustaajabisha kwamba hata nyinyi Makomishona wakati mume kuja hapa kama huu mkutano munge weka gombeni haamunge fika kwa sababu barabara hatuna. Na tume kuwa na uhuru tangu mwaka sitini na tatu nikiwa na macho yangu hivi. Kwa hivyo, mapendekezo yangu ni kwamba asili mia zingi za rasimilimali zote za kila mukowa zirudishwe huko, zika weze kuwanufai wale ambao wali achiliwa kuridhi na wazee wao. Kama sheria ya kimungu inazo ruhusu.

Pia kuhusu hizi rasilimali, kuna mambo ya kimaendeleo kama zile uchimbaji barabara, hata mahosipitali, tunataka serikali ambao itachaguliwa, baada ya hii sasa, ihakikishe ya kwamba hospitali ni majibu wa baba wa nchi ambao hio ni serikali ilio mamlakani. Habari ya kuambia mimi nika lipe pesa hospitali na mimi sina kitu, yani kuni condemn kabla Mungu haja chukua roho yake hio ni watakata humo. Lakini sio ati kuambiwa wajilipie. Kule wenzetu wame jistawi wana ingia masecondary, manational schools, sisi hapa tume kaa hivi tuna zunguka tu. Uta staajabu kwamba hata kazi za hapa kuna wengine hata kuna wengine we degree wame keti nyumbani, na ukienda kwingine, huta wakuta watu kama hawa. Kwa hivyo nina taka ugawanyiko wa natural resources, ya asirimali ufanywe ki halali. Kama tunge pata tu hata asili mia sitini hio ya port hapo, pengine million sitini kwa mwezi, sisi tunge kuwa wapi, hatunge kuwa vile tumekaa.

Pia ninge penda kwenda mahali pana itwa Provincial Administration, ile power. Ninge taka ule nguvu walio wachiwa mamlaka

raisi upunguzwe sana. Sana zaidi, kiasi ya kuamba yeye asi chague Commissioner yeyote, pili, asi chague PC, tatu, asi unde Commission. Pia ninge pendelea kwamba, raisi yeyote atakapo kuwa mamlakani, baada ya kumaliza wakati wake, kama ali fanya makosa, ashtakiwe. Ili kama aliye ali fanya kasoro irekebishwe ndio wale wanao kuja baada ya yeye, wasi rudie mambo ambao yametendekea. Hivyo tuta jaribu kupunguza upikaji. Kuhusu hapo, hapo, kuna kitu kimoja kinaitwa Sessional paper number 1986. Hio paper hio ikiwezekana hii Constitution inge likiri kabisa hio paper isi fanye kazi. Kwa sababu kisa hio ndio ili leta Pwani kubaki nyuma. Wakati tulilikuwa tukiendelea sawa, sawa katika ilikuwa nafikiri single party wakati huo, tulipo kuja..

**Interjection – Com. Lenaola** Jina la hii paper inaitwa ..

**Mr. Ngala –** Inaitwa Sessional Paper number 186, ibadilishwe kabisa hata, na ninge pendekezwa ifutwe. Maana hio ndio ime leta umasikini pwani. Wakati ilisemekana lasirimali zigawane kisawa kwa kila mukowa na kila wilaya, wale waio tumwa kuja kusimamia huku, walikuwa wana toka huko, kwa hivyo hawakuweza kupinga kwamba hatupati lasirimali zetu kisawa. Sasa sisi hatukufanyiwa lolote, tume kaa tu tangu 86 hatuna maendeleo yote. Kwa hivyo ikiwezekana hilo karatasi itupiliwe mbali ili mambo mengine mapya yaweza kuletewa.

Pia ikiwezekana, kama Katiba inge ruhusu, nafikiri hatuna haja ya kuwa na District Commissioner. Kama tutakuwa na mbunge, hatuna haja ya kuwa na District Commissioner, kama tutakuwa na mbunge, hakuna haja ya kuwa na D.O. Kama tutakuwa na Councilor, hatuna haja na kuwa na Chief. Kwa hivyo hawa wawekwo, ikiwa ita wezekana basi ma Councilors wa ondolewe, tubaki na hawa ma D.O. Lakini kama ma DOs watakuweko, hio Constitution, kama inge kuwa uwezo wangu, mapendekezo wangu ….

**Interjection – Com.** (inaudible)

**Mr. Ngala-** Waondoloewe. Pia, kuna retirement benefits. Una jua kwamba rahia wa Kenya ni masikini, kulinganisha na nchi zingine. Basi ikiwa wewe ime andikwa kazi na masikini, na karibu kufilizika, hata anashindwa kulipa watu wake pesa, halafu mwisho mna aambiwa mlipwe pension, uta weza, mshahara ina kushinda ulipe pension? Kwa hivyo hii mambo wa kusema kwamba rais aki retire apewe mimi nina ona hayatusidii.
Kama inawezekana, hio pension iondolewe, hakuna haja ya kulipwa pension. Sisi tunateseka, chakula hakuna tunalipa pension ya nini.? Mambo yakiwa mazuri, pengine katiba ije igeuzwe baadaye, lakini kwa sasa, hio, afadhali inaweza kuwa (inaudible -noise).

Halafu kuna Judiciary, ambayo ni mambo ya sheria, sheria hii. Kwa upande huo mimi maoni yangu nafikiria ma jaji kuwe na commission ambayo ina chaguliwa na mbunge ambayo inapendekeza Chief Justice, ambaye wale majaji wote wanafanyiwa interview, kama zile za Public Service Commission, ili kusudi akipelekewa kesi, aamue akijuwa kuamba waandishi wangu ni

rahia. Lakini aki appointiwa na mtu tu, basi vile atakapo ambiwa na huyo mtu ndivyo atakavyo fanya. Kwa wao huwa saa ingine, hawatuamuingi sawa, kwa sababu wanao kile kitu kinaitwa kiingereza, allegiance, yani uwa wame shikiliwa humu na force fulani hivi. Kwa hivyo, hawana ule uhuru. Utakuta kesi yako wewe kesi ya ukweli umebadilishwa hapo halafu kiisha una kuwa una appeal, huna pesa za ku appeal. Ukiwekewa ma appeal, wanataka million tatu, utaweza, na wewe ni masikini. Kwa hivyo, wachaguliwe, I mean, sorry wasi chaguliwe, wafanyiwe interview. Mwenye ana qualify aandikwe kulingana na ujuzi wake. Halafu sasa,

**Interjection: Com.** Dakika mbili.

**Ngala –** Oh ni dakika mbili. Sasa kitu ambacho ninge penda kifanyike ni kwamba waziri wote walio husika katika ufisadi Constitution iseme washittakiwe. Warudishe pesa za ume, tufanye maendeleo tuone tuta fika wapi. Na, la mwisho ni kuomba tu kwa sababu unajua bila kuweka Mungu mbele na shukuru mambo yetu kufanikiwa, maani hali yetu imekuwa mbaya sana. Sasa, katika makomitii wale ambao wata chagua, wale wa mbunge basi iwe kuna wa dini ndani yake. Maanake wale wadini hata kama wanafanywa ufsadi hufanya kisha wakawa na haya kidogo. Hayo ndio maoni yangu.

**Com. Lethome –** Swali moja, umesema tunapo ingia katika uchaguzi, serikali inaye toka isisimamie uchaguzi. Kwa maana ikiwa mbunge likivunjwa, serikali nae ivunjwe. Si ndio? Sasa ninani atakae simamia nchi wakati huo wa uchaguzi? Nataka upendekeze.

**Mr. Ngala:** Kuna mtu ambaye huita Solicitor General. Mimi nafikiria huyo, na kama hiyo katiba pia vile nilivyo pendekeza mimi ime kubali kwamba hawa majaji wa apointiwe, sorry wafanyiwe interview, basi ipitishwe kwamba yule jaji mkuu kwa ule muda kama ni ninety days siku tisini, ama ni ngapi, ashikilie, na kama sheria isimruhusu kuendelea hata siku moja zaidi ya hizo siku.

Com. Lethome – Na inamaana ya kusema serikali isi simamie, kwa kuwa kuta kuwa na District Commissioners, kama watu wengine, wasimamizi wa serikali wote waache kazi kwanza, wasi shughulishe na uchagusi kabisa?

**Mr. Ngala.** Wasi huzike na uchaguzi kabisa.

**Com. Lethome –** Na kama tunataka usalama utasimamia na nani, polisi wanaweza kusimamia usalama wakati wa uchaguzi, ama wao pia tutawaona kama chombo cha serikali?

**Mr. Ngala.** - Sioni ubaya wa kuwa waskari wasimame pale watu wasi pigane. Kura nita piga mwenye pale ndani. Bora tu asi influence.

**Com: Lenaola –**Asante bwana Ngala. Eric Kahanga Mwanje

**Mr. Eric Kahanga Mwanje -** My name is Eric Kahanga Mwanje. Eric Kahanga Mwanje. I have made some few points in my memorandum.

**Com: Lenaola** - Just highlight the most important points.

**Mr. Mwanje** - Constitutional primacy – We should not have the 65 percent majority votes if any change or amendment to the constitution to be placed by national referendum, pending on approval by regional assembly. The parliament also to have of its representative. The Parliament should not have powers to amend any part of the constitutional before consulting the public. If like MPs not to increase their salaries. Number 4, If any part of the constitution, the Review Commission should be appointed to conduct the referendum.

Citizenship. Automatic Kenya citizenship applies to children born by both mothers and fathers being Kenya citizens, by ID. The Constitution to define the rights and qualification of the citizen. All citizens should be abide by the constitution. No dual citizenship - ID and Passports.

President: President should be properly married, should declare his wealth, should have sound health, age should be between forty to seventy years. Kenya, citizen by proper birth. Education – he should have a degree from a recognized university. Prime minister, should be Chief Executive, and should be between 35 to 65 years, others as above the president.

**Inaterjction: Com. Lenaola -** Age of prime minister…

**Kahanga** – Age of prime minister ?

**Com**. **Lenaola** Yes.

**Me. Kahanga** – should be 35 to 65 years. The others as above on the president. President tenure, should be fixed to two terms of five years each. Should declare his wealth. Prime minister should be fixed to two terms of five years each.
Ministers and Cabinet. The president should appoint the cabinet – the president should appoint the Cabinet but to be with his prime minister, not alone. The Cabinet should be appointed to their lines of qualifications. Officers to be appointed by their selected Committees.

**Interjection – Com. Lenaola** Two minutes.

**Mr. Kahanga** – Two more minutes?

**Com. Lenaola**: - I told you to highligt the most important points, for we shall read that. Tuta isoma, kwa hivyo, usitaje neneo kabisa.

**Mr. Kahanga –** Okay – Regional Government. 75 percent Revenue to remain in the Regional Government and 25 percent in the Central government. The government to be alo…the Governor to be a local man and be selected by their local people. All employment in the region to be given to the local 80, percent per-se, or otherwise. Administrators to be the locals in the regional government. Education to be managed by Central Government, security and all national resources to be managed by the Regional Government for the benefit of the local people. All public institutions to be managed by the Central Government and every region give a quarter. Primary education to be free and free basic health care.

Land Commission – Our property to be controlled by the Regional Government. Local Government. Mayors and Chairmen of their Local Authorities should be elected by their
locals every after two years. The councilors as above. The Chief of Staff should be employed by the Regional Government. Councilors to be above 18 years. Education- form four education, at least O-level certificate. Councilors to have two terms every after five years. To be a registered voter, he should have a clean record. Councilors should be paid by Local Authority. No nominated councilors. A councilor if has messed should be (inaudible) by the public.

Interjection – Com. Dakika zako zime isha. Sema la mwisho.

**Mr. Kahanga –** Well.. The last one is the.. we should have a government, which can protect everybody in the Republic.

**Com. Lenaola** - Thank you very much. Hand in your memorandum, sign at the book. Asante sana. Mwangemi Charo

**Mr. Mwangemi Charo** - How many minutes are you giving me?

**Com: Lenaola –** You have a memorandum?

**Mr. Mwangemi –** Not amemorandum, just my note of mine.

**Com. Lenaola** - I will give you four minutes.

Mwangemi - kwa jina naitwa Mwangemi Charo – Ahh, nita anza katika umuhima wa wananchi katika Katiba. Ni maoni yangu Bwana Commissioners kwamba Katiba ni mkataba wa watawala na wananchi wao. Katiba sitakayo iweke wananchi juu ya chanzu zile za serikali, kwa sababu, kwa sasa serikali watuwake wame kuwa juu ya wananchi. Tuweze kuwa na katiba ambayo wananchi watakuwa juu, hawa watawala wao ni (inaudible)

Muundo wa serikali – kwa sasa serikali wa Central Government, sio ku negotiate, ni maoni ya watu, na nina amini pia kwamba wakati umefika ya serikali ikuwe ya Majimbo. Na tukisema Majimbo wasiseme wambao walitoko jimbo wale waende kwao, hapana. Mali yetu ya jimbo itumike kwa kusaidisha watu wa jimbo hizo. Wezangu wamepewa viwango, na mimi nitabidi ni pendekeze kiwango changu, kwamba kazi zote za jimbo hili mali yote ya jimbo hili asili mia sabini na tano ibaki hapa kwa kuwa faidisha watu wa jimbo hili.

Tatu, fedha za uma, iwaje kwamba sehemu nyingi zime umia sana na hali ta changia katika mfuko wa serikali, matumishi za fedha za uma. Ni mapendekezo wangu kwamba katiba iweke wazi, wazi kwamba kaguzi wa pesa za uma apewe uhuru katika ofisi yake. Na katiba imwezeshe kushitaki wale wote wanao haribu na funja mali ya uma, na lamsingi, … na lamsingi, mkuu wa sheria asiingilie kesi yoyote ambayo mkaguzi au mtibiti wa pesa ya uma ame shitaki. Tena nina ongezea kwamba pia hapa, bunge liizimishwe kwamba matumizi yote ya kutoka wa uma dhibitishwe au iimishwe na bunge. Nne, Taifa na serikali – Maoni yangu ni kwamba Katiba mpya sharti ifafanue kwa uwazi, wajibu wa kiongozi wa taifa, na kiongozi wa serikali. Katiba pia iwawekee majukumu watu hawa wawili. Ipasa katika kazi yawo, ifafanuliwe sawa sawa katika katiba. Tano, katiba iweke kaununi, sahihi inazo mwezesha mwananchi kuwa na uwezo wa kuondoa viongozi ambao wame geuka katiba au wana enda kinyume ya matako walio wachagua. Sita, uchaguzi wa rais, waziri mkuu, kwamba rais awe mkenya by birth. Aweze kutangaza utajiri wake, na awe kati ya miaka hamsini na sabini. Naye kiongozi ya serikali, nadhani kwa lugha anaitwa Prime minister, awe kati ya miaka arubaini na sitini. Atangaze utajiri wake na apate sio chini ya asili mia hamsini na moja kura zote zakazo pigwa wakati wa uchaguzi mkuu, so that he is not minority elected leader. Bwana Commissioners, nataka kuongea juu ya Judiciary ya kwanza upande wa mkuu wa sheria kwamba aendele kuchaguliwa na rais. Lakini haiwezekani mkuu wa sheria kama kiongozi wa mashtaka na pia awe advisor, legal advisor wa serikali. Katiba imwekee vikwazo, kwamba awe na jikumu moja. Kichini nyuma kuwa yeye aweze kuwatetea wafanyi kazi za serikali na pia ndio aweze shtaki wafanyi kazi za serikali, haiwezekani. Apewe jukumu lake mmoja la kuwa kiongozi au advisor za serikali na mambo ya mashtaka tupate mtu mwingine ambaye pia ata teuliwa na rais kutokana kwa maoni au advise ya Commission fulani.

Nane, lakini ni ya mwisho. Mamlaka ya rais. Sija soma katiba sawasawa, lakini section 14 ya katiba ina mpatia rais uwezo wa kunyakua hata mali yangu hata mali yangu na kwenda Scott free. Commissioners, tuwe na katiba inamwekea mipaka rais ya kwamba aweze kushtakiwa kama mtu mwingine ambaye ni Mkenya kwa vile yeye pia ni Mkenya. La mwisho kabisa Commissioners, Preamble katika constitution ni muhimu, hasa katika maisha ya sasa. Ninge omba, au sio kuomba, ni kupendekeza constitution ya Kenya iwe kama zingine katika upasa ule kwamba kuwe na muongozo au vibaji ya lengo ya wananchi katika Kenya. Lengo lao ni nini, vision yao ni nini katika katiba? Na indandikwe tafiti, lengo la wananchi wa Kenya wataka katiba yao iwe namna gani, yani preamble.

**Com: Lethome**- .. (inaudible) Rais kusema awe ni Mkenya kuzaliwa, aweze kueleza, kutangaza mali yake na umri wake, lakini hutueleza kiwango chake cha elimu. Tafadhali tupe kiwango chake cha elimu ukipendekeza, awe..

**Mr. Charo**. Ninge pendekeza awe na degree.

**Com: Lethome** – Na huyu waziri mkuu

**Mr. Charo** – Waziri mkuu pia. Na pia ninge ongeza MPs pia wawe katika kiwango hicho lakini, concillors, form four ina tosha.

**Com: Lenaola** -Na Preamble umesema kwamba iwe ni national tu lakini hujatoa maoni yako tupeleke wakenya (inaudible)

**Mr. Charo** – Katika vision nime sema ina maanisha kwamba wakenya weweze kutambua lengo lao la baadaye ki uchumi, socially na hasa ki uchumi, na socially, na mambo kama hayo. Waweze kuweza kile inavyo pata.

**Com. Lenaola** - Sawa. Asante sana bwana Charo. Jiandikishe pale. Stephen Mbaru.

**Stephen Mbaru** - Kwa Jina naitwa Stephen Mbaru Tunje, na ninge pendekeza mengi na mengineo yamesha tajwa lakini ninge pendekeza upande wa kuajiri. Ninge pendekeza tuwe na Katiba ambayo inge weza kuangalia upande wa uajiri, viwandani, na pia mahotelini. Utaweza kupata ya kwamba yeyote yule ambaye either awe ni mkubwa wa kutoka tutasema kama abara, yeye atakuwa na uwezekano ya ku chukua watu wale wa kutoka pande hio, hata ingawa kielimu, kuna mwengine ambaye ametoka point hii. Lakini kwa sababu ni damu, hata weza kumwacha. Ndiposa tunapata baadhi ya sisi huku, ambao sasa ni wakaaji, ni wenyeji, tume kaa bila, tuna kaa randa randa.

Na upande wa viwanda. Nukutia viwanda kwa sababu utapata viwanda ndivyo zenye kuleta uajiri. Viwanda vyetu vya pwani vime bomolewa. Hatujui ni kwa nini. Tuta chukua kwa mfano Ramisi, Kenya Cashew, viwanda hivi vili kuwa vina uwezo wa kuleta uajiri kwa vijana ambao ni wa eneo hilo. Lakini kwa kuanguka kwao zime tukatia nafasi hizo.

**Com: Lenaola** – Pendekezo …

Mr: Mbaru - Pendekezo langu ninge penda tuwe na Katiba ambayo inaweza kutupatia percentage, vile sasa tuna sema mambo kuhusu percentage, sabini na tano asili mia iwe ni wakaaji wa eneo hilo ndio wawe wata chukuliwa muhimu kwanza. Upande wa viwanda vile vile, lakini ki mazao. Uta pata kama muhogo ni mazao ambao tuna ya tegemea. Lakin kwa sababu wenye viwanda vile ni wahindi (inaudible) wana tununulia Masetu kwa bei vile wanao taka wao wenyewe. Cooperative, iwe ita weza kuwa na uwezekano wa kuingilia mambo kama ya bei, kuwe na msimamo ule ambao wakulima wata benefit. Kwa hivyo hayo machache, nime sema asanteni.

**Com: Lenaola**- Asante bwana Mbaru. Jonh Malingi Dzombo

**John Malingi Dzombo –** Asante kwa kupatia nafasi hii ya kuzumgmuza. Mambo muhimu hapa..

**Com. Lethome** - Anza na jina lako.

**Mr. Dzomo** - Jina langu George Malindi Dzombo, na ishi rusangani. Jibu langu maoni yangu ni serikali iwe ya Majimbo. Kwa sababu kutoka tuna nyakua mpaka sasa, mkowa wa pwani, hatuna chuo kikuu. Na vile ambavyo hatuna chuo kikuu. Na kwa vile ambavyo hatuna chuo kikuu, tu maskini kabisa waelimu. Na serikali ikiwa, ya Majimbo ndiposa sisi tutakuwa na sheiria ya kupanga ambavyo vile ambalo zina wezekana. Pili rais huyo ambaye tuko naye ni a stiza awe hapa kwa sababu kutoka aingie hatuja pata vita wala njaa kubwa. Kwa hivio sina mengi yangu ni hayo.

**Com. Lethome** - Kwa raisi unge pendekeza nin?

**Mr. Dzombo** - Aishi kuendelea, kwa sababu hatuja pata vita hapa wala njaa kubwa.

**Com. Lenaola –** Mpee nafasi. Ah na raisi mwengine ambaye atakuja baadaye unge penda waishi pia kwa ofisi maishani ama amawape muda fulani?

**Mr. Dzombo –** Kwa zile ambazo siwezi kumjua utawala wake kwa hivyo siwezi kumuambia aishi hivi wala hivi. Lakini katika huyo ambaye nina mjua ndio nina weza kusema awe anaendelea.

**Com: Lethome** - Wacha nikuilize Sali hili, yani mnapendekeza raisi akiwa mzuri kwa maoni yako akae katika kiti kwa mda gani?

**Mr. Dzombo** - Akae kiti kwa miaka hamsini.
(Laughter)

**Com. Lethome** - Maoni yake hayo.

**Com. Lenaola** - Asante - Jiandikishe pale. Francis Kalama

**Mr. Francis Kalama** - Asanteni sana, kwa majina naita Francis Kalama. Maoni yangu kuhusu katiba, kwa kweli kitu cha kwanza ni serikali yetu. Serikali iwe ile ya Majimbo hio ndio taa ya Kenya. Uta kuta kwamba, hapa pwani ni kama jimbo la kipekee. Lakini mambo mengi sana yame kinyagua ile serikali tuko naye.

**Com: Lethome** - Yame fanywa nini?

**Mr. Kalama**. Mambo mengi yame kinyagua. Kwa sababu utakuta mambo mengi, tuta anza na elimu. Elimu utaona kwamba kuanzia nursery mpaka form four kabla sijaingia university, hio elimu iko hali ya kwamba ni kama watu hawa somi kabisa. Maana yake hio nafasi ya elimu basi wale wanao soma zaidi watepelekwa huko mbele kwa wenzetu. Lakini hapa pwani wale wanao fundisha, sana wale ambao wana ile elimu ya sawa, sawa, hawa fishwi. Uta kuta pia katika hio elimu, kutoka degree, uhuru ume nyakuliwa. Yaani university hapa wekwa sijuni nini, sababu gani ambayo inatatiziza kwamba university isiwekwe.

**Com: Lenaola.** Pendekezo lako ni nini?

**Mr. Kalama –** Pendekezo langu ni kwamba hio katiba inayo ingia, elimu iangaliwe kutoka chini mpaka mwisho juu.

**Interjection Com: Lenaola** Ki vipi, iangaliwe kivipi?

**Mr. Kalama –** Eh, tuseme, hali ya elimu, serikali katika kila jimbo ndio ita pewa nafasi. Halafu utakuta mambo ya maji…..

**Interjection – Com: Lethome** - Ume seme kwamba wale wanao somesha huku elimu yao ni chine, ama si hivyo?

**Mr. Kalama –** Yes.

**Com. Lethome** - Sasa una pendekeza nini?

**Kalama** - Hio ninge pendekeza wale wanao chukua madegree, wanao chukua maelimu, warudi hapa kwetu jimbo na wa fundishe watoto wao kisawasawa.
**Com: Lenaola –** Katika hili jimbo?

**Mr. Kalama –** Katika hili jimbo

**Com. Lenaola –** Sawa.

**Mr. Kalama** - Kuhusu maji. Maji ni funguo ya wananchi. Bila maji uwezi ishi, hata Mungu mwenywe ame nyinyisia dunia hii maji. Lakini utakuta maji yanatatiza wananchi. Serikali inge kuwa ina umuhimu wa kupeleka maji kila pahali. Lakini utakuta mara nyingi maji yana pita tu kwa watu lakini haya pishi kwingine. Na ikiwa yana pelekwa itawekewa vikwazo hali ya kwamba hata wale watu maskini siyatumie. Hio ni jambo la maji. Barabara, barabara hio ndio uchumi kitu cha kwanza. Bila barabara hakuna uchumi. Bila barabara hakuna uchumi wowote. Mtakuta mazao yenu mkiwa muko nayo, kuyatoa utakuwa ni ngumu. Barabara ikiweko, serikali iakikishe kila area barabara safi iweko. Hata ikiwa ni moja ipitie tu hapo. Katika jimbo letu, bara

bara ni moja kutoka ukoroni. Ina pitia tu, hio inaenda kwa sababu ya mahoteli. Hio ni tatizo kubwa. Viwanda, soko, soko ni muhimu, viwanda ni kitu muhimu. Utakuta viwanda vimepewa wageni lakini wanachi wenyewe hawaruhusiwi kuweka viwanda. Mimi na shangaa sana. Hizo viwanda ambavyo ndio zinge saidia wananchi Wahindi watatoka kwao wacha waweke viwanda, si sisi. Viwanda ni kitu kingine ambacho kinaweza ku uzia mali ya wananchi kwa urahisi. Kiwanda kikiwa pahali, basi hio ina kuwa rahisi. Mwananchi yule ambaye ni mkulima, anatoa mali yake anapeleka kwa kiwanda.

Umeme – Umeme ni kitu kingine kinaleta kazi. Na hakika kwetu kutoka ukoloni, umeme basi tunafanya kuuona kwa wenzetu. Na umeme ukiingia, kiwanda bila umeme hakuna kiwanda. Mwananchi yule ambaye ame pata kazi za kisawa akiishi pale kwake, anatakikana atumie umeme kama kawaida. Lakini umeme haujatufikia. Serikali iangalie hiyo katiba ipange kila kitu, kila ki…mimi na sema kila division, serikali iangalie matatizo yale ambao tunaendelea kuyataja hapa. Na hospitali, hospitali hapo basi maiti ina zidi ikiwa hakuna hospitali. Maiti, watu wana kufa hovyo, hovyo bila kutibiwa. Mtu anataka ku zaa, mtoto ana toka vibaya, kubebwa mpaka huko hospitali ambapo iko, atakufia njiani. Hio tatizao iko hapa kwetu sana. Hospitali inatakikana iwe katika division, kuwe kuna hospitali hii ya ki serikali. Hio ni kitu changu, hizo ndio kitu changu muhimu, nina omba serikali inayo kuja ipange kwamba kila division, elimu, maji, barabara, soko umeme, eh, hosipitali, hivyo viwanda vyote, viwe iko kila division. Maanake division ina beba watu zaidi ya mamillioni, na sasa utakuta watu wote hao wakiwa hawana nchi, ni umaskini tu. Kwa nina omba serikali ijao itatue hio mambo.

**Com: Lethome –** Kuhusu viwanda, umesema serikali inaruhusu tu watu kutoka nje kukuja kuweka viwanda. Sasa swali langu ni hili, kuna mwananchi yeyote ambaye ame omba aweke kiwanda, kwa mfano kiwanda cha korosho, au kiwanda cha mnazi na nini, aka zuuliwa na serikali?

**Mr. Kalalma –** kuhusu viwanda, utakuta kwamba hapa kwetu, hata wazee ambao hawaku soma, waliamua kuweka cooperative. Cooperative ile, ili kuwa ina zui mali za wananchi. Wazee hawa kusome walifika tu darasa la pili na hawakuona katiba ambapo mali ilikua ikichopwa shambani chap, kwa cooperative, hio cooperative ili kufa, na mimi nina hakika kama inge kuwa wananchi wenyewe wange shikana watu wako hapa na madegree wanao, wange weka hio kiwanda na kuhakikisha kwamba wale wenzetu ambao ndio wana uwezo huo, wange kuwa wana pandisha hizi mali.

**Com: Lethome –** Swali ni hili, nani ame wazui kuweka hizo viwanda?

**Mr. Kalama** - Mimi naona hawa wageni wame zuia, wame ungana. Hawa wahindi ambao wana weka hizo, inaoneka hawaruhusu sisi kuweka viwanda.

**Com: Lenaola –** Okay asante sana. Cornonel Kai.

**Cornel Kai**. - Kwanza ninge zitaka katika marekebisho ya hii katiba, katiba irekebishwe ni hali ya kwamba ina weza kulinda

mwananchi yoyote, kwa sababu serikali hii ya hivi sasa, na hata kutoka tupate uhuru, unakuta kwamba watu wana uawa hovyo, hovyo, wana tupwa mituni, na tume zina undwa kuchunguza mpaka sasa, dakika hii hatuja kuwa na jambo lolote. Tume imetoka. Ina undwa, nakufa, kwa hivyo watu wana zidi kupoteza maisha yao. Kwa hivyo ilinde uhai wa kila mwananchi. Baada kuwa serikali itakuwa ina tulinda, hapa nilipo basi, kama hivi leo ingeli kuwa serikali yangu ni ya Majimbo, nafikiri mimi lingeli faa kikuu. Kwa sababu tangu uhuru tulipo pata 63 mpaka hivi, watu wakisema jimbo, jimbo, naenda jimboni pwani, naenda kwa jimbo la pwani ana kwenda Mombasa. Akiona Mombasa, anajua jimbo liko sawasawa. Lakini kama hivi leo nyinyi komishonas mumekuja huku ndio kidogo mnaona jimbo liko namna gani. Barabara mbaya, maji hakuna, uchumi hakuna, vitu vingi hakuna. Hata nyinyi lazima mume shangaa kuona kwamba miaka yote karibu arubaine hii? Mlipo hata kuingia huku ndani hamukuona hata barabara moja ya lami. Sijui kama mliona pengine mtanieleza baadaye.

Unaona tuna watoto wengi ambao wako huku reserve. Wana soma huku, wanafanya kusikia ati kuna barabara ya lami, wanafanya kusikia ati kuna mfereji ya maji…

**Interjection Com: Lethome** - Una jua unakionge, time ina isha bile kupendekeza. Afadhali pendekeze

.

**Mr. Kai** – Pendekezo langu ni kwamba hii Regional Government iweko. Jambo lingine ni kwamba pesa zote za serilai ziwe under control, kwa sababu hivi sasa kakuna control. Ikija yyote ambae ana uwezo ana nyakua. Akiambiwa aende kotini kuna mtu moja mkubwa anasema hapa asiende. Wacha aketi..

**Com: Lenaola** – Nani ana control…control na nani?

**Mr. Kai** - Hizo nini -kama hii eh..Ministry of Finance should control. Jambo lingine ni kama mlivyo sikia kwamba kampuni hapa zime kufa na ni kwa sababu mtu asiye jua korosho, mtu asiye jua mbata analetwa ana ambiwa yeye ni director wa korosho, na hata yeye mwenyewe hio korosho haijui. Mtoto ulie…(inaudible)

**Com. Lenaola** – Pendekeza

**Mr. Kai** – Pendekezo ya kwamba, ikiwa ni vitu ambavyo ni material, raw materials zikiwa hapa ziwe zina weza kupata mtu ambaye anaelewa jinzi zina zikuzwa, jinzi zinazo fanyiwa kazi mpaka ziwe katika hali ya kutengeneswa. Jambo jingine katika katiba ningelelitaka kwamba huyu president asi chagua wabunge maalum, kwa sababu ana jua pale pana Rotich, anajua pale pana Kamau, anajua pale pana flani, hii ichaguliwe, pendekezo langu ni kwamba, hawa nominated mps wachaguliwe na kamati ambaye itakuwa imeundwa na bunge.

Pili, jambo jingine, tungelikuwa katika hii Regional Government ita tuwezesha kufanya hata Polisi wetu ambao tutakuwa tunao katika region, ambao tunaweza kuangalia wana weza kuwapa kitu gani, au tuna wezaku fanaya kitugani juu yao. Na hata

Administration Police iwe ni wa wajimbo. Huyu Auditor General, awe ana uwezo, baada ya kuona kwamba, fulani, ame tumia, au ni mtu wa serikali ametumia pesa vibaya hata kama ni president, huyo apewe uwezo wa kuenda kotini direct, sio kwamba mtu mwingine aingilie.

**Com: Lenaola** - Dakika mbili zako zimebaki

**Mr. kai** –Dakika mbili ni kkwamba, hizo mbili zilizo baki ni kwamba mimi narudi hapo hapo Regional Government. Asante.

**Com: Lenaola** – Asante sana bwana Kai. Nyamuya Nyamawi

**Nyamuya Nyamawi** - Mimi ni Nyamuya Nyamwai, kutoka kitsweni. Pendekezo langu ni kwamba, zamani watuwa wa wazee wetu wakisoma walikuwa wakilipisha fee, na serikali hio fee ikaja ni kaondoa, majengo yakawa yajengwa na wazazi wenyewe, lakini tunaona kwamba hii eleimu kwa kwa, kwa kuambiwa kwamba ni bure, tunaonelea kwamba sio bure. Wananchi wanaumia sana kwa watoto. Kwa hivio tumeonelea kwamba serikali iweze kujenga hizi shule yenyewe, halafu mwananchi awe ana lipa ile fee.

Pili ni katiba. Katiba ni kwamba Kenya ime komaa, kutoka ilipo inyakue uhuru, kwa hivyo sasa kwa vile Kenya ni mpya tunapendekeza kwamba iwe ya katiba. Hapo nime maliza.

**Com: Lenaola** - Fafanua jambo la mwisho iwe ni ya nini?

**Mr. Namwai** - Jambo la mwisho iwe ni Majimbo.

**Com. Lenaola** - Thomas George Wamuye

**Thomas Wamuye** – Mimi nina itwa Thomas George Wamuye, na maoni yangu hasa, kuhusiana na katiba ambayo sisi sasa tungetaka ni katiba ile ya USSR, yani ya federal, ndio ambaye ina takikana. Hio ndio the best type of prescription ambao inaweza govern this country fairly. Na katiba hio vile, vile tunge taka iwe ina uwezo wa kuweza kuwa kila jimbo liwe na Governor General wake. Governor General wake ndiye yule, yule, ambaye tena vile, vile awe akichaguliwa na wananchi wenyewe kutoka jimbo hilo, hilo. Na vile, vile, state hii, yani jimbo hilo, hilo, vile, vile liwe litakuwa na polisi yake yenyewe. Na vile, vile katiba hio ione kwamba, kampuni zote ambazo zitakuwa katika jimbo hilo,hilo, nina eleza maoini yangu kwamba sabini na tano za mia wapenze kazi ile labour force, iwe inatoka katika jimbo hilo hilo. Na, the other codes za twenty five percent iwe itatoka kwa watu wengine ili tusiwe tuna jaribu kuleta ubaguzi. Na vile,vile katika katiba hio ambaye inatawala hio ni kwamba, kwa upande wa resources. Resources hizo, sabini na tano ziwe zitabaki hapo hapo katika jimbo hilo lenyewe, ziwe zitaweza ku develop hio jimbo lake. Na ile twenty five percent ambae ime baki ita pelekwa kule kwa central government ika

saidie uko vile, vile.

Na vile vile, tukija upande wa amendment ya hio katiba kitu ambao tuna taka sasa, tunge guze upande za powers za president, tunge taka hizo zi punguzwe ili presient asiwe sana na mamlaka kamili kuwa yeye anaweza ku appoint government officers, yeye mwenyewe tu. Lakini kuwe na kamati special from the, from the parliament ambao ita chaguliwa na AG - yule Attorney General awe katika moja ya wale kamati, na Chief Justice, awe moja wa wale wa wele ambao wata chagua wale government officer, ili tusiwe na ubaguzi wowote. Na appointment zile zote za government officers zione kwamba tuna guza kariba kabila zote arubaini na mbili hapa Kenya. Na vile, vile, upande wa …(**Speaker Mr. Thomas Wamuye, goes off, a new speaker, Joseph lewa, comes on the tape)…**

**Mr. Joseph Mwangome Lewa** - Jina langu mimi naiatwa Joseph Mwangome Lewa. Kama tunavyo jua ni kwamba nchi yetu sana inategemea upande we ukulima. Kwa hivyo tungependelea kwamba hivi policies za serikali zionekane wazi katika Constitution, kwamba zina endekeza mambo ya ukulima, ili wananchi waweze kula vyakula bila kuteseka. Hio ni muhimu. Ohm…wakati wa ku geuza Constitution, tungependa kwamba kuwe na opinions kutoka kwa wananchi wenyewe. Kama ni parliament, parliament iweze tu ku propose, lakini wananchi wenyewe waweze kuamua. Kuhusu wananchi, mwananchi awe tu na citizenship moja, nchi hii ya Kenya. Kama iko na citizenship zingine, asiweze kuwa mwananchi wa Kenya.

Security- President awe head of armed forces, lakini vita zozote kama vinataka kupendekezwa, zipendekezwe na approval ya parliament, na kama ina sumbua zaidi, wananchi wenyewe pia wafishwe katika opinion poll. Serikali tunapendelea mimi ni Majimbo na polisi wawe wata andikishwa kutoka kwa hayo Majimbo ambayo yatakuwa wamewekwa. Vyama vya siasa viwe viwili, na serikali iundwe na chama kimoja kile ambacho kita kuwa kimeshina.

Aina ya serikali, wale mawaziri wasio wana wabunge, wachaguliwe tu kutoka kwa rahia, lakini wasio wabunge. Na president awe kichwa cha serikali, na president awe tu ata husika na mambo ya international affairs, lakini internal affairs, iwachiwe cabinet. Kuwe na pia na Prime minister ambaye atakuwa in charge of the cabinet. Mawaziri wachaguliwe kisawasawa kutoka kwa kila province, yaani kila, kila ministry iwe inachaguliwa kutoka kwa province ili ikuwe na equal numbers of ministers kutoka kwa province zote. President aweze kuappoint ministers'
akishappoint ministers, wawe watakuwa approved by the parliament, asiweze kuappoint mwenyewe basi ubaki hivyo hivyo. Na kazi ya MP iwe ni full time, iwe compulsory: kama yeye anatakikana parliament, abaki parliament sio kutoka toka nje na kurudi at will. Kama wanafanya makosa, wananchi wenyewe waweze kumwita huku na waweze kumsack if necessary.

Morals za wachaguliwa: wawe hawana record mbaya, wawe ni watu wazuri, ambao hawaja fungwa, hawaja fanya makosa, hakuna usemi mbaya kuwahusu. Kama kuna usemi wowote wasiweze kuqualify kuwa wachaguliwa.

Kama nilivyo sema kwamba, mbunge ama mtu yeyote ambaye ame chaguliwa, aweze kufutwa hata kabla term yake kwisha

ikiwa it is necessary. Mishahara ya wabunge, na wale, wengine wamechaguliwa iweze kupendekezwa na ministers, na ikiwa ministers hawawezi, wapeleke habari kwa wananchi na wananchi wenyewe waweze kutoa opinions zao.

Kuondoa serikali wakati kama imeonekana haiwezi, hio ipelekewe kwa wananchi wenyewe watoe opinions polls.

Wakati wa kupendekeza mijadala ya bunge, ili bunge liwe ndio supreme, president asiwe ndio mwenye kupendekeza awe na swala la mwisho kuhusu yale mapendekezo ya bunge. Yaani lolote ambalo wakaloamuliwa na bunge ikubaliwe straight away, kwamba ni issue ambayo imekuwadiscussed na ikubalike namna hio.

The executive –Serikali iwe ya miaka kumi, na zile kazi za president ziwe defined, asiwe anafanya lolote tu.

Local Government: mayors wawe pia wanachaguliwa directly by the people. Zile kazi ambazo zitakuwa zimepewa mayors, , na hii pia ni kwa wale wachaguliwa wote, ziwe predetermined by the people kwa sababu kabla mtu hajachaguliwa, aweza kuambiwa wewe sisi tuna kuchagua lakini kazi zako ambao tunataka wewe ni kuzi fanya ni kadha Kama hataweza kufanya hizo kazi, aseme mapema, mimi sitaweza kufanya hizo kazi hizo. Asije akasema mimi nitaweza, aende kule, akifika kule, halafu kazi anashindwa, halafu wananchi wanakuwa frustrated. Kwa hivyo awe kuzijua mapema, aelezwe mapema azijue, akienda kule awe na uhakika kwamba ataweza kuzifanya.

Basic Rights: mambo ya mashamba, title deeds ziandikwe na bwana na bibi. Si kwa madhumuni ya wale wawili lakini kwa madhumuni ya watoto, ili watoto wawe ndio watafaidika mwisho kabisa. Wanawake kama wamezaliwa pale, hii ni kudi discourge mambo ya prostitution, vile wameruhusiwa kuwa na mashamba. Kwa hivyo, yule ambaye amezaliwe pale nyumbani, iwe ni jikumu lake kutafuta babaake, kama ni mke, aende ajue ni wapi kule ata nda kuishi. Lakini isiwe ni responsibility ya wale wazazi ambao wamemzaa pale.

**Interjection – Com. Lethome –** Hebu fafanua hilo

**Mr. Lewa –**Nina sema hivi: ikiwa mke ameolewa, ataandikishwa katika title moja na bwanake, sawa. Akishaandikishwa katika title lile, wale ambao watariithi niwanaume.

**Com. Lethome –** Watoto wa kiume?

**Mr. Lewa –** Wakiume. Wale wanawake wataenda kuriithi kule wameolewa

**Com. Lenaola** - Na wasipoolewa?

**Mr. Lewa** - Wasipoolewa, na hatujui kama hawataolewa. Kwa hivyo vile tu tunaomba ni kwamba wataolewa. Kwa sababu tukisema tunawapatia mashamba, kutakuwa na ile problem ya kwamba, wata kuwa na confidence ya kwamba: niolewe nisiolewe, mimi lazima nitapata shamba hapa. Hio itaencourage a lot of prostitution around, watu wako na confidence…

**Interjection –Com: Asiyo**–Lakini ukumbuke hili katiba ni ya miaka mia mbili ijayo. Sasa ukisema mwanamke, na unajua sasa hivi karibuni wasichana hawatakuwa wakiolewa.

**Mr. Lewa** - Okay, kabla sijaendelea mbele nilikuwa nasema hii katiba iwe itageuzwa wakati wananchi wenyewe watahitaji. Parliament itasuggest wananchi wenyewe wataauma kama tunaona ile hali vile inaendelea. Lakini tusiseme itakuwa ya miaka kadha. Mia mbili., mia mbili ni muda mrefu sana. Mambo mengi huwa yamegeuka.

**Com. Lethome** - Kwa hivyo, mtoto wa kike asirithi?

**Mr. Lewa –** Mtoto wa kike asirithi kwa sababu akirithi atakuwa na confidence, kutakuwa na wanawake wengi watabaki nyumbani kwa sababu, wanajua mimi hata nisipoolewa, mimi nitabaki hapa na shamba.

Kuhusu information: kama vile broadcasting, kuwe na a lot of transparency. Haya mazungumzo ambayo yatakuwa kwenye maradio yawe issue oriented, not personality oriented. Kama wakati tunazungumza, tuna zungumza rais Moi, rais Moi rais Moi. Sasa yani tuna sikiza mambo ya Moi ama tuna sikiza issues ambao ni za maendeleo.

**Com. Lenaola** -Asante kwa leo - Patrick Kai, halafu amfuate Rebecca Ndombo, utafuata huyu halafu, Sister Wachera atafuata Rebecca.

**Patrick Kai** - Kwa jina mimi ninaitwa Patrick Kai, napendekeza mfumo wa sasa uwe katika Majimbo. Kwa kuwa kwa miaka hii yote arubaini tuliokuwa, bidhaa zetu hapa pwani hazija tatuliwa na serikali ile ambayo tulikuwa nayo. Nikiguzia hapa ninaanza: Kama hio korosho, mitambo wa korosho umeangushwa; naangalia kama ni sukari Kwale, mitambo umeangushwa; nikiangalia vitu vingine kama punde pojo, muhogo haujatambulika na serikali hii ambayo inatutawala kwa miaka arubaini. Ninapopendekeza kuwa serikali ya Majimbo, hawa wote, yule atakuwa ni Governor, ataangalia kuwa mimea hii yote, wapende wakatae, ni lazima wataitafutia soko la nje, na hatimaye kumuinua, yule mkulime ambaye yuko ngazi ya chini kuamka.

Nina guzia tena hali kama ile ya utalii, chochote kinachopatikana hapa kwa kuwa ni biashara, ishirini na tano inaenda kwa serikali kuu na sabini na tano iwe ita tekelezwa hapa. Kwa upande mwengine tuna endelea, elimu. Ni aibu sana tuseme ya kwamba miaka hii arubaini yote pwani haija kuwa na chuo kikuu. Nahata ingawaje hawajiwezi ki elimu. Ningeli pendekeza ya kwamba, serikali inaokuja angalao ipunguze mean grade, za watoto hawa ambao wana soma, wavulana, wasichana, kutoka Lamu hadi huko chini. Angalao ile mean grade iweze kuingia kumvuta musichana wa pwani, na mvulana angalao iwe ni quarter

system. Kujua ya kwamba katika pwani yote, mwaka huu tume wezesha kuingia watoto kadhaa university.

Hasa niki gusia kwa akina mama. Tuta sema ni aibu, kwani si akina mama wengi hata tuki wahesabu katika, tuchukue kilifi kwa mfano, ikiwa tuta sema wame fika kama akina mama mia tano walio pata , walio kuwa, ambao wana degree sasa, nafikiri ita kuwa ….hawaja patikana kwa jumla. Hali hii ambaye tuna angalia kama tuki ingia katika kwa mashamba, wale ndugu ambao wamepata ma title deeds, hali mwenyeji hawaja pata, tungalionelea, au ninge pendekeza ya kwamba, hawa wapewe lease kwa kiwango fulani, na shamba zile baada ya muda fulani, waziwache kwa wale wenyeji, au watendelea nazo wawe wakilipa na malipo yale, yawe yata faidisha watoto wa hapa.

Niki gusia katika kazi, viwanda vyote au kazi zozote zitakazo tokea katika mkowa huu, sabini na tano ipate wenyeji, ishsirini na tano zipate ndugu zetu wengine ambao hawa tuna jua kwa wakati huu maana wame ingia katika vio vikuu, wako na taruma za juu, tupate kama mainginia na wengineo hapa. Tukiguzia katika mukowa wa pwana, hatuja pata hata engineers kumi ama ishirini.kwa kufika kama hapa. Walio pata ni ishihada kweli.

President- mamlaka yake ninapendekeza yapunguzwe. Na ugeuzi wa wale watu kama wale ambao wata pewa na mamlaka na yeye amewa teua kama wa bunge, basi waweze ku idhinishwa kwanza kielimu. Mtu huyu aki chukuliwa kama ame kuwa appointed na president ata ingia faculty gani kusaida mwananchi yule wa kawaida? Mipangilio hii nikitaja hakuwa tuna hitaji Majimbo, ni kwamba, kwa miaka hii yote njia zeto haziriithishi. Moto hauja tufikia, ngasi za spaki pengine wala hata simu zenyewe hatuja ziona. Kwa hivyo napendekeza Majimbo iwapo governor ata tekeleza haya yote basi na wenyewe wafanye kazi kwa bidii, hatuta chukua kama muda mrefu, tutaweza kupata vitu hivi.

Mahospitali - Ni aibu kusema kwamba kama Wachuonyi, kwa miaka hii arubaini hatujakuwa angala na sub-hospital. Watu wanapo fariki tuna pata shida sana. Cost general, ama kilifi. Na si wote ambao wana uwezo wakuwa pengine watu wao wanapo fariki, wanaweza kuwapeleka kule. Garama zime kwenda juu.

**Interjection – Com.Lenaola** - Mapendekezo..

**Mr. Kai –** nina pendekeza, ikiwa serikali ya majibo ime ingia, iweze kujenga mahospitali ya kisasa, na iweze kuleta huduma hizi za ambulenzi kuwe karibu pamoja na mortuary za ki siku hizi. Nafikiri niki malizia, ni elimu ya watoto wa darasa la kwanza hadi la nne, serikali napendekeza kwamba, mimi napendekeza ya kwamba wale watoto serikali iwe itaangalia criteria yote. Lakini hawa kama ni ma headmaster, wawe watoto wale hawata wa charge hata senti moja kwa wezesha kila kabila, watoto wataweza kwenda mashule. La si ile kusema tuna taka building fund, tuna taka watchman. Watoto wa darasa la kwanza hadi la nne wasiwe wana malipo yeyote. Pia nina pendekeza, tunapo enda hadi darasa la nane, kwa kuwa watoto hawa ni wadogo, nina pendekeza masomo huu wa elimu wa nane, nne, nne, hapa tuwe na bridge ya kumpa form six, ili wanapo ingia form five, university, watoto hawo wawe wame komaa. Ni hayo.

**Com: Lenaola** - …Sasa Rebecca Ndombo.

**Rebecca Ndobo**
**(Rebecca's speech – not there**.)

**Speaker (un announced - unknown**)

Na ile ishiri na tano iweze ku tangos na uweze kwenda katika ki taifa. Katika mabaraza, ninge pendekeza kwamba mayors or wenye viti wa mabaraza wachaguliwe direct kutoka kwa wananchi. Na term ya miaka miwiliiwe itabakisha hio hio. Na pia mabaraza wepewe yasiwe kutoka ofisi kuu ya serikali. Itoke kwa Central Governemt,, waweze kujipangia na kutekeleza kulingana na vile wamepanga.

**Com. interjection** (inaudible) - peane memorandum pale na jiandikishe hapo Simon kitui

**Simeon Jacob Tonje -** Jina langu ni Simon Kitui mimi ni mkaaji wa hapa hapa, Chwonyi. La kwanza….

**Interjection -Com. Lenaola –** Uko na memorandum?

**Tonje–** Haiko tayari, lakini nitas highlight. Nita towa kama sikutowa hapa nita peleka kwenu. Kwanza mimi napendekeza serikali ya Majimbo ambayo mengi tuta kata shauri wenyewe hapa vile zinavyo patikana kazi, sababu kama kazi zilizo pata na kuja fanyiwa interview na watu wa kutoka bara na wana leta watu wao hapa, na bila kuchukua wetu. Pia lasirimali yote napatikana hapa ina kwenda huko tuna taka kutumia wenyewe.

La pili nataka kuzungumuza habari ya citizenship. Citizenship, urahia nataka yule amezaliwa na wazazi wote wawili na wenyeji wa hapa apate citizenship upesi, na aweze akapata identy Card au Passport. Hata yule ambaye kwamba ame zaliwa na babaake yuko hapa lakini mamaake ana toka mbali, nina pendekeza kwanba pengine ikiwezekana hata yule ambaye mamaake anatoka nje aweze kupata… I mean yule ambaye babaake yuko hapa na mamaake anatoka nje, aweze kupata double citizen.

Nateremuka upande wa Auditor General, mimi nataka iwe awe na personnel yake aweze kupeleka watu kotini, wale ambao wameshikwa na corruption. Awe na personnel wake, polisi na ma lawyers, kila kitu. Expenditure – Pesa za ume, ikubaliwe na bunge kwanza kabla hazija tumiwa. Niki fika kwa mahakama, jaji mkuu ninge pendekeza kwamba achaguliwe na parliament, na wale majaji wengine, kuunda kamati ambao kwamba ita husisha wambunge kama watatu, Attoney General na Chief justice

kuchagua ma jaji. Umri ya hawa, I mean qualification za hawa, tunataka wawe senior lawyers kutoka magistrate, judges na hata Chief Justice wawe ma lawyers. Umri wao uwe kutoka 35, waweza ku serve mpaka 70.

Members of parliament – Mtu akisha chaguliwa kama member of parliament au councilor for that matter, tunge penda asiweze kuitwa. Kwa sababu aki itwa wale wenye kuwaita mara nyingi huwa ni wachache. Sio sawa, sawa wale walio mchagua yule councilor au member. Kwa hivyo ita kuwa ameonewa. Kwa watu watatu kuita mtu arudi na ishiri au mia moja walichagua yeye.

President tuna taka awe mwenyeji wa hapa, umri wake ni 35 years, education graduate and above, hata kama ni professor, tuna taka. Pia vile vile termu mbili ya miaka mitano, mitano. Member of parliament lazima pia vile, vile, awe na umri wa miaka ishiri na tano, education form four and above. Councilor, form four. Member of parliament lazima achunguzue, kwamba ni mtu ambaye kwamba ana (inaudible) ya kutosha na hana madeni.

Security, wale wote Armed Forces, GSU, Police, Prison, and every wote wawe katika Constitution na awe watakuwa chini wa uongozi wa presient.

Political Parties, yeyote ambaye kwamba ni member wa chama fulani, amechaguliwa kuwa mjumbe aweze ku cross floor mpaka a resign kisha halafu achaguliwe tena. Parliament should have the power to appoint the Chief Justice and Corporations, their Managing Directors, ili kwamba tusiwe na ubaguzi. Salaries za macouncilors to be determined by the Local Government. Removal of president, vote of no confidence by parliament should be enough. Appointment of officers I have already said, judicial officers. There should be no special seats for women. Wome should struggle it, the same way as men. Kwa sababu special seats kwa women ni kuwarudisha nyuma hawa watu lazima wafanye kazi.

Registering of Voters – mimi na suggest kwamba iwe throughout, it should not be iwe ita kazwa tu wakati wa karibu na election lakini kila mwaka kuwe na mwezi mmoja ambao kwamba watu wana weza kujiandisha kama wapiga kura. Lakini wakati wa karibu na election, waweze ku enphasize kidogo wapewe muda mrefu ya kutosha.

**Interjection Com. Lenaola** - La mwisho.

**Mr. Tonje**– La mwisho mimi nasema Majimbo ndio serikali tunataka.

**Com. Lenaola** – Ngoja kidogo basi, kuna swali. Ume sema kuwa president awe 35 years, sealing yake ni ngapi

**Kitui** – Sealing yake ah sixty

**Com Lenaola** – Sixtty. Mps?

**Kitui** – Mp – 25 to 60.

**Com. Lenaola –** Councilors kutoka twenty five to sixty as well manake he is a human being.

**Com Lethome –** Councilors, Local Authority yenyewe ita amua. Na mshahara wa wabunge?

**Tonje –** Mshahara, mimi nina gependekeza kwamba kuwe na kamati ambaye kwamba ita kushisha mwakilishi kutoka ofisi ya president, Chief Justice, Attorney General and Speaker wabunge na wa bunge watatu kwa kamati hio.

**Com. Lenaola –** Nelson chiko

**Nelson Chiko –** Kwa jina naitwa Nelson Chiko - Mimi na taka kuzungumuzia juu ya mwananchi wa Kenya awe nani. Mwananchi wa Kenya nataka tiba iandikishe wazi kwamba mwananchi wa Kenya awe mtu amezaliwa na mafrica wa Kenya. Apate uanaichi wa Kenya akiwa akiitana awe mwanachi wa Kwenya kupitia kwa baba yake sio kwa mama yake. Nataka pendekezo langu lingine, vyama vya siasa, viwe vitatu pekeyake. Na system ya serikali ama system of government mimi nataka ya Majimbo tuwe na rais moja, hakuna waziri mkuu. Rais achasguliwe katika mikowa yote au Majimbo yote ambayo yata kuwa yametengezwa katika nchi hii ya Kenya.

Serikali za mitaa. Councilors, wawe wakiendelea sawasawa na wabunge miaka mitano. Chairman au mwenye kiti au mayor aendelee tu miaka mitano ile, ile mipango wa miaka miwili, miwili halafu uchguzi, ile ina regesha nyuma maendeleo. Juu ya mali ya uma, tuna taka kila sehemu za jimbo ambalo zitakuwako zi simamie yenyewe rasilimali vile, halafu kama asili mia ya sabini na tano kwa mia ibaki katika sehemu ile na ishirini natano ziende kwa serikali kuu. Asante.

**Com. Lenaola** - Majani Chibungu

Majani Chibungu – Mimi jina langu naitwa Majani Chibungu kutoka maratana station. Yangu ni machache sio sana, katiba Kenya – Muongozo wa serikali ndio Majimbo Kenya. Pili utamaduni wetu wakiafrica iheshimiwe hapa Kenya. Tatu, uchaguzi wa mlolongo. Nne, urithi. Utumiwe na watoto wale walio wachwa na alio kufa, shamba yao.

**Interjection Com.** (inaudible).

**Mr. Chubungu –** Kwa kiume, ikiwa kuna wanawake ambo hawaja olewa nao wapate haki yao. Tano – wajumbe wa pwani wawe na bunge lao. Kwasababu nasema hivio ni kwamba wakiwa na bunge lao wata zungumuza mambo yao ya mukoa wao na wapitishe na isiingiliwe na wabunge wa sehemu nyingine. Sita, askari ziwe na amnesty za kubeba wagonjwa kwa sababu

tangu tulipo nyakua uhuru hospitali zetu hapa, watu wana poteza maisha yao, wengine wana zaa wakifa, sababu wameshindwa na izazi, hakuna usaidishi, na pia wana pata ajali barabarani pia wana pata shida ya kupelekewa hospitali kuu wa mukowa. Kwa hivio tunaomba serikali hii ya Majimbo ikiwa katika uongozi iangalie sana ya kupiga darubini katika hospitali zetu ziwe za kisasa. Sina mengi mengine.

**Com. Lethome** - Umesema kuwa uriithi wa mtu amekufa watoto wake wariithi hata wasichana ambao hawaja olewa. Na wale ambao wame olewa?

**Mr. Chubungu** - Wale wame kimbia boma,

**Com. Lethome** – Wamekimbia ama wameolewa?

**Mr. Chubungu** - Wame olewa, hawana uwezo kwa sababu tayari…

**Interjection – Com Lethome** – Ni uwezo ama haki, wana haki ya kuriithi ama hawanahaki ya kuriithi?

**Mr. Chubungu** - Mimi kwa maoni yangu nataka wale walio baki pale waachiwe shamba.

**Com. Lethome** – Na mama yao, mjane, na huyu mjane aliye wachwa?

**Mr. Chubungu** - Huyo mama yao, atakuwa pamoja nao.

**Com. Lethome** – Ariithi ama asi riithi?

**Mr. Chubungu** – Ata riithi kutumia yale sehemu ambazo zime wachwa na bwana yake pamoja na wanawe.

**Com. Lethome** - Na mambo ya ufwa una sema aje?

**Mr. Chubungu** – Mambo ya ufwa hayafai, tume kataa.

**Com. Lenaola** –. Akina mama sasa hivi tuta pata nafasi mta zungumza wengi.
Sawa. Nyamai Sanga, Nyamai Sanga.

**Mr. Nyamai Sanga** – Kwa majina, Nyamai Sanga. Yangu ni mawili tu.

**Com. Lenaola** – Nyamai Sanga

**Mr. Sanga** - Katiba ya Kenya ninge penda hivi, awe serikali ya Kenya ni majimbo. Ya pili, wale viongozi ambao wana ongoza wananchi kuanzia sub-chief, chief, councilor mpaka raisi wachaguliwe na wananchi. Ni hayo tu.

**Com. Lenaola** - Asante. Haya, Mbaya Lewa, Patrick tembo, Patrick Haro, halafu ufuate.

**Mr. Mbaya Lewa** – Mimi naitwa Mbaya Lewa kutoka Chasimba. Mbaya Lewa.

**Com. Lenaola** - Endelea.

**Mr. Lewa** – Mimi nataka katiba ya Majimbo, kwa sababu kule kuzaliwa kwangu nime fungua macho nili ona serikali ya Majimbo. Kwa hivyo, toka hapo ika nina ingojea, na sasa nimeona imefika wakati wa kuchagua mwenyewe, ile serikali ilio pita imepita. Na sasa wakati wangu uwa kuwa imefika. Bado nina ona sija kufa, kwa hivyo nina sisitiza Majimbo. Kwa sababu, moja wapo ambalo ni nalo, toka wakati ule mpaka sasa, sijaona barabara kwetu, nina ona mavumbi, bado sijaona ma university kwetu, basi sijaona ma hospitali wetu, bado masikuli sisi wenyewe tulikuwa tuna soma kadhi ya shillingi tatu kwa mwezi lakini pia nina shukuru nimepata elimu kidogo. Uliobaki ni watoto wetu wana teseka, Kuwa ma university hakuna. Mtoto akisoma akifika form four, basi. Mtoto huyo hana kazi Mombasa ana baki ya kusafisha viungo ya watoto, ya akina mama wa kihinidi. Kwa hivyo, ndio nikaonelea nimefika hapa kwamba nieleze kinaganaga, serikali afadhali iwe ya Majimbo…..

**Interjection -Com. Lethome:** Pendekezo lingine, hio tumesha sikia.

**Mr. Lewa**……sababu moja wapo moja wapo si ndio sawasawa, moja wapo, lasirimali zetu hapa bado zina potea. Kama nazi, toka hapo mpaka sasa haija pata marketi, mihogo, haija pata marketi, ndio hata watoto wetu wana didinia kwasababu zile mali yetu ina potea.

**Interjection Com.Lenaola**: Pendekeza.

**Mr. Lewa** – Kwa hivyo napendekeza mali hio yetu zipate market. Vile, vile watoto wetu nataka wapate vibarua maanake vibarua Mombasa vimekuwa ni tabui,.. Sisi wenyewe tulipata, ukondoka hapa na pale una tafuta kibaruwa. Sasa na mwanangu anazunguka mwaka mzima, na ni form four. Kampuni ina andikwa hapa, hapa Mombasa kwetu kotu. Na hapo hapo yule mtoto wangu hapati kazi. Akipata mwengine wa form four ana toka huko aaje apate kazi hapa.

**Interjection – Com. Lenaola –** Una pendekeza nini?

**Mr. Lewa -** Kwa hivyo nina pendekeza, watoto wa jimbo letu wawe kwanza waende wao kuandikwa katika kampuni. Sabini na tano iwe ya hapa costi. Halafu wengine, tukuwe wenzetu nao tusije tuka wa sahau, kwani wale ndio ndugu zetu vile, vile. Vile, vile, pesa zauma nazo vile, vile kule, tuna ziona nyingine ati tuna kimbia. Pesa zile nazo pia ziko hapa ambazo zina ingia kutoka njia (inaudible) manake kuna ingia ingine ya nchi kavu zingine za baharini. Kuna pesa kule zina ingia, na pesa zile nazo pia zikiingia hua zina pita through. Kiwango chetu hapa costi hatupati maanake mali ikija kwangu nataka niweke..

**Com. Lenaola** - Lakupenda…

**Mr. Lewa –** Nina pendekeza iwe sabini na tano iwe hapa kwetu, halafu hizo zingine ipelekewe jamaa zetu. Maanake ndio ita jenga barabara na mahospitali hii. Sio kunyonyorwa kila miaka, tume choka. Sina mengi.

**Com. Lenaola -** Asante kwa maoni hayo. Jiandikishe pale. Patrick Haro, halafu Antony Kazenga, halafu Jimmy Ngala…

**Patrick Haro –** Kwa majina naitwa Patrick Haro, ni mkaaji wa Chwonyi. Ninge penda kuanza kueleza kwamba katiba ya Kenya kabla uhuru ilikuwa federal in nature, ilikuwa ya Majimbo. Ni bahati mbaya kwamba baadaye ilikuja ika geuka ikawa unitary. Na mimi ninge pendekeza iwe federal type of Contitution, Katiba ya Majimbo, ilikila jimbo katika jamhuri ya Kenya liwe litakuwa na mamlaka administratively, legislatively, yani kila jimbo liwe na Regional Legislative Council yake. Na kila jimbo liwe na Regional Executive Council yake. Na kila jimbo liwe na powers yaku panga mipango yake ya jimbo lake economically socially and everything. Kusiwe na kuingiliwe sana kutokana na Central Government, lakini kuwe na ushirikiano. There should be some sort of cooperation between the Central Government and the Regional Executive Council. Mapato kutoka kwa Majimbo kadha wa kadha, katika jamhuri ya Kenya, the way they are going to be devided. Iwe ni sehemu fulani, a certain fraction iwe ni twenty five percent …

**Interjection – Com Lenaola** - (inaudible)

**Mr. Haro –** Nina sema ni twenty five percent ya total income ya kila jimbo iwe ita pelekwa kwa Central Government, na zingine zibakie katika jimbo lenyewe.

Makomishonas nina sikitika kusema kwamba observation yangu imeonyesha kwamba Mchonyi amefanya kuvamiwa leo. This is an ambush to the Muchonyis. Nikiseme ni ambush nina maanisha kwamba wawili watatu walio kuja hapa hawakuelewa neno katiba ni nini. Nanielewavyo mimi, under terms and reference of service, terms of reference ya Ghai Commission, moja wapo ni ku provide civic education to the people. Halafu mna rudi mnakwenda mna collect views. Nina shindwa kuelewa Mchwonyi alielimishwa lini? Hata leo wame fuata atoe maoni yake. Ame vamiwa Mchwonyi. Hajui katiba ni nini.., stahili kupewa au kutumia forty seven thousand shillings kwa civic education. Bahari constitutrency was also supposed to be allocated with the

same amount, forty seven thousand shillings. Je, Wachwonyi wame elimishwa mara ngapi, ni seminar ngapi zime fanya za maelimisho kiasi cha kuwa leo tuna takiwa tutoe maoni? Where these civic education seminars, where were they conducted in Chwonyi as such? I have not come across any. I would even go to the extent of suggesting, hata pengine ninge pendelea kwamba hii section ivunjwe leo, Mchwonyi alimishwe kwanza halafu murudi baada ya miezi mitatu, muuje mtake maoni kutoka kwetu. You cannot look for opinions from us when you have not educated us at all. Au ni vibaya ninavyo sema?

**Chorus** - No, no, no.

**Mr. Haro** - Hawaja tueleimisha, na Bahari Constituency ina stahili kutumia elufu arubaini na saba kutuelimisha sisi, kuhusu katiba. Iko aina katiba mbalimbali. Hatuja elimishwa.

**Interjectio**n - (A lot of noise)

**Com. Lenaola –** Unajua eh yale ambao umesema si mabaya. Maana leo ni siku ku kuchua maoni. Na hayo ni maoni. Hatuko na District Coordinator wenu wa Kilifi hapa, ame enda Ganze. Kama ange kueko, haya maswali angeyajibu, maana mimi sikuja hapa kujua ulifanyiwa civic education lini na wapi. Lakini ni kweli kwamba kuna forty seven thousand kwa katika kila constituency, kwa kuingia kwa civic education. Lakini kwa maoni yangu, sasa mimi wacha nitoe maoni pia mimi. Kwa maoni yangu yale mme yasema, ni ya maana zaidi. Si mambo ya mchezo. Kwa maoni yenu, si mambo ambao ni kama watu povu, mmeongea mambo ni ya maana sana. Kwa hivyo ninge waomba kuvunja kikao haita wasaidia. Afadhali tusikie maoni yako kuhusu civic education, lakini maoni ya wale ambao wamekuja pia tuchukue. Kiisha tunayaandika tuna zitape mambo yako. Hii shida si Bahari Constituency pekeyake. Ni kwa nchi nzima. Hakuna mahala nime enda sijaambiwa, baado civic education. na nivigumu kuangalia, si kama mtihani hawa watu wa Bahari wa Chwonyi mketi tujuwe mume elewa katiba maneno gani, marks hamsini, marks sitini. Ni vigumu kufanya hivyo. Kwa hivyo ni vizuri, mmeketi vizuri tangu usubuhi, ime fika saa saba, maoni kwangu kama uakili bwana Mwea najua kwamba, maoni yeni ni ya izito sana kwa Katiba. Kwa hivyo huu, ninafikiri nafasi msi poteze. Muko hapo hamsini, tumefikisha watu ishirini. Wapi thalathini? Ninge penda ku malize na wale wako. Kama kuna sabu ya kurudi tena hapa Barahi, tuta rudi. Lakini maoni yako bwana Haro nime ya sikia na nita chukua mbele. Tume agana hivyo?

**Chorus –** Sawa,sawa.

**Com. Lenaola** - Basi tuendelee, lakini yale mambo mnayo sema ni ya ukweli na ni ya maana. Lakini naomba tuendelee. Sawa, sawa? (laughter) Okay bwana Haro. Basi jiandikishe pale. Asante sana. Antony kazenga. Bwana Kazenga?

**Antony Kazenga –** Naam.

**Com. Lenaola** - Haya karibu.

**Mr. Kazenga –** Kwa jina nina itwa Antony Kazenga, first and foremost kuhusu katiba na pendekeza serikali ya Majimbo. Sababu ziko wazi. Tangu uhuru ime kuwa kwani kwa sisi zote wa Kenya. Lakini Majimbo mengine kwa wazelendo wa huko. Ndipo utakuta kila moja yu akilimbilia pwani, na akifika hapa ana pata. Pia napendekeza vyama vya siasa viwe vitatu. At the moment tuna zaidi ya, kuna viama zaidi ya makabila ya Kenya. Kwa hivyo, ni kwamba kila kabila liko catered for. Vyama vya siasa ziwe vitatu. Eh, rais wa Kenya na pendekeza asiwe mbunge wa mahali popote. Asichaguliwe kuwa mbunge wa mahali popote, maananke ni kwamba akisha pata uongozi basi definitely ata pendelea sehemu yake iendelee zaidi kuliko sehemu zingine.

Kitu kingine ni kuhusu land registration ya hapa pwani. Ni wachache sana kwa pwani ambao kwamba wana own land hapa. Kwa jumla ni kwamba wapwani wengi ni squatters. Tuna ambiwa mashamba yana kuja kuandikishwa, baada ya hapo title deeds hazionekani. Wamekuja hawa watu wandikisha sehemu hapa, waka chukua pesa waka enda zao. Na tuka ambiwa kwamba ule uliandikishaji ulikuwa ni fake. Sijui kutakuja lini wandikishaji kamili wa mashamba haya. Kuhusu kazi, wenyeji wa pwani, sio kwamba hawakusoma, wamesoma, lakini hawapewi nafasi za kazai. Nafasi za kazi hapa pwani zina enda kwa wenzetu kutoka bara. Sio kwamba ati wao wame some zaidi kuliko mpwani, lakini ni kwa sababu ni wao ni vile walivyo. Nafikiri unaweza uka, uka malize wewe mwenyewe hapo.

Eh… mazao, tume tegemea hapa mnazi, muhogo korosho. Kutoka kwa mnazai tuna nazi zenyewe, kuna fagio, kuna pombe ya mnazi, lakini kama ingeli kuwa umnazi uko huko bara, pombe ya mnazi iko bara, basi inge kuwa huwezi kununua kwa shillingi ishirini au ishirini na tano. Unge nunua kwa shillingi mia mbili na zaidi. Lakini kwa kuwa ni wa hapa pwani, haupati bei. Mnazi ina nunuliwa kwa sumuni. Mnazi, sumuni mmoja. Ufagio una nunuliwa kwa shillingi tatu. Ufaguo huo, huo mpaka yule mtu aangalie ni bumba la ufagio ili akaweze kugawanya gawanya ufagio moja huko kwa wenzetu ni shillingi sabini na tano. Na ufagio moja hapa ina nunuliwa kwa shillingi tano ukigawanya intoka fagio nne; kwa shillingi sabini na tano kila ufagio hapa una pata shillingi mia tatu kwa huo ufagio wa shillingi tano; alio pata bure hapa.

Pia na pendekeza wazee wengi wame staafu lakini malipo….

**Interjection. Com. Lenaola** - toa pendekezo laki juu ya mnazi.

**Mr. Kazenga** - Manazi, mnazi napendekeza kwamba manzi ufanyiwe utafiti na kuwe kutaweza kuwa na factory ya kutengeneza eheh.. itwa je hii, whisky,…..pombe.

**Com. Lenaola –** Sema mnazi, pombe au whisky?

**Mr. Kazenga –** Pombe.

**Com. Lenaola –** Na mambao yake yote.

-.

**Mr. Kazenga** - Na mambo yake yote, all products. Nili kuwa na onge juu ya pension, kuna wazee wengi sana wame staafu lakini mara nyingi hua wana kufa kabla yakupata eh..marupu rupu yao ya uzeeni. Hili jambo serikali hua hata halitii manane. Na ni kwa sababu wale ame pewa jukumu ile wana ile tabia ya kutaka hongo ndipo watengeneza, na serikali ni kama ambao haioni. Labda pengine katika kaitba hakuna kitu kwamba kina saidia jambo hili, ili mwenye staafu, mwezi ule, ule wa kustaafu, apate haki yake, na endelee na maisha yake.

Education - Elimu ni kwamba hapa pwani sio kwamba vijana hawafanyi bidii lakini wanana pata sehemu elimu ya kutosha waingie university. Lakini hata wakienda kula wata chaguliwe zili sakafu kusema kwamba ni za hali ya chini, na wenzetu kule wapewe zile zinaitwa kwamba ziko marketable. Tunaomba hi irekebishwe.

Ah..hositali kuna hii kitu ina itwa cost sharing. Nafikiri watu wengi wame potesha maisha yao. Wenge sana wamepotesha maisha yao, kwasababu ya hii, kununua dawa. Sijui kama serikali ina umasikini huo kwamba haiwezi ika toa dawa bure kwa wananchi. Nasema hosipitali madawa yawe bure kwa kila binadam, maanake ana haki ya kuishi.

Eh..secutiry – Mkenya sasa imekuwa afadhali ule wakati wanyuma alikuwa ana usalama. Alikuwa ana weza kutemebea local wa kwake. Sasa imekuwa mwananchi ama wananchi wana uwana wenywe kwa wenyewe, na serikali ni kama ambao haioni. Ninge pendekeza kidog hili jambo liangaliwe. Nasema rais wa Kenya asiwe juu ya sheria. Aweze kushtakiwa ikiwa ame fanya makosa. Aweze kuondolewa katika uongozi ikiwa ame fanya makosa. Kwa hivyo Katiba itengenezwe, katika hali ya kwamba raisi awe anaweza yeye kushtakiwa, ama kuondolewa kwenye uongozi wakati wowote ule mwananchi atakapo pendekeza. Ni kwamba serikali iwe ya mwananchi mwenyewe. Rais awe mtumishi, sio bwana. Mbunge awe mtumishi sio bwana.

**Interjection Com. Lenaola –** (inaudible)

**Mr. Kazenga** - Ahh.. Ninasema narudia pale, pale mwanzo ni kwamba nina pendekeza serikali ya Majimbo. Asanteni.

**Com. Lenaola** - Bwana Mwimunye – welcome.

**Mr. Boniface Mwimunye** - Asante sana Commissioners, nita fanya yangu yawe mafupi. Kwanza nina pendekeza ya kwamba katiba yetu iwe na Preamble ambayo ita kusia objectives za Constitution yetu ita vet rules of governance vile ambavyo

Kenyans wanafikiria wange hitaji wawe governed. Niki gusia kuhusu Constitution Review, nina pendekeza ya kwamba kila miaka ishiri ama ishiri na mitano isipite ishirini na mitano isiwe china ya miaka ishirini, Katiba ya Kenya iwe ina kuwa reviewed for adequacy, ili tuweze kujiulize sisi wa Kenya hii katiba yetu ije ika liendelea kututosheleza ama la. Tuweze kuibadilisha wakati mambo yanavyo elekea.

Lakini pia vile, vile, wale wataalamu Constitutional ehm…Lawyers, wawe wana weza kuangalia vile vitengeleo katika Katiba ambavyo haviwezi kugeuzwa na parliament. Ili kwamba ile main framework ya Constitution iwe ina ngojea ah review billwords Lakini yale madogo, madogo, parliament inao uwezo wa kufanya amendment while they sit.

Nita kuja kuhusu, nita gusia kuhusu basic rights, kwa ufupi tu nina taja kwamba basic rights tuwe katika Katiba time taja ya kwamba food ni basic right water, health care education, haya mambo haya ina husu maisha ya wananchi the public, kwa hivyo Katiba iwe ina provide ya kwamba hii ni basic rights. Kama vile ambavyo Civil na Political rights, na Social Economic and Cultural Rights, haya mengine pia tunawe tuwe tuna weza ku ya provide.

Niki gusia upande wa education, nina pendekeza kwamba kuanzia standard one mpaka standard eight, yani youth wa Kenya mpaka miaka kumi na mitano, primary education iwe free. Primary education….sorry. Primary education iwe compulsory up to the age of fifteen years, Primary education is compulsory, awe ni mke, awe ni mume, ana takikana kwamba aende shule. Mahali popote katika Kenya hii; awe yuko Masai land ama yuko Pwani, ama yuko Central, awe anaenda shule. Lakini pia katika hapo nina pendekeza ya kwamba, kutokea standard one mpaka standard four, hio education iwe free. Kwa hivyo nime tafautisha katika miaka minne ya kwanza, ile education ni free. katika ile miaka minne ifuatayo it is compulsory but you pay for it. Hii ita wezesha sisi tuwe tuna waendeleza wasichana na wavulana kisawasawa.

Niki gusia kuhus natural resurces, nina furaha ya kwamba yale ambao labda ninge kuwa nime yataja kwa urefu, tayari yamegusiwa, lakini nita fafanua. Nina ona ya kwamba lands forest mineral resources, hizi ni natural resources ambazo Katiba yetu iwe ina provide ya kwamba they are to be protected, not to be misused. Na niki sema hivi nina gusia ya kwamba kila region ama kila district katika Kenya yako mazao, maanake taifa hili liko agricultural based, yako mazao. Mazao haya, yawe yana weza kuwa identified ili yawe developed for economic growth of the country. Hapa umetajwa huu mti eh..wa mnazi, mimi nina geneneralize ya kwamba huku tuna zungumza kuhusu mnazi lakini mimi nita zungumza pengine kuna mkahawa, kuna mchai, iwe iko provided ya kwamba the natural resources ambazo zina leta economic growth to that region, should be developed, for prospertity. Hapa ndipo ambapo tuta pata employment, hapa nipo ambapo tutapata sababu ya kujenga ya kujenga barabara ya lame, kuleta saafi. All the infra structure zita kuja kama vifaa hivi, ama mazao haya yamekuwa developed.

Nita rudia kidogo kuhusu Katiba. Ninge pendekeza ya kwamba kuwe na public sensitization on the Constitution. Na hii isiwe tuna ngojea tu mpaka tuna review constitution yetu. Tuwe na utaratibu wa kwamba katika mashule yetu kuanzia primary tunayo yale ambayo tuna weza tukaya fundisha na yaka eleweka hasa kwa watoto wadogo. Tuwe tuna incalculate value ya

Constitution yetu kwa watoto wetu kuanzia umri ule udogo, mdogo. Yaani waendelee kukua waki elewa ya kwamba kuna constitution ambayo ina walinda haki zao. Kwa hivyo, tuta ona ya kwamba tutaweza kufunza utaratibu katika kiwango cha chini kabisa katika mashue yetu.

La mwisho na muhimu kabisa, ninge taka ku pendekeza ya kwamba, objective ya Constitution, ni kwamba, the governed, should be properly governed. Lakini tunaona ya kwamba hakuna feed back. Ninge pendekeza ya kwamba kila miaka mitatu, huwe kuna independent office ina weza ikawa ofisi ombudsman ambaye yeye atakuwa ana andika report how this country has been governed over the last three years, katika areas zote muhimu iwe ni Human Rights, iwe ni Education Provisions, iwe ni Public Service Provision, aangalie hizi atowe report, and this iwe ni Public Report. Tuwe tuna weza kujua sisi kama rahia vile tume kuwa governed namna gani. Ni muhimu ya kwamba ofisi hii iwe entrenched katika Constitution ili kwamba iwe free and fair. Nina shukuru sana.

**Com. Lenaola**- Yuambie jina lako

**Mr. Boniface Mwamuye** - Jina langu mimi ni Boniface Mwamuye. Boniface Mwamuye.

**Com. Lenaola** - Sasa, bwana Peter Mwamuye, peter Mwamuye

**Mr. Frederick Jilani** – mzaliwa wa Chwonye. - Nina mawili matatu tu. Kwanza niki anza napendekeza kwamba serikali iwe ya Majimbo. Pili nina pendekeza kwamba, nguvu ya rais ya kuchagua mawaziri awe ana wachagua halafu, awe ana peleka mapendekezo ya uchaguzi wake kwa parliament for approval.

Nominated member of Parliament. - Mimi katika maoni yangu nina pendekeza kwamba hii member of parliament wakuchaguliwa waondelewe lakini tuongeze viti vya wabunge kwa sehemu zili za division and so forth. Ni mapendekezo yangu. President ninge pendekeza awe na terms mbili za miaka mitano, mitano. Maendeleo, - mimi nina pendekeza kwamba hii DDC ambayo ni District Development Committee ziondolewe. Badala yake , viwekwe Village Development Committee ambazo hizo zita kuwa na uwezo wa kujua hapa sehemu hii haija endelea ikiwa ni barabara, ikiwa ni maji, ikiwa nini kwa sabau wao wanajui mahitaji yao. Lakini DDC ina sema ime pitisha, na hakuna chochote ambacho kina fanyika. Pia katika hio, hio Village Development Committee, kuwe na locational of money ambao wana patiwa DDC.

Umri wa president huwa anaweza kuchaguliwa kama president, mimi ninge pendekeza iwe miaka arubaini na mitano. Ndiyo achaguliwe kuwa president, maanake ame kuwa mature, anaweza kujua shida za mwanawe, mtoto, mjuku, eh, kwa hivyo ninge pendekeza iwe miaka arubaini na mitano. Education ….

**Interjection Com Lethome** (inaudible)

**Mr. Jilani** - Miaka arubaini na mitano kwenda mpaka….

**Com. Lethome –** Ahadi mingapi?

**Mr. Jilani.** Ahadi sitini. Kutoka arubanne na mitano kwenda mpaka sitini. Ahh..kuwe kama vile ambavyo nime sema, kuwe na Majimbo kuwe na Regional Assembly ambao hapo kila district ita kuwa ime chagua representative wake. Nafikiri pengine nikirudia hapo ikiwa nime sikusahau, ni kwamba zile powers za president awe anaweza kuchugua mawaziri lakini apate kibali kwamba fulani huyu yu afaa, kwa parliament, ndio sasa iwe na…vile vile hata kule kuchagua Mabalozi au ah. Attorney Generals, and zile sehemeu ambazo zina takikana. Awe ana chagua ana suggest, halafu yeye ana peleka parliament for approval. Hayo machache, nafikiri mengine mengi ya gusiwa na wenzangu. Hasanteni.

**Com Lethome -** (inaudible) –Upande moja ulisema tusiwe na wabunge maalum, na wana apointiwa Kwa sababu ltunajua kuwa hawa hua wana akilisha (inaudible) sasa hao unge penda mahitaji yawo yawakilishwe kikundi kama akina mama, kuna watoto kuna walemavu, mambo yawakilishwe na nani bungeni?

**Mr. Jilani –** Ah..nina sema wakiweko kwasabu, wao wakati mwingi hua anaenda ilo nyimmbo ya yule yule alie mchagua tu.

**Com. Lethome** - Alie mchagua?

**Mr. Jilani -** Eh.. ikiwa ni president, maanake yeye ana chaguliwa apige vote ya ku, ya kuunga mkono serikali tu. Lakini ile interest ya wale ambao ameambia kuwa awe nominated ili awapelekee maombi yao, hana. Lakini ikiwa yeye atakuwa ni mjumbe amechaguliwa na wao wananchi wana weza waka seme wewe, mwaka ujao miaka miwili hatutakuridisha tena.

**Com. Lethome** - Sasa wao interest yao ina wakilishwa na nani?

**Mr. Jilani –** Ina wakilishwa na member of parlieament, ndio interest yake.

**Com. Lethome –** Kama akina mama wachaguliwe, wasio kuwa na uwezo na watu kilema wachaguliwe.

**Com. Lethome** - Mimi nina sema hivi, au nina pendekeza hivi waakina mama wapigania kama vile vile wanaume. Kama vile ambavyo wengi wao wana sema wamekwende Beijing sijui wapa kwamba wao wana taka ile usawa. Kwa hivyo wakiwa wana taka usawa basi, waingie kwa wananchi wao wenyewe wajipiganie. Ehh, kama wale waume vile vile, ndio usawa ule. Eh…kwa hivyo, mimi ninge pendekeza kwamba badala ya nominated member of parliament, tu ongeze viti vya parliement. Ni

hayo tu.

**Com. Lenaola** - Nataka kuwajulisheni mwenzetu Mama Kamishona Phoebe Asiyo. Ame chelewa kufika. Uwamukie watu.

**Com. Phoebe Asiyo** – Habari zenu wananchi

**Chorus** - Mzuri

**Com. Asiyo** - Poleni sana nime chelewa kidogo lakini sasa kasa moyo sikiza maoni yenu, na nina ona tayari wengi wame jiandikisha.

**Com. Lenaola** – Peter Mwamuye Chando, halafu Babto Thomas, uta mfuata huyo.

**Peter Mwamuye Chando** - Jina langu ni Peter Mwamuye Chando. - Serikali ninayo taka mimi ni Federal Government, point one, na president moja, atakae tawala katika inchi hii katika Federal Government. Bunge ita kuwa na senate ambayo ni kama upper house. Tuta kuwako bunge lingine tena ita kuwa, National Assembly. Bunge lingine litakuwa Regional Assembly. Sasa huyu president asiwe na powers za ku nominate members of parliemaent. Tusha fika hapo. Kila jimbo lita kuwa na governor wake. Army ita kuwa moja. Kenya Army, one Armed Force, ambayo ita kuwa answerable to the senate. Haiwezi kuingilia nchi yeyote ya nje bila approval ya senate. Hii ni army. Police wata kuwa wa Majimbo, Police Regional Agent, PrisonR regional Agent. A.P. wafutiliwe, hatuna haja na A.P, hatuna haja na G.S.U. Kila jimbo polisi wake, kila jimbo na jela zake, na administration zake tafauti. Recruitment ya watu kwenda campus, university, kila jimbo litakuwa na university zake. Lita kuwa na haki za ku interview wanafunzu na kuwaingiza katika vyuo vyao katika Majimbo yao. Hii ni upande wa elimu. Polis nisha maliza.

Habari ya judges. Majaji hawa wata kuwa kama Chief Justice, ana takikana awe na umri wa miaka hamsini mpaka sabini awe ame retire, sabini. Jaji wa kawaida, awe na miaka arubaini na mitano. Magistrate anaweza toka campus akawa magistrate mara moja.

Ministers – President achague mawaziri kulingana na record zao, file zao. Wame ishi namnagani, wamesha kuwa kotini, wame kuwa mamna gani. Mawaziri kama hawa wametowa kotini, wasiruhusiwa kuwa cabinet ministers – records zao ikiwa ni mbaya. Attorney General, si lazima apigiwe kura. Huyu atakuwa aki chaguliwa na president, lakini nae lazima awe na record safi kabisa, kuweza kuitetea nchi, kimataifa na katika serikali, ikishtakiwa. Awe ni wakili wa hali ya juu. Mapato ya pesa za Majimbo, seventy five percent ibaki katika Majimbo. Twenty five percent iende katika serikali kuu.

Wanawake, wanawake nao waweze kupewa nafasi zaidi katika bunge, yaani tuweze kupata mazungmuzo yao katika bunge.

Wanawake hawa wame wachwa nyuma kwa katiba na leo katiba tuna anza mpya, wapewe nafasi zaidi wanawake katika bunge.

Elime kwa watoto wa primary, iwe bure, kutoka standard one mpaka standard eight, serikali ifanye Majimbo wenyewe watu kama wanataka Majimbo zao, watengeneze lakini wapate elimua ya bure. Hali ya barabara, sitima ita tengezwa katika Majimbo. Sina memorandum nyingine, hali yangu ni Federal Government peke yake

**Com. Lenaola –** Asante sana- ngoja kidogo.

**Com: Asiyo -** Sasa una fikiria kwamba inge faa akina mama wapewe nafasi zaidi kwa vituo kama ya bunge na pia pengine kwa…serikalini. Ni njia gani ambao ina wezesha wanawake kufika kiwango kama hizo? Kwa vile kama sasa una jua vile walivyo, ni vigumu baba akipata pesa, vile wame kuwa maskini wana tuma vijana pekeyao shuleni. Halafu pia serikali haija kuwa na nia ya kuweka wana wake mahala ya kusaidiana na wanaume kwa mambo ya kuletea (inaudible)

**Mr. Chando –** Kweli mama. Waakina mama hawa wakina dada katika skuli pass yao ya kwenda campus ipunguzwe. Kama ni B+ - waweke B au B-, compulsory, waende campus. Hawa akina mama. Tukipata wakina mama wengi katika campus, tutaweza kupata viongozi wanawake pia, hawata weza kubaguliwa. Katika hawa uta pata mawakili utapata madaktri, utapata wakuu wa elimu. Wanawake wapate nafasi hizi. Maana katika kiwango cha sasa katika elime ina wabagua wanaenda chini. Ikikua ma B+ wakina mama, wakina mama wanapata C+, hawae…hawaendi. Lazima tuwa peleke juu kidogo. Ukielimisha mama, uwa ume elimisha dunia nzima.

**Com: Lethome –** Umesema kuwa ikuweko na viti vingi kwa akina mama bungeni, sasa hivi viti vya bunge ni viti ambavyo vita hesabiwa vyao tu au ni vitiambavyo vita gombania na n wale (inaudible) Is it reserved seats ama ni nomination?

**Mr. Chando -** They should not be nominated They should fight like others, but again ahh..no, I would recommend they should not be reserved for them, they should fight like others.

**Com: Asiyo -** Hebu nikueleze vile nchi zingine kama Tanzania na Uganda wana fanya, wao huwa wana (inaudible) tafauti. Kina mama wana simama kwa vyama vyao na wana kuwa na uchaguzi yao mbele ya ile general election. Kwa hivyo kila chama kina towa akina mama wa ku pigana na wengine kwa district, halafu yule amechaguliwa kwa district kwa hio chama chake ndio ina enda bunge kusimamia wanawake we hio district. Kwa hivyo unaweza kutpata wanawake kama, in Tanzania waaepata sitini na saba, kule Uganda arubaine na tano, ambao wana chaguliwa na watu tu lakini wanawake pekeyao ndio wanagombania hivyo viti vya akina mama. Sijui kama unge pendekeza vipi, mtindo huo wa ki Tanzania na Uganda?

**Mr. Chando -** Mtindo huo wa Tanzania ninge sema una faa, maana vile, vile huwapa nafasi akina mama zaidi. Nina kumbuka

kuna wakati ambapo serikali ili tafuta mama. Nafikiri ni wewe, ulikuwa mama wa kwanza kuwa Senior Superintendent of Prisons, kweli?

**Com: Asiyo –** Eh ni kweli.

**Mr. Chando –** Langata, nikiwa na wewe. Basi, wakati huo tulikuwa tuna jidai, kulikuwa wa Africa hakuna. Tukikuona wewe, tuna shukuru sana tunaomba Mungu. Lakini kulikuwa hakuna wanawake. Hawapewi nafa ….nafasi. Sasa tukiona akina mama kama vile wanasonga ma Assistant Commissioners, ma Deputy Commissioners wanawake hua tuna sikia nguvu, tuna pata nguvu. Tuwape nafasi akina mama.

**Com: Lenaola** . Asante sana bwana Chando. Mki penda kukueti kusikiza (inaudible)ni sawa, (inaudible)Kwa hivyo ukiamua kusikiza maoini keti – ukisikia huyu ukiamua una kwenda ni sawa. Tume elewana?

**Chorus –** Sawa.

**Com. Lenaola –** Kwa hivyo, Ravasco Kaisuma, nafasi ni yako. Joseph Lewa, Joseph Lewa, kaa hapo basi.

**Ravasco Kaisuma –** Kwa jina naitwa Ravasco Kaimuma – mkaaji wa Chwonyi Diani. Na ninge pendekeza kutoa maoni yangu kwa kamati ya tume ni kwamba ninge penda serikali isio ya katikati, iwe ya pembeni. Nikipendekeza serikali isiwe ya katikati iwe ya pembeni. Ikiwa ya pembeni ni kwamba ni serikali ya Majimbo. Serikali ya Majimbo ni kwamba ita ongoza kila mukowa kama sisi tuko mukowa wa pwani. Tutakuwa tume jivunia kwamba tuna jitawala wenyewe na kujitafutia kile ambao tutapata. Hata tukipata kidogo tuta shukuru maanake ndio tuna aambiwa tume pata. Tukipata kingi, pia tuta shukuru maanake tume itafuta wenyewe. Sio kutafuta halafu umpatie mwingine wa katikati aende akale, wewe ubaki ni njaa. Sisi hatutaki. Tuna taka tuki tafuta tupate, na wale wa katikati tuwaganyie asili mia ishiri na tano. Zile asili mia sabini na tano ndio ita baki hapa pwani tu fanye yale mambo yetu ambao tuna ya taka. Na kama Katiba ange andikwa namna hio, inge kuwa Kenya ina kuwa huru, na kila wamoja ange kuwa ina jitawala mwenyewe, sio kama sasa. Sasa, wa pwani wana tabu. Niki sema wa pwani kama sisi wa Chwonyi, kutoka uhuru, watu wame pata uhuru, sixties mpaka sasa, Mchwonyi haja jua uhuru, yuko tabuni sana.

**Interjection Com. Lethome –** Tabu ni zani?

**Mr.Kaisuma** - Matope mme ona, barabara matoke, mashamba hawaja andikishwa.

**Interjection – Com** - Pendekeza.

**Mr. Kaisuma** - Tuna taka mashamba tuandikishwe kama watu wa bara zile walipewa title deed, mpaka sasa wana jiendeleza.

**Com. Lenaola** – Endelea.

**Mr. Kaisuma** - Hapa kuna wazee. Hata (inaudible) Hajawahi kuuza shamba lake na title deed, nga apate nga' kujimfuraisha. Tuta weza kweli kusomesha sisi? Fee hatuna.

**Interjection – Com: Lenaola** - Sema mapendekezo …

**Mr. Kaisuma –** Sasa tuna penda ikiwa serikali ya Majimbo ita tuletea mapato kwetu nchini hapa pwani, kama Chwonyi nita sema tuna taka tuweke mitambo huu. Wa nazi, wamarifu, sisi nao tuta kuwa tunaweza ku jiendeleza na kujulikana Kenya nzima.

**Com. Lethome** - Wamarifu ni?

**Mr. Kaisuma** – Yale makuti. Pia sisi ni wakulima sio wavivu. Nakifiki mme pitia huko mka ona, kuna mihogo, pia tuki uza na kama tuna itupa tu. Kilo shilingi nane. Sio kazi ya kufanya, sio mkulima ata fanya hivyo. Sina haki Kenya ni huru, Kenya si huru. Tuna taka Majimbo na fikiri itakuwa ndio kitu cha kwanza kwetu uhuru hapa Chownyi.

**Com: Lethome** - kiongozi wa jimbo tumuite aje?

**Mr. Kaisuma** - Kiongozi wa jimbo ata kuwa governor. Lakini ma wa Chownyi atakuwa ata sema ni kama president wao. Maanake tutakuwa kila siku tunamuona tukimtaka. Sio kama raisi sasa. Hapa hakuna mtu yule wa chini anae mjua rais Moi. Ana ona kwenye pich, kwa gazeti, Lakini hajaonekana hapa Chowonyi.

**Interjection –Com: Lenaola** - Jambo lingine?

**Mr. Kaisuma –** Nime tosha hapo nashukuru.

**Com. Asiyo** -Kwa nini hio ita kuwa kwa kiwango gani, kwa mukowa au kwa district

**Mr. Kaisuma** - inaudible

**Com. Lenaola** – Joseph Lewa, Patrick kai

**Patrick Kai** - Mimi naitwa Patrick Kai. Eh, napendekeza hua ufumo wa sasa uwe ni katika Majimbo. Kwa kuwa kwa mwaka hii yote arubaini tulio kuwa, vidhaa yetu hapa pwani haija tatuliwa na serikali ile ambao tuli kuwa nayo. Niki guzia hapa nina anza kama hio korosho, mitambo wa korosho ume angushwa, nina angalia kama ni sukari Kwale, mitambo ume angushwa, niki angalia vitu vingine kama kundepojo muhogo, hau haija tambulika na serikali hii ambao ina tutawala kwa miaka arubaini. Ninapo pendekeza, kwa serikali ya Majimbo, hawa wote yule ambay ata kuwa ni governor ata angalia kuwa mimea hii yote wapende wakatae ni lazima wata tafutia soko la nje na hatimae ku muinua yule mkulima ambaye yuko ngazi ya chini kuamka.

Nina gusia tena hali kama ile ya mambo kama ya utalii. Chochote, kinacho patikana hapa kwa kuwa ni biashara, ishirini na tano inaenda kwa serikali kuu na sabini na tano iwe ita tekelezwa hapa. Kwa upande mwingine, tuna endelea.

Elimu. Ni aibu sana kusema ya kwamba miaka hii arubaini yote pwani haija kuwa na chuo kikuu. Na hata ingawaje hawajiwezi ki elimu, ningeli pendekeza ya kwamba, serikali inayo kuja angalo ipunguze mean grade za watoto hawa ambao wana soma wavulana kwa wasichana, kutoka Lamu hadi huko chini. Angalao ile mean grade iweze ku ingia kumvuta msichana, wa pwani na mvulana, angalao iwe in quarter system. Kujua ya kwamba katika pwani, yote mwaka huu tume wezesha kuingia watoto kadhaa university.

Hasa niki gusia kwa akina mama, tuta sema ni aibu, kwani si waakina mama wengi hata tukiwa hesabu katika, tuchukue kilifi kwa mfano ikiwa tutasema kama akina mama mia tatu ambao wana degree sasa, nafikiri ita kuwa, hio si, hawaja patikana kwa jumla. Hali hii ambayo tuna angalia kama tukiingia katika kwa mashamba, wale ndugu ambao wame pata ma title deeds, hali wenyeji hawaja pata, tungali onelea, au, ninge pendekeza ya kwamba hawa wapewe lease kwa kiwango fulani na shamba zile baada ya mda fulani, waziwache kwa wale wenyeji au wataendelea mazo wawe waki lipa na malipo yale yawe yata faidisha watoto wa hpa. Niki gusia katika kazi, viwanda vyote au kazi zozote zita kazo tokea katika mukowa huu, sabini na tano zipate wenyeji, ishirini na tano zipate wandugu zetu wengine, mbao hawa tuna jua kwa wakati huu, maana wame ingia katika vio vikuu, wako na tarima za juu kupata kama ma engineers na wengineo hapa. Tukuguzia katika mukowa pwani hatuja pata hata ma engineers kumi ama ishirini kwa kufika kama hapa. Walio pata hii ni mshahada kweli.

President, mamlaka yake napendekeza yapunguzwe. Na uteuzi wa wale watu kama, wale ambao wata pewa mamlaka na yeye ame wateua kama wabunge basi wa weze kuidhinishwa kwaza ki elimu. Mtu huyu akichukuliwa kama ame kuwa appointed na president ata ingia katika faculty gani kusaidia mwanan nchi ile wa kawaida? Mipangilio hii, niki taja hakuwa taunahitaji Majimbo, ni kwamba, kwa miaka hii yote njia zetu hazi riidhishi. Moto hauja tufikia. Ngasi za kiparty pengine wala hata simu zenyewe hatuja ziona. Kwa hivyo, napendekeza Majimbo iwapo governor ata tekeleza haya yote basi na wenyewe wafanye kazi kwa bidii, kwa hatuta chukua kamamuda mrefu, tuta weza kupata vitu hizi.

Mahospitali – Ni aibu kusema kwamba, kama Wachwonyi, kwa miaka hii arubaini hatuja kuwa angala na sub hospital. Watu wanapo fariki tuna pata shida sana. Costi general ama kilifi. Na si wote ambao wana uwezo kwa kuwa pengine watu wao wanapo fariki wana weza kuwapeleka kule. Garama zime kwenda juu. Nina pendekeza ikiwa serikali ya Majimbo ime ingia iweze kujenga mahosipitali ya kisasa, na iweze kuleta huduma hizi za ambulensi kuwa karibu pamoja mortuaries za kisiku hizi.

Nafikiri nikimalizia ni elimu ya watoto wa darasa la kwanza hadi la nne. Serikali na pendekeza ya kwamba, mimi napendekeza ya kwamba wale watoto, serikali iwe ita angalia criteria yote. Lakini hawa kama ni ma headmaster, wawe watoto wale hawata wacharge hata penny moja kuwezesha kila kabila, watoto wata weza kwenda mashule. Le si ile kusema tuna taka building funds, tuna taka watchman. Watoto wa darasa la kwanza hadi la nne wasio wana malipo yoyote. Pia nina pendekeza, tunapo enda hadi darasa la nane, kwa kuwa watoto hawa ni wadogo, nina pendekeza msomo huu wa elimu wa nane nne, nne, hapa tuwe na bridge ya form five form six, ili wanapo ingia form five….university, watoto hawa wawe wame komaa. Ni hayo tu.

**Interjection – Com. Lenaola** Asante sana Bwana Kai, jiandikishe pale, sasa Rebecca Ndombo.

**Rebecca Ndombo** - mimi kwa jina nina itwa Rebbecca Nzombo – Mapendekezo yangu ambayo nime yaona. Ni kama yule msemaji alio sema mbele kwa katika mambo haya yalikuwa ni, tutayarishwe ili ndio tuyajue. Hata mimi nime zinika hapa na wale ambao wame tangulia kusema. Lakini nilikuwa sina ujuzi wowote juu ya mambo hayo. Kwa hivyo nita toa mapendekezo kidogo ambao nime ya.. Pendekezo langu ni serikali ya Majimbo. President ata kuwa moja. Na ita kuwa rahisi ikiwa ni Majimbo kwa ita kuwa ni sehemu ambayo yule atakae kuwa muongozi atakuwa yuaijua vile ilivyo, kwa kuwa ita kuwa si kubwa sana. Ata jua matatizo yake na raha yake, ndio na pendekeza. Hasa hapa kuna matatizo ya barabara. Barabara ni kama zile ambavyo mmeona ni chafu. Barabara inatatiza wagonjwa hasa akina mama ambao ni wajaa awazito, husumbuka sana ikiwa wana taka kusafirishwa kwenye hospitali ambazo zina taka tuka wa humie.

**Interjection – Com. Lenaola** - Pendekezo ya mambo kama hayo?

**Ndombo** - Upendekezo wa mambo kama hayo, ninaona Majimbo, yakiwa yako yatajua matatizo hayo kwa urahisi. Kutuma za, barabara zetu zikisha tengezwa, na huo usafirishaji pia uta kuwa rahisi. Na wa pwani, kuna matatizo ya mambo ya mashamba. Wengi wetu wanaambia ni maskota. Hawana vibali. Nakutokana na wengine ambao hata hatufahamu, tuna fanya kuona tu mtu amekuja na title yake, anasema mahali pale ni mahali pake. Sasa sisi hatujui, tuko tu, tuna ishi lakini, sio wenyeji wa hapo. Tanaishi tukuja, akuja yeye mwenyewe, ana ondoa watu kwa gafla ambao hua wana stajabu sana kuwa mambo haya hua yametoka wapi. Lakini najua ikiwa ni Majimbo, wata zijua matatizo hayo na wata ya tatua.

Watoto wetu hawana kazi Na viwanda vinavyo tolewa vya kazi, hata wakiandika mabaruwa ikifika huko ata ona mahali pale pame jaa, ambao hua hata hafahamu kuwa mambo yame pita kivipi. Na hata wengine sio kuwa huwa watu wa karibu kama

huku pwani. Ingawa wata fanya nusu au kama robo aka waandika. Sasa utakwenda ukaone wote waliojaa pale ni wale wageni. Sasa yale pia hua matatizo kwetu.

**Interjection - Com Lenaola –** Mapendekezo yako..

**Ndombo –** Napenkeza Majimbo yatatue mambo hayo yote, kwa kuwa watakuwa wako karibu, na kile upande watajua matatizo yao na raha zao wata zifahamu. Na upande wa bunge, tuna penda wanawake wapewe nafasi, kwa kuwa wanawake ndio wanaojua tabu za wanawake wenzao vile vilivyo nao wana weza kupeleka kule bendele ili zika tatuliwe. Sio waseme wanawake yale ya zamani hawaku kua wako nyumb yamekwisha. Na kwa sasa ni hayo tu.

**Com Lethome –** Mama ninge penda kusikia kutoka kwako, uriithi wa mwanamke ikiwa ame olewa, sijui unge sema nini.

**Ndombo** - Uriithi wa mwanamke, mwana mke na mwana mume wote wako sawa. Na hata zile shamba pale nilipo kuwa mimi na baba yangu, tulikuwa tuki fanya kazi na wale watoto wakike piya walikuwa wakifanya kazi katika hayo mashamba, kwa hivyo hawo pia wana uhuru wa kupewa sehemu yao.

**Com. Lethome** - Wariithi kwa baba na kwa mume?

**Ndombo** - Hawo kwa mume basi ni yao huko. Lakini huku kwa baba ni …

**Com. Lethome** - Nataka upendekeze

**Ndombo –** Napendekeza wapate uriithi.

**Com. Lethome –** Kwa mume ama kwa baba

**Ndombo** - Kwa baba pia.

**Com: Lethome -** Kote huko na huku?

**Ndombo** - Sasa ya kwa bwana basi nita yajua mimi, kwa baba ni mimi na yeye babaake. Au ni mimi pekeyangu naweza kumpa, lakini huko kwa bwana.. sijui….

**Com. Lethome** - Una jua ya kwamba tuna tengeza sheria. Tunapo tengeneza sheria sikuangalii wewe. Muangalie huyo binti ambaye ni msichana wako awe ni msichana wa wengine, leo na kesho na miaka ijayo. Unge penda je, wasichana wakisha

olewa wariithi kwa baba pekeyake ama arithi kwa mume na kwa baba? Pendekeza.

**Ndombo –** Kote, kote wata ariithi.

**Com. Lenaola –** Thank you very much mama. Sister Wacera. Jiandikishe mama pale.

**Speaker –** Lakini kama hatuja ruhusiwa ku uliza maswali pengine utasema je, ikiwa tukona na swali.

**Com. Lenaola**. Hapana. Ni sisi Maoni si, Maoni si kwetu, maoni ni kwenu. swali yatoka kwetu (inaudible) haya endelea sister. Sema jina halafu uendelee.

**Sister Katherine Wacera** - Kwa majina naitwa sister Catherine Wacera, na nina mapendekezo ambapo mengi ni yale yamesha semwa. Natilia nguvu tu pale ambapo naona pana umuhimu. Kwanza kabisa napendekeza kuhusu president Umri wa president uwe una wekwa, kuanzia miaka arubaini na tano hadi sabini. Pia education level yake kabla haja kaguliwa kuwa president iwe ime chunguzwa kisawa.

**Interjection –Com: Lenaola** - Sema pendekezo.

**Sis. Wacera –** Ninge pendekeza kwamba akichaguliwa awe educational level yake ime chunguzwa vizuri.

**Com Lethome –** Kiwango gani, kiwango gani ya masomo, standard three, form four

**Sis. Wacera** - Form six, university, awe anaweza kuwa president. Ah..pia katika kuchaguliwa kwake, uwe kuna terms za five years, kama ilivyo kuwa lakini asichaguliwe zaidi za terms mbili. Hours za president, asi pewe mamlaka kama ilivyo sasa. Awe, ikiwa ame kosa mtu awe right ya ku msitaki. In this I suggest judges pia wawekewe security of tenure. Kwa sababu ikiwa hawata kuwa na security, kwa case haita wezekana kuwa ikimshtaki rahisi uta weza kushinda maanake sasa pia ata ji defend, na hata weza kutoa uamuzi ambao ni sawa. Katika uchaguzi wa M.P. Ni kama wenzangu walivyo sema ninge pendekeza wanawake wawe na viti sawa na wanaume. Na kama ilivyo kuwa hapa mwanzo, ule yale tume elezewa hapa kuhusu Tanzania wanavyo fanya ninge pendekeza kwamba ifanyike hivyo, hivyo. Pia katika wale nominated mps, ninge pendekeza katika serikali ambao una kuja, kama ume kuwa nominated, ipelekwe ili ipendekezwe kwa wabunge, halafu wabunge wapitishe ikiwa ni sawa ama si sawa. Isiwe tu president, ndio ame fanya mamlaka na ame pitisha. Kuhusu wanawake kuingia katika campus, ninge penda kumuunga mkono Mwamuye, kw yale alio pendekeza kwamba ikiwa katika wale wanao ingia katika elimu ya juu zaidi ni vizuri the grade iwe lowered kidogo kwa wanawake. Ndiposa tuweze kupata wanawake zaidi, wenye elimu ya hali ya juu.

Pia ninge pendekeza kwamba, katika kumiliki shamba, na women's, rights they should be valued, kwa sababu, mwanamke ni mtoto kama vile wa kiume. Na ikiwa wakiume ana haku ya kuriithi, hata mwanamke ana haki ya kuriithi. Kwa sababu, tukisema mwanamke asi riithi ni kufanya kwamba si mwanadamu. Ni mnyima haki zake kabisa. Kwa hivyo ninge pendekeza katika hii constitution hile jambo liangaliwe sana na zingatiwe. Kwamba mwanamke apewe the same rights as a man can be given. Halafu uki angalia katika ku waakilishi katika ki kazi. Pia waangaliwe. Maanake wanawake wengi wana weza kuongoza hata vizuri zaidi ya wanaume wengine wanazifanya.

Katika mahospitali na hasa zaidi, kwa ajili ya eneo hili, ninge pendekeza iwapo serikal inge angalia. Waache kuangalia distric, ati district kuna endelea aje, waangalie villages kuna endelea aje, Chwonyi kuna endelea nini, Mariakani kuna endelea nini, Kaloleni kuna endelea nini. Si kuangalia tuseme Kilifi district ina endelea vizuri ili hali wengine wana teseka. Kwa hivyo, hizi mahospitali ziwe karibu; na hasa jambo kubwa ambalo nime ona kwa kuifadhi maisha. Kuna shida. Mtu hawezi kufa halafu tuna safirisha mpaka Mombasa tena tuna rudisha hapa ina kuwa ni matatizo. Kwa hivyo ninge pendekeza sana hio iwe.

Pia tukiangalia, sawa, tukiangalia katika rights of worship, ninge pendekeza katika serikali inayo kuja waangalia sana madini yanao chupua. Kwa sababu tukiangalia kama mungiki. Wana vunja mambo. Wana fanya kinyume na mapenzi ya mungu. Wana uuwa wana fanya nini. Halafu seme wako na rights of worship. Kwa hivyo ninge pendekeza sana, vitu kama hivyo ziwe ziki angalia. Pia security, hasa kwa watu yeyote, mtu yeyote yule ambae ana fight for huma rights, awe na security wa kutosha. Hasa zaidi niki angalia unaweza uka kupendekeza kitu ambacho una pigania rights ya wanadamu. Lakini unaambiwa wewe ni mtu wa kanisani. Ushughulike na ya kanisani. Lakini yale tunao shughulikia haya tafauti na ya serikali, maanake we are fighting for human rights and even in the church, we are fighting for human rights. Kwa tuwe na uhuru wa kupendekeza tunapo pigania haki za mwanadamu. Tukiangalia, mengi yamesha tokea, hata mauaji kadhaa, kwa ajili ya mtu ambae amesimamia huma rights. Kwa hivyo ninge omba hio security iwe, kwa kila binadamu ane taka kuongea kuhusu human rights.

Halafu pia ninge pendekeza, katika reviewing of the constitution, ni vizuri after some years, tuna ambiwa tume fikia wapi. Na ni vipi serikali yetu ina ongozwa. Sio tu tuna kaa mpaka tutakapo review the Constitution again. I would like this to be in the consititution, in the new constitution, ndio iweze kupendekeza zaidi, ni after how long. Lakini Kwangu mimi ninge sema baada ya miaka mitatu, kwa sababu wako karibu kumaliza term yao wale wako pale, ina kuwa mpaka miaka tatu wame tuongoza ki vipi. Wana tuelekeza wapi, ama wametuendeleza ama wame turudisha nyuma.

Halafu the basic rights ziwe zime kuwa zame pewa kila mtu, kulingana na mahitaji ya kila pahali. Tukiangalia kama eneo letu, ni wengi ambao hawaja soma, kwa hivyo ni mapendekezo yangu, ya kwamba from class one to class four, hapo ni mahali ambapo unweza kuwa ume jifunza kuandika na kusoma. Wengi wetu hapa katika eneo hili hatujui ku andika na kusoma. Kwa hivyo hata mnapo tuita kusema maoni yetu kuhusu constitution, hatujui ni mnyama gana, na ndio maana hatuwezi tukatoa maoni yetu ni ili hali hayo maoni yange yaku faa na ya ku fanikisha hapa mahali petu. Kwa hivyo from class one to class four, at leat masomo yawe bure, na kuanzia hapo, yasiwe tena ya zaidi ya hali ya juu kiasi ya kwamba mtoto hataweza fikia eight. Halafu

kwa kuingia form four nakuingia university, ni kama nilivyo sema hapo hawali.

Pia tukiangalia natural resources. Ina kuwa kila mahali kuna kitu ambacho kina weza endeleza wale watu. Mungu alipo kuwa aki umba nchi ame umba akijua hawa watu watakuwa supported na nini. Kwa hivyo, tukiangalia mnazi yetu ni mnazi ambao kuna fagio zina toka pale, kuna mafuta yana toka pale, kuna pombe ina toka pale, kila kitu ambacho kama serikali inge kuwa imetusaidia na vifaa, namna ya kujiendeleza, Chwonyi hainge kuwa ilivyo, tune kuwa tume songa mbali sana. Kwa hivyo natural resources kupitia kwa serikali watusaidie kujiendekeza sisi wenyewe. Tusitegenmee tu tupewe kutoka juu, na hili hali mazingira yetu yana tutosha kutoa kile ambacho tuna pata.

Tukiangalia pia kama mihogo hapa pia wana panda vitu kama rice. Hivyo vitu kama tunge pata marketing ambao iko nzuri, kwa kweli watoto wengi hapa wange enda shule. Ninge penda serikali iangalie mambo muhimu hasa ya marketing, friom the grass roots. Wasiangalie marketing ya vitu products from Kenya nina zile ziko pale chini tuna waacha watu kutekeka. Asanteni sana.

**Com Lethome –** Ume sema majaji wawe na security njema ili waweze kutowa uamuzi bila kuogopa, kuwa wata kosa heshiwa yao. Lakini ninge penda tu useme wateliwe na nani wale majaji – ni pendekezo

**Sis. Wacera –** Ninge pendekeza wale majaji wateuliwe na…, asi ateuliwe tu na president pekeyake. Kama nilivyo sema wabunge wale wako nominated, wasi nominatiwe na basi wakiwa nominated imekuwa ime pitishwa tayari. Wa nominatiwe na ije kuwa confirmed in the parliamentary meetings. Sasa ninge pendekeza hata hivyo, na hawa majaji wanapo chaguliwa wasichaguliwe tu na president na kuwa ime tosha. Wachguliwe na pia ipitishwe katika members of the parliament na wale ambao wame teuliwa kuwa wata akilisha hili jambo, ili wapitishwe kama wana faa ama hafai.

**Com. Lenaola –** Asante Sana, jiandikishe pale. James Karisa –

**James Karisa** - Hamjamboni – mimi kwa jina ninaitwa James Karisa, ambaye ninaishi hapa Chwonyi. Jambo la kwanza kuhusu katiba hii yetu ambaye tuna ipanga, nataka serikali hii yetu iwe ya Majimbo. Kwa sababu nina ona ya kwamba ikiwa ni ya Majimbo, tuta, wale viongozai wa Majimbo wata jua shida za jimbo lao. Na pia katika hayo Majimbo, wata kuwa kila mmoja, kila jimba lita kuwa lina bidii wenyewe ku jiinua. Hii serikali ya umoja, nimeona ya kwamba ina tu didimiza. Wengine wana kuwa wavivu kwa Majimbo yao kujiendesha. Kuhusu, kuhusu, yani yule mkubwa wa jimbo awe ni governor. Governor na wajumbe wake wata fanya mipango yao wenyewe, wata kuwa na bunge lao. Kila jimbo lita kuwa na bunge lake.

Na, kuhusu waendeshaji wa … nina enda kwa upande wa ukulima. Naomba ya kwamba ikiwa tume kubaliwa serikali hio ya Majimbo, basi title deeds, uwezo isitoka Nairobi. Kila jimbo au kila district iwe na uwezo kwa kuwapatia watu wao title deed. Mashamba kila district itakao kuwako, waki pimiwa, waki pima mashamba, wao katika hio district iwe na uwezo wa kutowa

tayari title deed na kuwa patia wenyewe. Isiwe ni juu huko, itoke huko title deeds zije huku. Ndio kuna kuwa na confusion ya hizi title deeds. Uko hapa una shamba lako, mwenyewe ume buni shamba lako, na una ona mtu anakuja na title deed yake kutoka huko juu. Ina kuja ana kuja anasema hapa ni pangu. Uki angalia kweli ana title deed. Na huyo haja kanyaga maisha yake hapa. Haya yana ndio yana fanyika na hii serikali kuu, ambao tuna ona kuna makosa inayo tendeka. Kwa hivyo title deeds zitolewe kila district wawe na uwezo wa ku wapa.

Haya matibabu, hosipitali, naona, ikiwa serikali ime kuwa ya Majimbo, kila jimbo lita kuwa lina juwa ya kwamba kwa nini tuta fanya nini mpaka watu wetu watoshelewi kwetu kwa nini, kwa utabibu. Isiwe mapka huko yapitishwe huku. Kuhusu upitishaji kama ulivyo ni kwamba, yote yana pitia katika D.C.C. Yaki fika kwenye D.C.C, basi yapitishwe mpaka mbele. Hata yakifika huku, mengi yame achwa, yane chaguliwa tu kidogo. Kwa hivyo, ndio naona ya kwamba, tuna unyonge kupitia hii serika yetu kuu moja. Tuna unyonge sana. Wengine, hapati usaidizi wa kutosha, kwa sababu D.D.C zina panga hili, ina peleka mpaka Mombasa, zininge yana teremshwa mpaka huko, lakini anachukuliwa moja ndio lina fanywa au ni kufanywa (inaudible). Kwa hivyo, nina ona kuna udhaifu kwa serikali tuliokuwa nayo. Kwa hivyo ndio tuna taka majimbo.

**Interjection – Com Lethome –** Hii D.D.C – unge pendekeza nini, hii D.D.C?

**Mr. Karisa –** Hii D.D.C. naona ya kwamba ikiwa serikali ya Majimbo ita kuwa liko karibu na D.C.C, au sio D.C.C haita kuwako, isiweko.

**Com: Lethome –** Na badala yake kuwe na nini?

**Mr. Karisa –** Badala yake tuwe katika ile, vile ambavyo kamati zitakuwako, ikipitishwa tu, zina pelekwa kwa jimbo maramoja.

**Com: Lethome -** Ita kuwa katika daraja gani, kwa unajua, DDC iko katika daraja ya wilaaya. Sasa hii kamati unayo pendekeza wewe iwe katika daaja gani?

**Mr. Karisa –** Hii nafikiri sita weza kulijibu hilo swali.

**Com: Lenaola –** Asante sana. Jiandikishe pale bwana Karisa.
Halafu Nyanga yuko, hayuko, Erastus Jembe,

**Mr. Erastus Jembe -** Kwa majina naitwa Erastus Jembe. Mimi ninge penda ku changia pia katika utenegenezaji wa hii Katiba mpya,ambayo ina andaliwa kwa miaka ya usoni. Hapa mimi mapendekezo yangu ninge taka katiba hii ambayo ina andikwa iweze kuruhusu mukfumo wa serikali ya Majimbo. Hii ni kwa sababu serikali hii ya Central Government ambayo tume

kuwa nayo, kwa hakika tume ona kwamba maeneo mengine yame inufaika, ili hali mengi yame dhulumika kwa upande mwengine. Kwa sababu haku kuwa na ugawaji wa mapatao sawa.

Kitu kingine ninge nina taka pia hizi Local Authorities, pia ziwe zita angaliwa vilivyo hasa mshahara ya hawa ma councillors, kwa sababu tuna ona kwamba, wakati tunapo chagua hawa wabunge, huwa wakati mwingi wana kimbia kwa sababu, wakienda Nairobi wana kaa huko na hapa masinani tuko na ma councilors. Lakini tuna ona kwamba mishahara yao wakati mwingi ina angaliwa na mabaraza, na mabaraza mengine hua pesa zao, hawana njia nyingi za kupata pesa kwa hivyo mshahara ya ma councilors ina kuwa ni kidogo na wakati mwingi tuna wa shirikisha katika harambee na wakija hawana kitu. Kwa hivyo ninge pendekeza mishahara ya madiwani ilipwe na serikali kuu.

Kitu kingine ambacho pia ninge taka kifanyiwe mabadiliko ni land ownership. Uta ona kwamba serikali hii ambayo tume kuwa nayo, kama vile wenzangu ambavyo wame tangulia kusema, ni kwamba sisi wapwani tume jifunza mengi, kwa sabu hawa viongozi ambao wanaletwa hapa, ma PC, ma DC wame nyakua trust of land zetu, kwa sababu wana stress na huko juu, wana aenda wana chukua title deed, ana kuja ana kugafulisha anakuambia toka, na uta ona kwamba hasa wale ma PC, ma DC ukienda hapo kilifi wame nyakua mashamba makubwa kabisa, na mtu ali toka pengione ku Koibatek huko, ana kuja ana fukuza mwenyewe, kwa hivio..eh.mwenyeji wa hapa. Kwa hivyo tuna, ninge pendekeza kwamba, hizi title deeds ziwe tuna tolewa katika district level, na wale ambao watakuwa wame letwa hapa na Central Government kuja kufanya kazi, wawe tu wana kuja kufanya kazi, lakini sio kuingilia kunyakua mashamba ya watu.

Kitu kingine ni uwwezo wa rais. Rais wa Kenya ame vishwa taji nyingi ambzo wkati mwingi, hua ana tumia pia kuongoza vibaya taifa. Uta ona kwa vile ame pewa uwezo wa kuchagua wabunge wateul, na pia mawaziri, wakati mwingi aki wa chagua watu hawa hua basi ana wa ..ah..ni wamfuasi vile ambavyo anampenda yeye mwenyewe. Kwa hivyo sasa uta ona kwamba wakati mwingine, baada ya kuwa ana wakilisha wananchi, ana kuwa kama mungu mdogo. Kwa hivyo ninge penda kwamba uwezo wa rais, upunguzwe na hasa pia asiwe Mkuu wa vio vikuu. Hio apokonywe, wale ma Chancellors' wawe ndio watakua wana simamia hizo. Pia kuchagua wabunge wateule, hii pia asi fanye yeye bali ifanywe na bunge. Na pia si kwamba hawa wawe ni watu ambao anawa chagua yeye, bali watu wa…hawa wabunge wateule wawe watu hasa ambao wana wakilisha wananchi wa Kenya, hasa hawa ambao wana wakilisha viyama vya wafanyaji kazi, ambao pengine wame zidi laki moja. Watu kama hawa ndio wawe anaweza kuchaguliwa kuwakilsha kwa sababu, watu hawa wana mambo mengi mambayo wana wafanyia watu, na wana, pia wana jifunza mambo mengine. Pia watu kama wakuu wa makanisa, wao ndio wanaweza kupawa vitu kama hivi. Kwa sababu, ni watu ambao wana wakilisha watu, na wana jua matatizo ya watu, sio kwamba tu wana chaguliwa na rais wana enda wamfanyia mambo yake. Si wazile special interests, bali wana enda kuakilisha interest za rais.

Kwa hivyo tuna taka vitu kama hivi vya wabunge vya wateule, vipawe viongozi wa makanisa, kama makanisa watapata moja, hawa ambao wana wakilisha makundi ya wafanyaji kazi, ambao wame zidi kama laki moja pia wao wanaweza kupawa vitu hivi, ili waweze kuwakilisha huyu Mkenya ah.. kwa manufaa ya nchi kwa jumla.

Pia hii, kuna hii president accent. Hii nime ona kwamba ina tumika vibaya, kwa sababu wakati mwingine kina weza kuwa ni kitengele ambacho ni kutia sahihi yake, kina weza kuwa cha maana lakini kwa sababu ana jiona yeye yu bora anakataa, pengine hata ata kubali dakika za mwisho kwa sababu anaona kuna kitu fulani ambacho kina elekea kwamba yeye anaweza aende akose. Kwa hivyo, anaweka hio signature ili kujitakia kura na vitu kama hivyo dakika za mwisho. Kwa hivyo hii president accept kwamba ndio ina backshisha hizi bills isiondelewe na wabunge, waweze, kama ni kitu ame thibitisha, wote waweke sahihi na kiruhusiwe.

Pia majaji wasi chaguliwe na rais, majaji wakuu na majaji wasichaguliwe na rais, wachaguliwe na wabunge. Kwa hayo ninge penda ku fedhea hapo. Asanteni.

**Com. Lenaola** – Asante sana bwana Jembe, Sebastian Mwanyamau

**Mr. Sebastian Mwanyamau** - Kwa jina mimi naitwa Sebastian Mwanyamau. Nime pata notice kidogo tu juu ya kuja kwenyu. Kwa hivyo sikuwa enough kujitayarisha kwa kutosha. Nilipo fika pale katika registration, nika ambiwa mpka uji register ndipo uingie kule ndani. Kwa hivyo ika nibidi ni register. Lakini mimi nina mambo matatu tu nataka kusema.

Kitu cha kwanza, nilikuwa, maoni yangu napendekeza kuwe na Federal Government. Hii Federal Government ita angalia interest ya Majimbo yao. Iongozwe na president, na serikali iwe na Prime Minster. Ma askari polisi wawekwe na Majimbo, waandikishwe na Majimbo, wasi andikishwe na serikali kuu.

Kitu kinginie ambacho nili kuwa nataka kuzungumuza ni finance. Finance proceeds zote za jimbo ziwe zika chukuliwa seventy five percent kwa Jimbo na twenty five percent kwa Central Government.

Kitu kita kacho malizia mimi ni land. Nataka lands yote mamlaka makuu yapewe Majimbo. Yasiwe kwa serikali kuu. Hayo mimi nime ndiyo nilikuwa y akusema.

**Com. Lenaola** – Asanti. jiandikishe pale. Raymond Kazenga. Halafu, Daudi Kaigu, uta mfuata huyu.

**Mr. Raymond Kazenga** - Kwa majina mimi ni Raymond Kazenga, niki changia mjadala huu, niko na ma pendekezo matatu tu. Ahh….na kwanza, ninge penda kugusia sehemu ya president kuwa Commander in Chief. Mimi nina pendekeza kwamba, asiwe mkuu wa majeshi. Sababu ya kwanza ni kwamba Kenya tuko na makabila zaidi arubaini na mawili. Lakini leo hii ukiangalia katika Jeshi uta kuta…ama Armed Forces as a whole, uta kuta ni makabila machache sana ambao wana wakilishwa kwa wingi, na wale wengine ni wachache, kama kwamba hawana haki wao pia kulinda nchi yao. Pili, president akiwa Commander in Chief kwa mfano, mimi niko kwa chama cha upinzano, yeye ndio ana tawala. Niombe ruhusa ya mkutano, Na

pengine aone kuna hatari fulani ambao mimi naelezea wananchi wajue, Yeye ni rahisi kukatiza kwa sababu yeye ndio ako na nguvu, na ako na uwaezo..Hivyo basi ita mnyima ule muingine haki ya kuweza kuwaelezea wananchi ili wamuelewe ma lengo yake ni nini.

**Interjection-Com: Lenaola** - Unge penda nani awe Chief wa Majeshi?

**Mr. Mwanyamau –** Hivi basi nina pendekeza, huu adhifa upawwe kikundi maalum – executive. Hio ita kuwa ina angalia usalama wa nchi, ita kuwa ina angalia matatizo yoyote katika nje ya nchi ambayo yana kuja, ndio wata kuwa wana kaa waangalie halafu wapeleke bunge, bunge lipendekeze, kama ni vita vifanyike, vifanyike. Lakini asiwe president yeye akisema kwamba, shika, ashike; hapana.

Ya pili ninge penda kuongea habari za vijana. Mpaka sasa kuna wimbo wa vijana kwamba wa pawa uongozi. Lakini niki angalia katika Kenya, vijana hao wame sahaulika sana, hawatanguliki mpka leo. Hatu huyu kijana akiambia sasa shika uongozi, hajui aingie wapi na ata zindikiza wapi. Sababu ni kwamba hawaku husishwa na hawahusishwi katika maendeleo ya nchi. Na ule umri ya vijana ambao una tajua sasa nina uona kama uko na tako, na ninge pendekeza maoni yangu vijana waanzie na miaka kumi na minane mpka thalathini na mitano. Wakianzia thalathini na sita kuendelea mbele yeye ata kuwa ame kuwa mtu mzima. Kwa hivyo asihesabiwe kama kijana na pewa uongozi. Ahh,.. katika hii serikali ijayo basi, ninge pendekeza, kama inge wezekana kwa kila district, kuwe na watengewe kitu kimoja, vijana. Wawe wakilishi bungeni kila district, at least waweze kuangalia vijana wenzao, shida zao wa zinaweza kutatuliwa namna gani.

Ah, zingine ni kuhusu mashamba. Mashamba yame kuwa tatizo katika Kenya, na watu wana endelea ku ongezeka, mashamba hayatoshi, lakini tukiangalia, tutakuta wakubwa wako na meno makubwa sana ya mashamba. Ana weza kuwa ame anza hapa mpaka pengine vipingo, ama kilifi. Hilo ni shamba la mkubwa, na hali guswi na mtu. Ule mwananchi wa kawaida hana hata robo acre. Kwa hivyo tuna ona huo kama ni unyanyasaji. Ninge pendekeza kama inge wezekana, kuwe na kiwango mahali. Kila Mkenya, kila mwanadamu wa nchi ya Kenya, awe na kiwango kichwa awe mkubwa awe mdogo, at least isikose kama acre sita kila mutu. Yeye nawe aweze kujiendeleza maisha yake.

**Interjection - Com: Lethome –** Ume sema kiwango cha chini ni acre sita, na kiwango cha juu?

**Mr. Mwanyamau –** Acre sita, isizidi plot moja, acre kumi na mbili. Acre kumi na mbili.

**Com: Lethome –** Hio ndio plot moja?

**Mr. Mwanyamau –** Yah, hio plot moja. Ahh.. nne, ninge penda kugusia habari ya uchaguzai. Uchaguzi wa sasa ambao tuko nao tuna ona ya kwamba, tukianza uchaguzu tuna anza president, mps, diwani siku moja. Hivi basi naona kwamba, wengine

huwa wana pata kura zisizo kuwa za ukweli…..Asimame peke yake aombe kura kwa wananchi apawe uje hua mbunge, the same halafu uje wa president. Ahh, nafikiri kwa leo ni hayo tu asanteni.

**Com. Lenaola –** Jiandikishe opale, Asante sana. Sasa huyu ni bwana Daudi Kaigu.

**Mr. Daudi Kaigu Matela** - Mimi naitwa daudi matela.

**Com: Lenaola –** Daudi who?

**Mr. Matela –** Naitwa Dauidi Matela. Mimi nime kuja kwa hasa kwa habari ya tatizo ya kuwa tuna shida ya barabara nzuri kwamba hapa. Barabara ina matope. Na jambo lingine lahakika pili, kuna soko hatuna hapa. Jambo la tatu sisi hapa hospitali ya kuzalisha hatuna.

**Com. Lethome** - Ukisema tu uongeze ni kupendekeza Hakuna barabara, pendekeza, hakuna soko, pendekeza, hatuna hospitali pendekeza.

**Com. Lenaola** - Una taka nini, ulikuwa una taka nini?

**Mr. Matela –** Napendekeza barabara. Na lapili napendekeza habari ya hospitali hapa. Napendekeza tena jambo lingine la tatu hapa soko hatuna.

**Com: Lenaola** - Soko la nini?

**Mr. Matela –** Za matunda, maembe, hata ndizi, kila kitu, hakuna. Na jambo lingine tena, hatuna solo ya mbata. Mbata, hatuna. Mbata nataka ijengewe hapa,. Mbata ule mnazi. Kwa hivyo mimi, sita kwenda mbege mbege sana, nime komea hapo.

**Com. Lenaola –** Asante sana, – Hannington Karisa, ..Haya, kaeni karibu pale. Alphonse, Alex Mohamed Bashir, Alex Otieno, (inaudible)

**Mr. Hannington Karisa**. Haya habari zenu wageni? Kwa jina nina itwa Hararison karisa Mbaru. Katika mjadala huu ambao tuko hapa leo kuhusu katiba, number one, ninge gusia upande wa rais asiwe above the law. Awe yeye iwe ame kosea, awe ana weza kushtakiwa, kama mwananchi wa kawaida. Asije akawa yeye, basi atakavyo sema yeye, ndio hilo tu, na hata aki kosea, hakuna mtu anaye kumweza kumjaji kwa makosa yake.

Ya pili ninge pendekeza mufumo wa Majimbo. Mufumo wa Majimbo iwe kuna kila province ina jitawala wenyewe, ina angalia rasilimali zake zenyewe, na wawe wakiwa wana gawa, wagawe seventy five percent kama ilivyo kuwa na wenzangu waki tatua zije kwa Majimbo kwa province yake, halafu twenty five percent iwe ita pelekwa kwa Central Government. Sababu, tukiwa na Majimbo hapa, tuta kuwa na mkubwa wetu ambaye pia atakuwa ana wahusiana na mkubwa wa Central Government kule. Hio ni ya pili.

Ya tatu, upande wa security – upande wa security tuna ona ya kwamba, katika serikali hii tuko nayo sasa, ina maonezo mengi. Uta kuta ya kwamba, katika recruitment ya security, hasa niki angalia sana wakati upande wa pwani tume wachwa nyuma sana. Hata ikiwa mimi mwenye nime wahi kwenda recruitment karibu tano lakini uta kuta sijui hawa wajamaa hua wana tokezea nawapi watu wa bara, watu kuwa wale wanachukuliwa wengi zaidi, uta pata Mgiriama ni moja, au tu semem Mji kenda ni moja au wawili watatu, na majority wana toka huko.

**Com: Lenaola** - Una pendekeza nini?

**Mr. Karisa** - Kwa hivyo nina pendekeza ya kwamba, tukiwa na mfuo wa Majimbo, ita kuwa recruitment yetu tuna fanya sisi wenyewe, tuna chagua wale wanao weza na kutegemea na elimu zao, na miaka ina waruhusu, kuingia katika Jeshi au Polisi, Navy, Adminstration Police, hizi zote tuta kuwa tuna zipandga sisi wenyewe hapa, badala tuwe tuka chukue mtu mwingine kutoka nje, aje atukalie hapa na hajui mambo memngi ya hapa.

La nne, ugawaji wa pesa. Ugawaji wa pesa katika mfumo wa Majimbo, ni kma nilivyo sema mwanzo tayari kwamba ita kuwa pesa ina enda twenty five percent kwa Central Government, and seventy five percent ina baki na sisi wenyewe. Niki sema hivyo ni ya kwamba, kufafanu, hapa tuna rasilimali nyingi sana, lakini unaona Central Banks zote zina kuwa ni kule. Uki fanya kitu, porti iko hapa tunayo, lakini ukifatiliza sana mambo mengi, uta kuta pesa una ambia mpaka zitoke Nairobi, ndio centre, ndio pesa nyingi huko, ambavyo hivi sasa, sisi kuzipata na ku jiendeleza ina kuwa ni vigumu. Hio port ya kwanza, hapa Pwani tuna upande wa Fisheries. Fisheries pia ina tuletea mapato, lakini pesa yake hatuioni. Upande wa utalii, tume gandamizwa. Kwani tuna mahoteli mengi zaidi sana, na tulipo ona ajabu ya kwamba chuo cha utalii kina jengwa Nairobi, na Nairobi hoteli za kule si nyingi kushinda hapa. Hapa ndio mukowa wa Pwani na ndio iko ma hoteli mengi zaidi. Kwa hivyo, ninge pendekeza ya kwamba, tukiwa na serikali yetu hapa Pwani itakuwa mambao kama hayo, tuta yafanya sisi wenyewe na serikali yetu.

Sita, sita ni kama hio rasilimali, nilikuwa nime sha izungumuza tayari. Kuchaguliwa kwa mameya, mayor lazima achaguliwe na wananchi wenyewe, kwa sababu, ikiwa meya atakuwa ana chaguliwa na Local Government, wao huko ofisi ya Local Government kama manufaa, wao ndio ma staff, wao ndio wenye kuchagua meya, halafu mwananchi ataka kusikia oh Meya Mwasuma sijui nani ame chaguliwa, ita kuwa sasa hai pendekezi, kutegemea na wananchi, vile ata wakilisha. Lakini ikiwa wananchi wenyewe hapa Pwani, wata hushishwa jambo hilo kuenda kuchagua meya ita kuwa ni ubora zaidi. Na pia aangiliwe huyu meya nikwa kiwango cha eleimu gani.

**Com. Lethome –** Una pendekeza kiwango gani?

**Mr. Karisa –** Huyu napendekeza kiwango kiwe cha kuanzia form four, akimaliza vizuri mpaka university, awe anaweza kuchukuliwa kama meya. Maanake tunge husika mpaka class cha saba nane lakini unajua watu wana sema elimu yake ni ya chine, kama huyo ambaye tuna msikia tayari Mombasa, ame wekwa nje, kwa sababu ina onekana elimu yake ni ya chini. Kwa hivyo wa meya, nime pendekeza.

Upande wa viwanda, upande wa viwanda hapa Pwani tume kaliwa sana, ambapo kwamba ni kama ambao serikali hakuna. Na tunayo serikali. Serikali tuko nayo, tume pata uhuru tuna jua tunao uhuru kweli, lakini tukiangalia upande wa viwanda coast province iko nyuma sana. Na hii mfumo wa Majimbo ikiweko nafikiri viwanda vile ambavyo vime fungwa kutoka miaka na miaka, hata kutoka mimi sijafungua machjo, nafikiri zinge fufuliwa. Kwenda kama vya mkorosho vilie kuweka ika fungua. Haya, kukawa kuna Ramisi Sugar Factory, ime fungwa, kukawa kuna Bidco Factor hapa, ime fungwa. Haya viwanda vingine vingi aziendelei, kwa nini? Kwa wenzetu kule zina endelea. Miwanai Sugar Factory kule, kuna sijui nini factory, sijui kuna Mumias sijui nini, zina endelea havifugnui. Lakini hapa kwetu tukiangalia, tume kaliwa, mnazi yetu zimekuwa hazi tambuliwi..

**Com. Lenaola** – Pendekeza

**Mr. Karisa –** Napendekeza kwamba vitu kama hivyo hapa, tuwe zina funguliwa, na tuwe tuna fushishwa kazi tuwe tume pata kwa uraisi. Kama mbata hivi sasa wakati huu, kama ni upande wa serials hizi mbata ime kuwa mpaka dakika hii. Hatuna bei maalum ya mbata, uta sikia ni mbata ina nunuliwa shilling tano, pengine tisa, pengine kumi. Mti kama huu, inge kuwa sehemu ya bara nafikiri, sijui wange fanya nini, badala ya mkahawa. Tume tegemea sana mnazi hapa, na umnazi tuki ifanyia utafiti manzi wetu una faida ishirinina nne, kwa mti moja wa mnazi. Lakini kwa sababu, hakuna viwanda, hapa hatuwezi kuona manufaa hio, tume kaliwa kabisa.

Upande wa elimu, ah, upamnde wa elimu, pia tume kuwa nyuma kama yamesemekana, kwa sababu pesa za kupelekea watoto wetu ku endelea na masomo ime kuwa ni haba. Na hii yote inaletwa na ukosefu wa pesa, kwa sababu hatuna rasilimani ambazo serikali ina zaitambua tupate pesa, tusukume watoto wetu, wasichana na kwa vilana waende mbele. Kwa hivyo hapo hivi kuna jambo moja lipo guswa wasome kutoka standard one mpaka four, at least wawachiwe three, kule kuingine ndio wana weza kuchajiwa. Lakini, hii elimu ndio kidogo huku ime tugandamiza. University kutoka 1963, tukipata uhuru, eh.. kutoka muanzilishi, mpaka juzi ndio tuna sikia hii Bandari College ina fanywa university, ambao nii.. Inge kuwe at least, hatakakama hatuna elimu, lakini pia tukiwa na university school hapa, hata mtu kutoka Rwanda, Sudan, nchi za nje wakiija, wakileta ile pesa, ndio maendeleo hapa pwani na sisi pia tuna pata usaidizi.

Ahhm Kama muongozo wa akina mama ulikuwa una zungumuzwa, pia hata mimi ninge pendekeza akina mama apewe mistari

wa mbele, hata kuchaguliwa kama president pia hio pia wana vutishwa, wasi wekwe nyuma. Wao ni kama wanaume wengine. Kwa hivyo wananawake tuna wapa mustari wa mbele kuanzia hii serikali mpya inayo kuja, wanawake wahusishwe sana. Hata kama kusimamie upresident pia, asimame.

Uhhm ..Uskota ndio ume turudisha nyuma pia. Na mengi yame tajwa, tajwa lakini sasa uskota hapa kwetu kwa kusema kweli yame zungumuzwa, mtu anatoka Nairobi ana kuja na title deed, hatujui hii shamba huyu mtu amejua kutoka wapi. Tuna shindwa. Una kuja kufukuzwa una wewe ni skota na wewe una miaka thalathini minne, babu yako ame zikwa pale, nyanya ako amezikwa, pale nani na nai wame zikwa pale, leo kuna kuja mtu anaitwa kinyanjui, anakuja na karatasi kwa meza ana pewe sasa visa kwa DC, pale na DO, anasema hii shamba mahali fulani, baruwa lipo pale sikwake ni kwangu. Huo uskota unataka uondoke, tukisha pata ufumo wa Majimbo. Huo uskota ndio imetuwacha sisi pia tuna umia sana.

Mahospoitali, kusema kweli, hatuna. Ilivyo sungumuzwa hapa, mtu anakufa hapa pengine ame jitia kamba. For example, kuna ile Sea side, mtu ana elekeza kujiuwa mwenyewe. Akisha jiuwa mwenyewe, tuna pata shida sana hapa. Tuna report kwa Sub Chief, Sob Chief, kwa Chief, ana kuja yule ana bebwa ana pelekwa Kilifi either Mombasa. Sasa serikali akisha chukua yule mtu, haya kurudisha ni juu yetu, ambao ni garama. Kwa hivyo kama tunge kuwa hapa mfumo wetu wa Majimbo una weza kutuletea mambo ya hosiptali na ma mortuary, yakuwa jambo kama hayo ikifanyika tuna zitatua, kama zile ambazo dakika hii tuna tayarisha kuwa na ofisi ya D.O, tuko nayo, halafu itakuwa karibuni ina ehh…sijui waitaje ile wanao tazamia kuiendeleza. Hospitali ziwe hapa, polisi ziwe hapa na kila kitu. Ita kuwa ni vizuiri.

Sasa kumalizia, ni kwamba ni ingilie upande wa cerials. Cerials zime tajwa hapa. Cerials kwa kweli hapa Pwani ziko nyingi sana. Na hizi kama zinge kuwa zina funguliwa viwanda, at least huu umasikini kwa Pwani ingeli kuwa hakuna. Cereals zenyewe niki zitaja kama michele, kunde, mbaazi, pojo, maharagwe, eh. Michele, hizi zikiwa ziko, hua tuna weza kupata viwanda ambavyo, vitu kama hivyo vina hifadhiwa. Na kuhifadhiwa hizi vitu tuwe navyo ni mpango wa maji. Maji pia wame tugandamishwa sana. Irrigation ina semekana. Lakini sana hatuwezi kufanya irrigation maanake ahh.. mifereji yetu haija kufishwa kuwa na pipes za kupeleka mpaka mashambani. Na hii yote ina letwa serikali ambo tukanayo hivi sana. Lakini tukiwa na mfumo wa Majimbo, nafikiri mambo kama hayo tutakuwa tuna weza kutatuliwa, na tuna weza kutengeneza maanake pesa tuta kuwa tuna ziweka wenyewe, kule kuna enda pesa kidogo, nyingi tuna baki nazo, kwa hivyo tuna weza kuji… kujiendeleza. Sina mengi zaidi, haya asante.

**Com: Lenaola** - Haya asante sana. Kujiandikisha ni pale. (inaudible)…Samson Viagu, Basi akina mama, mkiwa tayari, tutawapa nafasi pia mtoe maoni, baada ya hawa wawili, kwa hivyo msi toroke. Haya endelea.

**Mr. Washington Bwaga –** Mimi kwa jina naitwa Washington Bwaga, na nataka kutoa, kuongeza mawazo zaidi kutoa maoni yangu niki anzia na elimu. Kama wenzangu walivyo, sema kuwa elimu iwe ya bure mpaka standard four, mimi sipendelei standard four, maoni yangu elimu ya bure iende mpaka form four, kidato cha nne.

**Interjection Com. Lethome –** (Inaudible)

**Com. Lenaola**- Endelea.

**Mr. Bwaga –** Na kwa upande wa maji, katika sehemu za wenzetu una ona maji yatolwewa bure, lakini Kenya, mahali popote maji yana uzwa, na maji ni naturual resources ambao ina patikana. Kwa hivyo serikali yetu inge fanya bidii ili wananchi wapate maji ya kutosha tena yasiuzwe, yawe ya bure. Kwa hivyo, nafikiri elimu, maji na mambo mengine ya barabara. Barabara zetue ni chafu sana. Ukiangalia barabara hii kutoka Kaloleni mpaka Makweni, tokea tuanze pate uhuru mwaka sitini na tatu, mpaka sasa, haija tiliwa lamu. Kwa hivyo, na pendekeza kuwa, serikali yetu ya Majimbo iangalie juu ya barabara zote ambazo zina pita mashambani, ili wakulima waweze kupeleka mali yao kwa ile mji ama seheumu ya soko ambavyo, ambapo mali ile ina takikana.

**Com: Lenaola –** Una penda serikali ya Majimbo, huja sema hivyo.

**Mr. Bwaga –** Napenda serikali ya Majimbo. Maana serikali hii kuu ime tunyanyasa hapa sana hata sisi watu wa pwani. Niki rudia upande wa Urashi, urashi, ninge taka urashi kusema kweli, watoto, tuna watototowakike na wa kiume. Na katika mji kenda, mtoto wa kike huwa harishishwi, huuwa anae rishishwa ni mtoto wakiume. Maana yule mtoto wakike ata olewa na kule anako kwenda hua ame tengeneza mji wake, na ile mali ambayo ata ipata pale ya bwana yake hua, ndiye mali yake. Na yeye hua ndie custodian, yani mchungaji wa ile mali yani waki ingia watoto wake watakao rishi. Kwa hivyo, tukisema kuwa mtoto wa kike awe ata pata gawanyiwa tena kule anapo toka apate sehemu, basi, itakuwa tuna nyanyasa ule mto wa kiume, ambaye hana mahali pa kwenda, isipokuwa yeye ata leta mwengine ambaye ata kuja mtunza pale. Kwa hivyo maoni yange ni kuwa, ikiwa yule ata pata, isiwe kubwa ama sawa, sawa na yule mtoto wa kike. Mtoto wa kike apate sedusi moja na yule wa kiume apatesedusi mbilii.

Na uchumi. Katika Pwani, ni Jimbo ambalo kusema kweli mali yote ambao ina enda bara inatoka hapa. Lakini uta ona kuwa vitu vyiote vina ingia hapa bandarini, vina pelekwa huko juu, ambako ni headquarters, halafu zina letwa hapa, na zikija hapa zina, tuna uziwa kwa bei ya juu. Kwa hivyo tunge pendelea, vitu vikiingia hapa ziwe tunauziwa kwa bei ile na watu wa bara. Ziki pelekwa huko nawauziwe kwa bei yao, ile transportation, iwe ikiwa ita ongezwa iongezwe kwa sababu ya bei ya huko, lakini sisi tuna ongezewa hali, sisi zime pakuliwa hapa na tuna nunua bei ya juu kuliko watu wa bara. Halafu hapa tuna mali ya asili. Hizi mali za asili zote, tuna taka ziwe za Majimbo. Hata kama kume funguliwa mafuta, mafuta yawe ya Majimbo. Kuna ule titanium ambayo uko kwa wingi sana hapa pwani, karibu kila mahali kuna titanium. Kwa hivyo hio iwe mali ya Majimbo.

Nyumba za serikali – kulikuwa na mtindo wa kujinyakushisha nyumba za serikali, mpaka nyumba zote zime chukuliwa. Tukipata utawala wetu ma Majimbo, hizi nyumba zote zita regeshwa, maana tuta kuwa na watu wa serikali, na tuta wapa

nyumba. Kwa hivyo wale ambao wamenyakua hizi nyumba, basi, tuta taka ziwe za serikali, zirudi ziwe za serikali. Na kila mali ambayo ime chukuliwa ya kibinafsi, iregeshwe kwa wananchi, yani kwa serikali.

Mahakama – Tumeona mahakama kweli hazitoshi, ndio sababu kuna nishwa wazee wa magogo. Na hawa wazee wa magogo hawajui sheria yoyote, isipokuwa wanajua zile sheria za kienyeji. Na wana ukumu kwa kutumia akili zao, lakini hii si tabu. Tunge taka hii koti hii ya magogo iendelezwe kidogo. Wale ambao wana hukumu pale, wana hukumu zile civil cases, ambazo ni za mali, za kupokoshana na… za mashamba, na kesi nyigine hizi ndogo, ndogo. Na wana fanya kazi muhimu. Lakini shida ni kuwa hawana elimu, maana kesi zile aziandikwi, na pia wana tosha pesa nyingi sana. Wana mtosha yule msitakiwa, na mshitaki. Na halafu yule ametolewa haki haregeshewe, yani yule alie shindwa haregeshi pesa kwa mwenziwe. Kwa hivyo ni kama wana wadhilumu wananchi. Kunge kuwa na mtindo maalum na hawa watu wawe wame elimishwa, wajue jinzi ya kukata kesi na refund, yani kuregesha pesa kuta regeshwa namna gani.

**Interjection – Com Lenaola** – Dakika mbili ndio ime baki.

**Mr. Bwaga** - Ninge taka kueleza juu ya mtihani, ya lugha kwa wabunge na wa ma concillors. Mtihani ya lugha ni muhimu sana. Mtu asipo shinda mtihani huu, sijui atakuja sema lugha gani kule na wenzake. Na mtihani nili ona ili kuwa ni rahisi, na wengi wanao kwenda kule hua hawakupita vizuri. Hawawezi kuongea. Ukiangalia ni shida sana mbunge kuongea Kiswahili na hali ali pita mtihani. Ama kuongea kiingereza, na hali ali pita mtihani. Kwa hivyo tunge taka,mtihani, yule ambaye ata kwenda bunge, kiwango chako cha elimu kiwe kina mwezesha kuongea kiingereza na kuongea Kiswahili vizuri.

**Interjection – Com. Lenaola** - Hebu pendekeza hiki kiwango.

**Mr. Bwaga –** Kiwango ni form four kuendelea mbele, mpaka degree level.

**Com. Asiyo** - Kwa hivyo Kiswahili kisomeshwe?

**Mr. Bwaga –** kisomeswe mashule. Kiswahili kisomeshwe na iwe lugha ya taifa, na kiingereza pia. Zote mbili ziwe lugha ya taifa. Ili ziweze kuongewa bunge na mahali popote nchini.

**Com. Lenaola** – (Inaudible)

**Mr. Bwaga –** Nili kuwa nataka nieleze jambo moja.

**Com. Lenaola** – Tuta angalia memorandum.

**Mr. Bwaga** – Basi nafikiri ni kama hivyo.

**Com. Lenaola** – Asante sana – Okay. Haya Bwana Viagu

**Samson Viagu** – Habari Zenu. Kwa jina mimi na itwa Samson Viagu. Na mimi nime kuwa chairman wa kikao cha location ya Chasimba Chwonyi, katika mradi huu.

Kitu ambacho ninge taka ku zungumza, mengine yame shazungumuzwa lakini nita kuwa naya rudia kidogo, kidogo tu kwenda mbele. Kanuni za kuongoza fedha za dola. Nafikiri hapa tuseme hii katiba yetu iweze kuhushisha kutambua usawa na heshima za kila mtu bila kujali rangi kabila, dini jinzi au chewo cha mtu, kuona kwamba watu wote ni sawa mbele ya sheria. Kila mtu awe chini ya sheria ya nchi. Wa Kenya wana madini muhumu, yanao paswa kuwekwa kwenye katiba. Ikiwa ni mila, desturi na utamaduni. Madini haya, yaweze kutekelezwa kisheria na kuwe na uhuru.

Ukuu wa katiba – Nina sema katiba iwe ndio ambayo ita kuwa juu ya kila mtu, kwa sababu hii ndio sheria kuu kabisa katika nchi. Na bunge lisiwe litaweza kuruhusiwa kubadili, kubadilisha hata section yeyote katika bunge bila kuhusisha wananchi. Kwa hivyo, tuna taka kama kukiwa tutakuwa na mageuzo yoyotoe katika katiba, wawe wananchi wata husishwa kupitia kwa maoni ya rahia.

Urahia - tuingilie habari ya urahia. Urahia ni kitu muhimu kwa kila nchi. Kwa hivyo tuna taka wale watu ambao wata kuwa rahia, kwanza wale ambao ni wazaliwa wa hapa, wenyeji ambao wame zaliwa hapa. Pili kuna wale ambao wame bahatika wame kwenda nje, wame kwenda ng'ambo na pengine wame pata mabibi kutoka kule. Wakija hapa, huyo mwana mume huwa ni automatic citizen, kwa sababu yeye ni mzaliwa wa hapa na ni mwenyeji wa hapa. Yule mwananmke tunge taka awe pia ata ingizwa kama rahia, kwa sababu ni bibi ya rahia wa hapa. Isipokuwa sasa, tukiwa tuna bibi, mwanamke wa hapa ambaye ni rahia wa hapa, halafu kuna kuja kama mjerumani aje awe amuowe, huyo mjerumani tunge taka apigwe tochi, ndio apewe urahia wa Kenya. Kwa sabu hatujui, pengine ana fanya vile kwa sababu zake. Pengine ana owa ili kusudi, awe ata weza kupata ngazi ya kupata urahia wa Kenya. Kuna wengine hapa Kenya hata hivi sasa ni rahia wa nchi mbili. Una sikia mtu ni yuko rahia wa Kenya na pending ni rahia wa Ungereza au ni rahia wa Urabuni au wa India. Tunge pendelea ya kwamba, urahia wa Kenya uwe moja, tu siwe na double citizenship, apokonywe ile moja na apokonywe hii yetu. Tunge taka katiba pia iweze ku rahishisha hati za kutenbelea. Kwa sababu, hivi sasa mtu akitaka kupata passport, it is a nightmare. Kwa hivyo tuna taka wakati ule, mtoto anafika miaka kumi na minane na ana taka kupata kitambulisho cha Kenya, pia aweze kupata kitambulisho cha kusafiria. Vyote viwili vitolewe, mara…kwa wakati moja.

Ulinzi na usalama wa taifa – vyombo vya usalama majeshi na ma matawi yake, yaundwe na katiba. Kuwe na Commission ya kuajiri na kunidhamisha majeshi ya usalama. Kwa hio majeshi yawe ata andikwa na Commission, na yawe taratibu zake zita tunzwa na Commission. Discipline iwe chini ya Commission.

**Interjection - Com Lenaola** - (inaudible) – Eleza tu zile za muhimu, nina one ni mrefu sana.(inaudible)

**Viagu** – Okay, kwa hivyo ninyi mta soma hapa. Viama vya kisiasa. Ahm.. vyama vipewe uhuru vya kutekeleza maendeleo ya uma, kama Manifesto yao ilivyo na serikali ilioko. Yani tuna taka vile vyama vya ki siasa, ziwe zita, zita kuwako na pia viwe vita pewa pesa na serikali, ili ziweze kudumisha udemocratia. Mjumbe asiwe ata fungwa tu na chama, kama vile tunavyo ona huko Cherangani, na upande wa Bomet. Awe mjumbe ana nafasi ya kuzungumza mambo ambayo ame pawa na wananchi. Lakini sio kwamba awe ata zungumza mambo ya chama. Chama kisiwe juu kushinda wnanchi.

Miundo ya aina za serikali – Serikali ambao tuna taka hapa ni ya Majimbo na pia VDCs, Village Devbelopmemt Committees, ziwe pia zita pewa uwezo katika sera hizi za serikali. kwa sababu tunajua VDC ndio iko katika grassroots.

Bunge, hili bunge tuna taka liweze kupiga mpaka kwa wale wote ambao wana chaguliwa na rais, mawaziri na ma Commissioners, iwe wakisha chaguliwa warudi wapelekwe bunge ili wa weze kutazamwa na hawa wajumbe. Hayo nafikiri imesha semwa na jamaa wengine. Kuwe na kamati pia katika bunge, ambayo ita hakikisha kwamba kila mswada ambao ambao ume pitishwa una tekelezwa. Kwa mfano hivi sasa, hapa tuna mswada huu wa mnazi ambao uli pitishwa bunge, lakini hata sasa hauja tiwa sahihi, na hakuna mtu ambaye ana weza ku point his thing. Kwa hivyo tuna taka kuwe na kamati ambaye ita simamia mambo kama haya.

Bunge liwe juu katika hizi ngazi tatu. Parliament iwe ita kuwa juu, ya executive na judiciary. Parliament iweze ku msummon rais kwa mambo ambayo pengine ana yakosea. Awe ana weza kuzungumza na wabunge taratibu zake ambazo ana zitumia kwa kuendesa nchi. Na katika kuchagua rais, mimi au tume onelea ya kwamba umri huu wa miaka kumi na minane, ni mdogo sana. Wale ambao wata pigia kura rais, inge kuwa kama wawe na miaka ishirini na mitano kuendelea mbele, kwa sababu mtoto wa miaka kumi na minane, hasa kwa wakati huu ambao watoto sasa wana pata vyakula vizuri hua akili yake bado ku kuwa tayari kwa kuweza kuchagua mtu kama huyu, kwa kulingana na taratibu. Na rais, umri wake awe ata kuwa miaka arubaini na mitano, ikiwa ana taka kugombe kiti hiki cha urais.

**Interjection – Com. Lethome.** - Hadi miaka mingapi?

**Mr. Viagu** – Mpaka miaka sitini, kwa sababu akiongeza sabini huko ata kuwa akili yake ina anza ku, ku deteriorate. Tena, rais pia awe ana taratibu nzuri. Mishahara wa wabunge, iwe iki chunguzwa na Commission. Wanawake pia wapendao kuingia bunge, wapiganie viti kama vile wanaume, on merit basis. Viongozi pia waweze kuwa ondoa hawa rais au wa bunge waweze kuwaondowa wakiwa hawafanyi kazi nzuri. Sisi tue pemdekeza ya kwamba ikiwa tuna taka ku muondoa mbunge tuwe tuna malalamishi ya watu kama eluf moja. Na kama tuna taka kumuondoa diwani , tuwe na kama malalamishi ya watu mia moja.

**Com Lenaola** – Saa zako zime pita.

**Mr. Viagu –** Zangu zime pita,

**Com: Lenaola -** Dakika tano ikiwa una memorandum, na kumi kama hauna.

**Mr. Viagu -** Kwa hivyo sasa nita kuachia hii memorandum. Okay.

**Com. Lenaola –** Asante sana bwana Viagu.

**Mr. Viagu –** Lakini nili nataka hii ya mahakama, kwanza kidogo tu.

**Com. Lenaola -** haya endelea.

**Mr. Viagu –** Hii ya makahama, tulikuwa tuna, tuna, tuna sema ya kwamba, kuwe na koti ndogo, ndogo, kama zile za Sheriff kule nje, ambazo ni kama koti za mtaa. Yah, ziwe zita kuwako, maanake zita punguza kabisa matatizo ya watu.

**Com: Asiyo –** Sio zile za magogo?

**Mr. Viagu** - A, ah – sio zile za magogo. Unajua zamani tulikuwa na na, na, courts ambazo zili kuwa zina muelekeo…

**Interjection Com Lenaola** - Tribal Courts.

**Mr. Viagu –** Yes, kama zile African courts. Zile zita saidia kupunguza congestion ya kule kotini.

**Com: Lenaola –** Asante sana bwana chairman. Tuna shukuru.

**Mr. Viagu** – Okay, asante.

**Com. Asiyo –** Lakini hio karatasi yako, afadhali upeane, hasa si mali yakio tena.

Samson – Zita wekwa kwa computer?

**Commissioners**, (all talking at the same time – inaudible)

**Mr. Viagau** – Okay, kwa sababu tulikuwa tuna fikiria tuna weza kwenda kuitengeneza visuri kwa sababu…

**Com: Asiyo –** Tuta ichukua hivyo hivyo, tuta ichukua tu.

**Mr. Viagu** - Hivyo hivyo tu?

**Com: Asiyo –** Ehe hivyo tu.

**Mr. Viagu –** Okay asante.

**Com. Lenaola** - Haya, bwana Viagu …Basi tuwaita akina mama, mnataka kuzungumuza, moja wenu, hata moja?

**Com. Asiyo –** Wata tafsiriwa.

**Com: Lenaola –** Ni sawa (inaudible) haya bwana Kai endelea.

**Mr. Andrew Kai** - Jina langu naitwa Andrwe Kai.

**Com. Asiyo** - Una itwa Mr.?

**Mr. Kai –** Andrew Kai.

**Com. Asiyo** - Andrew.

**Com: Lenaola –** Endelea bwana Kai.

**Mr. Kai**. Mimi nina memorandum yangu hapa nime andika kwa hivyo mimi hata sita guza (inaudible)

**Com. Lenaola –** Basi nina kupatia dakika zako tano (inaudible)

**Mr. Kai –** Haya. Kwaza nita anza na Katiba. Katiba ya sasa ime tunyanyasa sana,sisi watu wa Pwani. Ime tufanya sisi ni ngazi ya watu wengine kuvuka. Zisi zetu zina chukuliwa na hatupati chochote.

**Com: Asiyo –**Pendekeza

**Mr. Kai. -** Kwa hivyo tuna taka hii Katiba ambayo tuna taka saa iwe ita tuokoa. Na kutuokowa kwake, ni kuleta katiba nyingine ya ki Majimbo. Hilo tu ndilo jambo ambalo lina weza kutuokoa. Majimbo yata kuwa na uwezo wa kuchukua na kukusanya pesa ya mapato yote ambayo yakipelekwa serikali kuu. Na sisi tutawa chukua asilli mia sabini na tano na ishirini na tano tutawa pelekea wale wa serikali kuu, kwenda ku tumika malengo fulani, ambao ni ya kiserikali. Tume ona ya kwamba, hio ndio njia tu ambayo sisi ita tusaidia. Manaake hakuna maendeleo yoyote ambayo yana weza kufanyika hapa Pwani ama mukow mengine kama ile ambayo ime sahauliwa huko juu kabisa. Vile sisi wenyewe tugeuza muenendo wa kupata mapato. Tuna taka mapato yetu tu yakusanye, tuweke hapa na tu yaangalie tuta fanya nini sisi wenyewe. Sio mtu mwingine, kutufikiria hatufanyie nini. Kwa hivyo basi yale Majimbo yakija sisi tuna jua kwa tuta faidika na mambo mengi. Kama vile mashule, kama vile ma hospitali, na barabara, na mambo mengineyo.

Hii Katib, kuna kiwango au neno fulani ambalo lime tumiwa hapa sehemu, tangu lini. Hili neno nafikiri ni geni, ama wakigeni, lakini ikiwa ni geni katika katiba, basi hilo lina taka liwekwe. Na kuwekwa wakwe, kule kuli weka katika hapo, sio mtu kama mimi, a layman like myself. Ile ina taka watu wenye ujuzi ambao wanaweza kuliandika ki bara bara, ili liwe pale. Kwa hivyo ninge pendekeza kwamba, zile sasa ile ni jukwumu ya Kamishonas kwenda kuifanya kazi hili.

**Interjection - Com. Lethome –** Hapa; ni jukumu ya Commission lakini wewe ni jukwumu yako kupendekeza katika hio preamble una taka kuwe na nini ndani yake. (inaudible) huu utangulizi wa katiba. Una taka huu utangulizi (inaudible)

**Mr. Kai –** Nataka ile katibe ambayo ita linda mwananchi bila mapendeleo yoyote. Tuwe na usawa katika uendeshaji wa serikali. Sio wengine kutufanya sisi wanyonge na wale matajiri. Ha ha. Tuna taka usawa; katiba iangalie kila mwananchi maslaha yake, sawa sawa. Na hio nafikiri ni kwa ufupi tuna…yale mengine mtaongeza wenyewe.

Jambo nyingine ni uchumi. Uchumi wetu ume zorota hapa kwa sababu, wale ambao wame pewa jukwumu la kutu saidia sisi, wao ni watu ambao wana kuja hapa kujisaidia wao wenyewe. Tuna pewa watu kama ma DC, kama ma DO, wale wote sijaona mimi DC wa kikwetu. Na hapa wakija wao, kitu cha kwanza wana kimbilia nini, beach plot.

**Com Lethome –** Sasa una pemdekeza nini kwao?

**Mr. Kai –** Sasa watu kama wale sisi hatuwataki. Wakati tunapo pata Majimbo tuta wambias wakati wenu. Tuachiwe ni wenyewe na sisi tuvune. Yuki enda katika…

**Com Lethome –** Machifu mta ondoa ama ..?

**Mr. Kai –** Machifu tukipata Majimbo tuta angalia ufumo wake.

**Com: Lethome –** (inaudible) pendekeza sasa.

**Com. Asiyo –** (inaudible)

**Mr. Kai –** Wale machifu, wata bidi wachaguliwe na wenyeji. Hatutaki mtu mwengine, maanake wakiwa wao wana andikwa na mtu mwingine, basi yule wao wana kuwa sasa, sisi hawa tujali maanake wanajua mtu mwingine wana walipa na yeye ndie bosi huku. Hawata weza kututumikia sawa, sawa. Lakini ikiwa tume wachaugua, basi wao wata jua kwamba sisi ndio bosi wao.

Nina rudia kwenye uchumi. Uchumi wajimbo hauta endelea nchi ikiwa uta baki mikononi mwa wageni.

**Com. Lethome –** Kuna pendekezo….

**Mr. Kai –** Nina pendekeza kwamba kwanza, ukusanyaji wote ikiwa unakusanywa usanywe na watu wa hapa. Manaake ikiwa ule usanyaji una fanywa na watu wa nje, basi wale, ile njia ya kupora iko hapo katikati.

**Com. Asiyo –** Ukusanyaji ya nini?

**Mr. Kai –** Ukusanyaji wa mapato – Revenue.

**Com. Asiyo –** Na una sema uchumi isiwe, isiwe kwa mikono ya watu wa…

**Mr. Kai –** Uchumi ni economy. Uchumi tuna taka, watu wetu hawawezi kuendelea kama hawapati kazi. Maanake wakiwa wana kazi, ile mshahara wanao pata, ndio pesa zina circulate. Na ikiwa zina circulate, sasa ndio sisi tuta kuwa tuna pata pesa za kufanya ile miradi yetu. Kwa hivyo, tuna taka zine ngazi ambazo watu wana fanya kazi kama Kilindini, mahoteli….

**Mr. Kai** -…. kwa mia. Na wale wengine ni wale ndugu zetu ambao siku zote wamekuwa wakitu nyanyasa. Yume ona kwamba sisi tume tabika siku nyingi kwa sababu nafasi kilindini kiki tokea ama ofisini, watu wana jazwa malory huko wana kuja huku. Kwa hivyo huo mtindo huo hatutaki. Niki enda kwa raisi. Raisi yule alieko sasa ana tumia uwezo wake mara nyingine vibaya. Manaake yeye anaweza kusema hivi kesho minister ana sema hivi. Sasa hatujui minister ni mkweli au yeye ndie mkweli. Wananchi wana tatizika. Kwa hivyo yeye sasa in bidi apunguziwe yale madaraka ile abaki na ule mfupa na wengine wawe na moja. Na kufanya hivyo ni kwamba basikuwe na prime minister. Yeye ata kuwa anaendesha serikali kama zile serikali zingine zenye kidemokrasia. Yule president ana tuma mbakishisia tu kazi moja. Yeye ni mpokeaji kama wageni, ceremonious, ama kwenda kufungua bunge wakati waki kao fulani, kikao zile ambacho yeye anafungua wa rais wa sasa. Yeye asiwe ana madaraka makubwa, ya kuwa hata mtu hawezi kumsongelea. Hivi sasa wewe kwenda state house, haiwezekane. Kwa hivyo tuna taka mtu ambaye anaweza accessible, kama prime minister. Una weza kumuona. Lakini yule sasa kwenda

state house, wewe huwwezi kumuona, na kwa hivyo yule nguvu zake tuna taka kidogo zi punguzwe, na kuipunguzwa kwake ni kumfanyia tu, tumwambia kazi ni mbili tu. Ceremonial na kufungua bunge. Lakini ata kuwa akishauriana na yule prime minster kwa uongozi. Pengine ni kwa sababu yule ni mzee ana weza huyu prime minster akakosea jambo fulani. Kwa hivyo yeye lazima aende kule aka pate ushauri fulani. Yeye akiwa ana taka kufanya jambo lazima amshauri prime minister, na prime minister hawezi kupitisha lolote bila kwanza kwenda ku julisha rahia.

**Interjection – Com. Lenaola –** Saa yako ime isha.

**Mr. Kai –** Time yangu ime kwisha.

**Com: Lenaola –** Asante Sana bwana Kai kwa hayo maoni yako. Munyasi Mwatata

**Munyasi Mwatata** - (in vernacular-translated in kiswahili)

**(Translator)** - Jina lake anaitwa Munyasi Mwatata. Ata zungumza mambo ya hosipitali. Watoto wao wana teseka. Bei za nazi kwao haziwatoshi. Pia makuti bei yake ni kidogo. Ana taka wapate msada ya elimu ya watoto wao.

**Com: Lenaola** - Wanataka elimu ya bure ama …?

**Mwatata** - (**Translation**)- Wanapendekeza elimu ya bure.

**Com: Lethome –** Kuanzia kiwango gani hadi yipi?

**Mwatata –** Ana sema kuanzia class ya nane kuendelea mbele, huku mwanzo, huku mwanzo ana fanya mwenyewe.

**Com. Asiyo –** Hii mabo ya kia afya …

**Mwatata Translator) –** Ana taka hospitali iwe karibu.

**Com. Lethome –** Mama, una jua mwanamke akiolewa asi ariithi kwa baba, ariithi kwa mume peke yake. Unge sema nini kuhusu uriithi wa mwanamke?

**Mwatata –** Ana take wanawake awe wariithi kote, kote, kwa bwana na kwa wazazi.

**Com. Lethome** - Ange sema nini kuhusu mila ya ufwa.

**Mwatata –** Hawapendelei mambo ya kuingiliwa huku.

**Com. Lethome –** Wange taka mwanamke aki fiwa na mumewe aishi vipi baada ya mzee wake asha kufa mwanamke aishi vipi?

**Mwatata –** Ana taka afunuliwe na mtu yeyote mapato yake, awe ata kuwa juu yake.

**Com. Lethome**- Ana sema nini kuhusu mila ya kuhalwa?

**Tanslator –** Kuolewa?.

**Com. Lenaola –** Kuhalwa; sio kuolewa, kuhalwa.

**Com. Asiyo –** Kuolewa bwana akifariki.

**Com. Lethome –** Kuhalwa ana chukuliwa.

**Translator –** Ndio kuolewa basi.

**Mwatata -** Ana penda mtoto wake akiolewa apewe mahari.

**Com. Lethome –** Baada ya mahari yakitolewa, halafu mwanamke aje, pengine ame tengana na mzee mahari hua ita fanywe nini?

**Mwatata –** Ule mahari ilio tolewa iregeshwe kwa yule bwana, halafu mzazi, mzazi achukue mtoto wake aregeshe kwao.

**Com. Lethome** - Mzazi yupi sasa?

**Translator -** Yule alie toa mahari wakati kama yule mtoto anaolewa ndiye ata rudishiwa ile mahari halafu mtoto arudi kwa wazazi wake kule aliko zaliwa.

**Com. Asiyo –** Kwa mzazi mama?

**Translator –** Eh mzazi mama.

**Com Asiyo** - Kwa nini baba hashughuliki?

**Com. Asiyo –** Kwa nini baba asi chukui hii mahari?

**Translator –** Anyway, they are talking – wana zungumza kama family unit.

**Com. Lethome** - Ni musichana ame pata mimba bila kuolewa kwa kijana mwenye mimba. Unge penda huo mzigo aongezwe nani jukumu la kuangalia huo mtoto na kumshughulikia. Kama yule kijana yule kijana ameharibia yule musichana maisha yake, achukuliwe hatua gani?

**Mwatata –** Ana sema yule ambaye ana takikana kuchukuliwa hatua ni yule aliharibu yule kwa alazimishwe amuowe.

**Com. Asiyo** - Lakini kuna desturi ya hawa wengine ni kudunga mimba na kuenda tu. Hawa wezi kuowa hawa wasichana wote, ata fanyiwa nini?

**Mwatata** - Kukiwa na makosa kama hayo, kuna huyu ambaye ni maniac, ana penda sana wanawake awe akifanya zaidi ata chukuliwa hatua mbele ya sheria. Kwa jumla ana sema sheria ita pata kuondoa hio. Ni hayo tu.

**Com. Lenaola –** Haya, Buche Mbwana.

**Buche Mbwana** (in vernacular – translated in Kiswahili) – Buche Mbwana. Ana taka serikali ya Majimbo. Ana ishi kishida shida tangu azaliwe. Binadamu akiolewewa lazima awe na bwana. Bwana wako akikufa njiani bado uko na watoto, ambao bado waendelea kusoma, na yeye mama hajui hata moja kuandika, anaomba tu Mungu amsaidie. Mtoto aliye fundishwa wakati baba alipo kuwa hai, alikuwa ni moja na akafa. Alimaliza, alikuwa ni mwanamke nae alimaliza masomo yake. Form four. Niko na mtoto iko Lisangani Secondary hapa akiwa form one. Ange taka mtaka kwa watoto wa ndugu yake bwanake aliye marehemu, lakini hana msada wowote. Ana shukuru kwamba leo mme fika. Mnazi hainisaidi na lolote. Haina mnunuzi nazi haina mnunuzi, haina bei. Makuti hainunuliwi na mtu. Anauza pombe. Pia hakuna pombe, bei mzuri ya pombe. Ana uza pombe ili watoto wake wasome. Niko na kitinda mimba ambae iko darasa la tatu. Hasaidiwi na mtu yoyote. Mtoto wake alimaliza form four wakati ule Ford Party zilipo anza ku zungumuza, mpaka sasa haja pata kazi. Iko college mtoto huyo. Bado ana daiwa pesa huko shule. Ana uza mbuzi ili ajisaidie. Ana chukua ile lorry ana enda kuzunguka kwa walevi, na wengine wana mlipa, wengine hawamlipi. Hakuna msada wowote. Watoto wa bwana yake mkubwa, wana taka kumchomea nyumba, wana sema yeye ame kuwa pia na pato. Alipo kwenda form one mtoto wake, kwa jumla yeye ana teseka kwa kila njia.

Ana taka katiba iendelee kwa andikwa. Ifikirie mtu kama yeye, mwengine aliyeko. Pili, mtu akisome akimaliza, ajue ni wapi ataenda ambapo ataenda kufanya kazi. Tatu, mtoto wake akipata kazi na yeye ata pata kupumzika. Ame kuja lakini yeye ni

mgonjwa. Lakini aliambiwa mukutano ni mzuri. Akaseme lazima aje. Ame enda kusaidia wanawake wengine katika kikundi. Ame seme yeye ni mwalimu wao wakilimo. Lakini haja fanikiwa. Alienda Uganda huyu mama, na alizaliwa chasimba. Hapa ni bandara salama. Aliolewa chasimba. Hana baba, lakini mama iko naye. Hana bwana, mkubwa mtoto wa kiume ni moja. Niko na wasichana watatu.

**Interjection – Com Lethome –** Bwana akikufa haku waachia kitu chochote?

**Mbwana –** Alimuachia minazi, iko na shamba ambao wana endelea kulima.

**Com. Lethome -** Kuna mtu yoyote ambaye ali mingilia hio mali aliwachiwa?

**Mbwana –** Niko naye mtu ambaye ana mzumbua kwa sababu …

**Com Lethome –** (inaudible)

**Mbwana –** Yuko nao, wako hapo nyumbani. Watoto wa bwana ake mkuu.

**Com. Lenaola** - Lakini yeye haku lazimishwa kufanya ile kuhalwa?

**Mbwana** - Ali lazimishwa na aka kubali. Lakini sasa..

**Com. – Lethome** - Lakini ana endelea nayo ama vipi?

**Mbwana** - Hakuna watu wachukuliwe,

**Com. Lethome –** Aki maliza aishie?.

**Mbwana** - Eh aishe. Ana sema wale mabwana wanaowa, Ana sema ile mwana akingowa ufa tena hakuna msada wowote ambao ana kuja nao. Ana kuja tu mwili wake pekeyake. Ana omba kama kuna serikali ya Majimbo ambo ita fanya kazi, ifanye kazi sawa, isaidie mtu kama yeye. Ita saidia mtoto wake, hata watoto wa hawa wengine.

**Com.Lenaola** - Amborose kazungu

**Mr. Amborose Kazungu** - Mimi ni Ambrose Kazungu. Ninge taka serikali iwe ya Majimbo. Ikiwa Majimbo, hospital zetu huku ziwe zika hudumia watu bure. Na kiwanda chetu cha korosho hapa ilifungua kutoka mwaka juzi na tuna shida na kazi

hapa pwani, sisi vijana.

**Com. Lenaola** - Pendekeza.

**Mr. Kazungu** – Ninge pemdekeza mkorosho wafunguliwe kile kiwanda cha mkorosho, watu wa pwani wapate kazi kama vijana wa hapa. Na mashamba yetu iwe ita pimwa hapa huku kwetu, tupate title deed. Na barabara ziwe ziwekwa lami huku kwetu, ka sababu tuki pata mavuno shambani, tuna shida ya kuyapeleka nyumbani kwa shauri ya barabara mbaya. Kwa hayo machache, nina omba asanteni.

**Com. Lenaola** – Asante sana bwana kazungu. Kazungu, njoo pale.

**Mandas Bandari** – Mimi naitwa Mandas Badari kutoka Chwonyi. Maoni yangu nili kuwa nataka serikali iwe ya majimbo. Na kusema nataka serikali ya majimbo nilikuwa najua huduma zetu ita kuwa karibu na sisi. Sisi watu wa Pwani na wabara, tunaona kwenda bara ni mbali na huduma zetu zina chelewa hapa. La pili nataka serikali ya majimbo ita kuwa na viongozi amboa tuna weza kuwaona sisi wenyewe hapa karibu. Manake tuna waziri ni mtu ambaye humjui hata kwao kuzaliwa. Kuna mjumbe ndio tuna muona tuna mchagua lakini huduma zake hazi tutoshi. Maanake yeye yuko hapa, na ana wakilisha Kenya nzima. Kwa hivyo, akiwa karibu hapa, ama kwa jimbo letu tutakuwa tuna uwezo wa kumuona, na kumwambia vilio zetu ambazo tuko nazo.

Pia tuna taka huduma zetu pia ni kama hospitali. Hatuna hosipitali ambao ni ya kutusaidia zaidi hapa, isipokuwa ni dispensary na health centre. Wakati wa Majimbo, tuna uwezo wa kufanya mchango sisi wenyewe na tuka jenge hospitali ambayo ina weza kutusaidia. Kuna akina mama hua na shida hata ya kuzaa hapa. Tuko hapa na cliniki tu hapa ya mission. Na mtu akija hapa, uwezo wa hawa wako hapa wameandikwa, hawa wezi kuzalisha mtu kama huyo. Ina tubidi tupeleke mama mpaka Kilifi, na barabara zetu ni chafu.

Magari yenyewe tunao pata hapa pia hai tusaidia manake ni matatu na katika njia ya kuelekea kwa hospitali haina gari ya kumchukua.

Na masikuli yetu pia tuna taka yawe ata kuwa yana jengwa kimodern kama zile skuli zetu zingine. Maanake sikuli zetu, tuna jenga kama hizi tume kaa, lakini madawaji wenyewe, sisi wenyewe tuna pigania lakini hatuwwezi, hatuna uwezo zaidi. Ukiwa huduma iko karibu tuna weza kumuona yule officer ama waziri wa elimu aje atuelekeze tuende muelekeo wa kutengeneza hio msada. Nafikiri sikujirayarisha sawa, sawa, kwa hivyo kwa hayo machache, nina sema asante.

**Com. Lenaola** –Asante sana bwana bandari. Sasa watu wa Chwonyi, tume kamilisha kikao na ninge penda ku washukuru wale wame kuja, maoni yenu mazuri, na sasa ninge muomba mmoja wenu atuombe ili tufunge kikao halafu tuta rudi siku

nyingine. Ni nani ana tuombea? Nafikiri ukiomba si mbaya? Haya.

**Maombi -** Mungu mwenye huweza tunakushukuru ewe Mtukufu kwa jinzi Ulivyo tupa watu wako kufika sehemu hii. Mungu tuna kushukuru pia kwa kuongoza Kamishionas zetu ambao wana kazi ngumu katika jamhuri yetu. Lakini Mungu tunakuomba uwape nguvu siku baada sikuingine ili watimize kazi hii ambaye ita kuwa ni urithi letu hata kidacho (inaudible) Sasa Uwaongoze wanapo rudi ili kwamba Baba Uwalete upande hii siku zingine, chini wa uongozi wako. Baba Upawe vyema, Ukawatangulie mbele na wao kapo fika mahali popote Baba uta pata uajibu wako. Kwa Jina la Bwana wetu Yesu Christo, tume omba na Kuamini – Amen.

Meeting ended at 5.30 p.m.

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&**